**11 APRILI, 2023**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

### Kikao cha Nne – Tarehe 11 Aprili, 2023

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

### MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mkutano wetu wa Kumi na Moja Kikao cha Nne na tunaanza na maswali Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Athuman Almas Maige Mbunge wa Tabora Kaskazini aulize swali lake.

Na. 39

**Uhitaji wa ujenzi wa barabara ya Manoleo – Kituo cha Afya Upuge**

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE** aliuliza: -

Je, ni lini Barabara ya Manoleo hadi Kituo cha Afya Upuge itajengwa kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Athuman Almas Maige, Mbunge wa Jimbo la Tabora Kaskazini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Manoleo - Kituo cha Afya Upuge yenye urefu wa kilometa 22.10 imesajiliwa kwa jina la Nyambele – Upuge – Muhogwe - Magiri ambapo kutokana na umuhimu wake imeendelea kutunzwa kwa kuwekewa kipaumbele kwenye bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa barabara hii, Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 400 kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha changarawe kilometa 13 na kujenga makalavati saba, ambapo ipo hatua ya uandaaji wa nyaraka za zabuni kwa ajili ya kumpata Mkandarasi. Ujenzi unatarajiwa kuanza mwezi Mei, 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutafuta fedha ili Barabara ya Nyambele – Upuge – Muhogwe – Magiri yenye urefu wa kilometa 22.10 iweze kujengwa kwa kiwango cha lami. Aidha, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali itatenga shilingi milioni 91.8 kwa ajili ya matengenezo ya kawaida kilometa 15, ujenzi kwa kiwango cha changarawe kilomita mbili na kunyanyua tuta na kujenga makalvati mawili, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Athuman Almas Maige swali la nyongeza.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Waziri kwa majibu mazuri ya Serikali; nina maswali mawili ya nyongeza.

Je, Serikali iko tayari kukipa kipaumbele kipande kile cha kilomita nne kutoka barabara kuu ya Nzega kwenda kituoni ili kiweze kufikika wakati wa dharura?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Je, Serikali sasa iko tayari kumalizia kipande cha barabara kinachotokea pale kituo cha afya kwenda Kijiji cha Kasenga, Majengo, Ikongolo, Ipuge; vilevile vijiji vya Izugawima, na Nzuguka ili wananchi wa vijiji vile waweze kupata huduma haraka kwenye Kituo cha Afya cha Upuge?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Athuman Almas Maige, Mbunge wa Jimbo la Tabora Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iko tayari kuipa kipaumbele barabara hiyo ya kilomita nne ili kuweza kusogeza huduma za jamii kwa wananchi. Nimwelekeze Meneja wa *TARURA* wa Halmashauri ya Uyuwi kuhakikisha kwamba wanatenga fedha kwenye eneo hilo, kwa maana ya kuipa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kwa kuwa barabara hii ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja, ambayo inaunganisha kituo cha afya na vijiji kadhaa alivyovitaja ni muhimu kuwawezesha wananchi kupata huduma za afya

Serikali iko tayari kuipa kipaumbele barabara hii ili iweze kujengwa na kupitika vizuri. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ritta Kabati nimekuona, Mheshimiwa Hasunga atafata.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, je, ni lini barabara ya Ihanda-Ipunga hadi Chinji itajengwa kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza ya Mheshimiwa Hasunga, Mbunge wa Jimbo la Vwawa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilishawaelekeza mameneja wa *TARURA* katika wilaya zetu kuhakikisha wanatenga vipaumbele vya barabara ambazo zinahitaji kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo naomba nimwelekeze Meneja wa *TARURA* wa Wilaya hii ya Mbozi kuhakikisha kwamba wanaleta maombi hayo kama ni kipaumbele ili Serikali iweze kufanya tathmini na kuona uwezekano wa kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi huo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ritta Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Lini Serikali itatenga fedha za kutosha ili barabara inayotoka Mtandika kwenda Ikula iweze kujengwa kwa sababu barabara ile ni hatarishi sana na wakati wa mvua haipitiki wanawake wajawazito wanapandishwa mshikaki kwenda katika kituo cha afya kujifungua?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza ya Mheshimiwa Ritta Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii barabara ya kutoka Mtandika kwenda Igula na vijiji ambavyo amevitaja Mheshimiwa Mbunge ni kweli ni barabara muhimu na inapelekea wananchi kufika kwenye kituo cha afya kwa ajili ya huduma za afya. Kwa hivyo Serikali itaendelea kufanya tathmini ya gharama zinazohitajika ili fedha iweze kutafutwa na kuiboresha barabara hiyo ili kipindi cha masika iweze kupitika vizuri na wananchi waweze kupata huduma nzuri za usafiri, ahsante.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Hassan Seleman Mtanga Mbunge wa Mtwara Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 40

**Ujenzi wa Jengo la Manispaa – Mtwara Mikindani**

**MHE. HASsAN S. MTENGA** aliuliza: -

Je, ni lini jengo la Manispaa ya Mtwara Mikindani litajengwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga, Mbunge wa Jimbo la Mtwara Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jengo la Utawala la Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara – Mikindani lilijengwa mwaka 1948. Hivyo, jengo hilo limechakaa na halitoshelezi mahitaji ya Ofisi. Serikali inatambua umuhimu wa Halmashauri hiyo kujengewa jengo jipya kwa matumizi ya Ofisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Novemba, 2022 Halmashauri iliwasilisha maombi ya kutengewa bajeti katika mwaka wa fedha 2023/2024 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la utawala na nyumba ya Mkurugenzi. Serikali itatenga bajeti ya shilingi milioni 180 katika mwaka wa fedha 2023/2024 kwa ajili ya ujenzi wa Nyumba ya Mkurugenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa sasa Serikali imeweka kipaumbele cha kukamilisha majengo ya utawala yaliyoanza kujengwa kisha itaendelea na ujenzi wa majengo mapya ya utawala likiwemo jengo la Halmashauri ya Mtwara Mikindani. Ahsante

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hassan Mtenga.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nishukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Nina swali moja la nyongeza. Iliundwa tume ya kuja kuangalia jengo lile la Mtwara tangu mwaka 2020 na tume ile ikapendekeza kwamba jengo lile lisitumike;

Je, ni lini sasa Seriali itaamua kutuletea fedha ili tuweze kupanga sehemu nyingine kwa sababu jengo lile haliko salama sasa kwa wafanyakazi waliopo mule ndani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga, Mbunge wa Jimbo la Mtwara Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimwakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua kwamba jengo lile ni la siku nyingi na ni chakavu na kwa kweli halina sifa ya kuendelea kutumika kama jengo la halmashauri. Hivyo, Serikali imeweka kipaumbele baada ya kukamilisha majengo haya ambayo mengi yako katika hatua za ukamilishaji katika halmashauri zile mpya, tutakwenda kwenye halmashauri kongwe ikiwepo Halmashauri ya Mtwara Mikindani na nimwakikishie kwamba tutahakikisha kwamba Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa jengo hilo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kunipa kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga ni halmashauri kongwe na jengo la utawala halijakamilika. Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa jengo la utawala Halmashauri ya Shinyanga?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Serikali ilipeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa jengo la utawala katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga. Tunafahamu jengo lile halijakamilika, lakini ujenzi huu unakwenda kwa awamu. Awamu ya kwanza fedha zimepelekwa na kazi ya ujenzi imeanza. Nimwakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatafuta fedha ili ipeleke awamu ya pili kwa ajili ya ukamilishaji wa jengo hilo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Jengo la Halmashauri ya Rungwe ni jengo la muda mrefu sana.

Ni lini Serikali itatupatia fedha angalau kufanya ukarabati na kuongezea baadhi ya vyumba ili kuwawezesha wafanyakazi wafanye kazi vizuri?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilitoa maelekezo kwa wakurugenzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwamba pamoja na kutegemea fedha kutoka Serikali kuu lakini wanao wajibu wa kutenga fedha kupitia mapato ya ndani kwa ajili ya ukarabati mdogo mdogo pia kuongeza vyumba viwili, vitatu katika majengo ya utawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nina uhakika kwamba Halmashauri ya Rungwe wana uwezo wa kufanya

ukarabati wa majengo yale nitumie fursa hii kumwelekeza Mkurugenzi kuanza kuweka kipaumbele kwa awamu kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya halmashauri na pia kuongeza vyumba vichache ambavyo vinahitajika, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Natambua Serikali imekuwa ikitenga fedha katika ujenzi wa hospitali wa halmashauri ya Mji wa Bunda. Sasa ningependa kusikia kwa mwaka huu wa fedha nini tamko la Serikali ili hospitali ile iweze kumalizika haraka?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ester Bulaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa hospitali za halmashauri ikiwemo hospitali ya Halmashauri ya Bunda unakwenda kwa awamu. Kuna awamu ya kwanza ambapo fedha zilipelekwa, awamu ya pili majengo yapo yaliyokamilika na yako ambayo hayajakamilika. Nimhakikishie kwamba Serikali imeweka mpango mkakati wa kuhakikisha inatafuta fedha kwa awamu zinazofuata ili hospitali hizi zote zikamilike na kuwa na miundombinu inayotakiwa kutoa huduma kwa wananchi na hospitali hii ya Bunda pia itapewa kipaumbele.

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea na Mheshimiwa Lucy John Sabu Mbunge wa Viti Maalum aulize swali lake.

Na. 41

**Hitaji la ukarabati Hospitali ya Bariadi**

**MHE. LUCY J. SABU** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya ukarabati wa miundombinu ya Hospitali ya Mji wa Bariadi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI) naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucy John Sabu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kutenga bajeti kwa ajili ya ukarabati wa hospitali kongwe nchini. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imetenga fedha shilingi bilioni 17.1 kwa ajili ya ukarabati wa hospitali 19, ikwemo Hospitali ya Mji wa Bariadi. Aidha, hadi kufikia mwezi Februari, 2023 kiasi cha shilingi bilioni 12.95 zimekwishatolewa kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya hospitali kongwe 14 ambapo hospitali ya Mji wa Bariadi imepelekewa shilingi milioni 900 na kazi za ujenzi zinaendelea, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lucy John Sabu swali la nyongeza.

**MHE. LUCY J. SABU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa fursa hii, naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza nishukuru Serikali kwa kupeleka fedha katika majengo ya *OPD* na upasuaji lakini Hospitali ya Mji wa

Bariadi bado ina majengo mengi chakavu ikiwemo jengo la wagonjwa mahututi pia na majengo ya wodi;

Je, Serikali ina mpango gani wa kuyakarabati ili yaweze kutoa huduma bora kwa wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Hospitali ya Mji wa Bariadi ina changamoto ya upungufu wa wauguzi na madaktari; je, Serikali inatoa tamko gani juu ya upungufu huu? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Lucy John Sabu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Hospitali ya Mji wa Bariadi ni hospitali kongwe na ndiyo maana Serikali iliona umuhimu wa kupeleka shilingi milioni 900 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa majengo ya upasuaji, na jengo la *OPD*. Zoezi hili la ukarabati na upanuzi wa hospitali ile ni endelevu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kila mara Serikali itakuwa inatenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa hospitali kongwe basi Hospitali wa Mji wa Bariadi pia itapewa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni kweli kumekuwa na upungufu wa watumishi wa sekta ya afya katika Halmashauri wa Mji wa Bariadi. Hata hivyo, mwaka uliopita Serikali ilipeleka watumishi. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba zoezi la kupeleka watumishi kila kibali cha ajira kinapotoka Halmashauri ya Bariadi pia itapewa watumishi hao, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Festo Sanga nimekuona.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi, naomba niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Matamba kinahudumia Kata tano za Kinyika, Matamba, Mlondwe, Itundu na Mfumbi. Kituo hiki kina zaidi ya miaka 30 hakijakarabatiwa.

Je, ni lini Serikali itakarabati kituo hiki ili kiweze kupata majengo mapya ikiwemo mochwari ambapo wananchi wanatumia Wilaya ya Mlale?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. FESTO J. DUGANGE)**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza ya Mheshimiwa Festo Sanga Mbunge wa Jimbo la Makete, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Kituo cha Afya cha Matamba ni cha muda mrefu na ni tegemeo la wananchi kutoka katika kata takribani tano katika Wilaya ya Makete. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imekwishaainisha vituo vya afya vikongwe na chakavu na vyenye upungufu wa miundombinu kwa ajili ya kupeleka fedha kwa awamu kwa ajili ya kukarabati na kuvipanua. Kwa hiyo tutatoa kipaumbele pia katika kituo hiki cha Matamba kwa kadri ya bajeti ambavyo tunakwenda kuipanga; ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abbas Tarimba.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana. Pale katika Jimbo la Kinondoni kwenye Kata ya Kigogo Serikali ilituletea jokofu la kuhifadhia maiti lakini limekaa zaidi ya miaka mitatu sasa bila ya kuweza kujengewa eneo lake ilhali tathmini imeshafanyika;

Je, sasa Serikali imepanga kutoa lini fedha ili nyumba zilizokaribu pale ziweze kufidiwa na jengo lile likaanza kujengwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza ya Mheshimiwa Abbas Tarimba, Mbunge wa Jimbo la Kinondoni, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Kituo cha Afya cha Kigogo kilipelekewa jokofu lakini Serikali ilielekeza mara vifaa tiba vinavyofikishwa katika vituo vyetu vianze kutumika mapema iwezekanavyo. Kwa hiyo kwanza nitumie fursa hii kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni kuhakikisha kwamba wanatenga fedha kwa ajili ya kujenga jengo la kuhifadhia maiti na kuingiza jokofu ili lianze kufanya kazi ya kuhudumia wananchi kama inavyotarajiwa, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa majibu hayo tunaendelea na Wizara ya Kilimo Mheshimiwa Oran Manase Njeza Mbunge wa Mbeya Vijijini sasa aulize swali lake.

Na. 42

**Kupanda kwa bei za bidhaa za kilimo nchini**

**MHE. ORAN M. NJEZA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kukabiliana na kupanda kwa bei za pembejeo  za kilimo ikiwemo mbolea?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Oran Manase Njeza Mbunge wa Mbeya Vijijini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imepanga mikakati ya muda mfupi, kati na ya muda mrefu katika kukabiliana na kupanda kwa bei za mbolea hapa nchini. Mikakati hiyo ni pamoja na kutekeleza Mpango wa Utoaji Ruzuku ya Mbolea kwa wakulima msimu wa 2022/2023, kuhimiza matumizi ya mbolea mbadala wa *DAP* na *UREA* kama vile *NPK, NPS, NPS-zinc*, Minjingu, mbolea za asili na chokaa, kupunguza gharama za meli kukaa bandarini ambazo pengine mwisho wake hujumuishwa kwenye mjengeko wa bei ya mbolea, kuhimiza wafanyabiashara wa mbolea kutumia njia ya reli ya *TAZARA* na Reli ya Kati kusafirisha mbolea kwa wingi kwenda mikoani na kuhamasisha uwekezaji katika kuzalisha mbolea ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kupitia mpango wa ruzuku ya mbolea, Serikali imeweka bei elekezi ili kuwawezesha wakulima kununua mbolea za *DAP*, Urea na NPK kwa Shilingi 70,000 kwa mfuko wa kilo 50, Shilingi 60,000 kwa mfuko wa kilo 50 wa mbolea ya *CAN* na Shilingi 50,000 kwa mfuko wa kilo 50 wa mbolea ya *SA*. Aidha, Serikali inaendelea kushirikiana na Sekta Binafsi vikiwemo viwanda vya *Minjingu Mines and Fertilizer Limited* na *Itracom Fertilizers Limited* kuhakikisha uzalishaji na upatikanaji wa mbolea hapa nchini kwa gharama nafuu unaimarika na kupunguza utegemezi wa kuagiza mbolea kutoka nje ya nchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Oran Manase Njeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza na pia napenda nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa jibu lake zuri na pia kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa kutoa ruzuku kwenye pembejeo za kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mikakati mizuri iliyowekwa na Serikali lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, hiyo mikakati hasa utoaji wa ruzuku utakuwa ni endelevu kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa sababu ruzuku ilikuwa kwenye mbolea lakini kuna pembejeo zingine kama mbegu hasa za nafaka, je, Serikali ina mkakati gani pia wa kutoa ruzuku kwenye pembejeo aina ya mbegu pamoja na viatilifu kwa ajili ya kilimo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa ruzuku ya mbolea unategemeana sana na bei ya mbolea duniani na namna ambavyo wakulima wetu wataweza kumudu gharama hizo. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mpango huu ni endelevu kwa muda wa miaka mitatu na tutakuwa tunaendelea kuangalia bei za dunia na kama ikitokea kwamba wakulima wanazimudu gharama, mpango huu pia hautaendelea kwa sababu ni mpango wa kumsaidia kumlima kuondokana na machungu ambayo ameyapata kutokana na kupanda kwa bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kuhusu mbegu za nafaka. Moja kati ya mkakati wa Serikali ni kuhakikisha

kwamba, tunawafikia wakulima na kuwafanya wakulima wetu waweze kuzalisha kwa tija na eneo mojawapo ambalo tumekuwa tukiliangalia ni ruzuku kwenye eneo la mbegu na katika mwaka huu wa fedha tumefanya katika zao la ngano. Vilevile katika mahindi kupitia Wakala wa Mbegu Kilimo Tanzania, tumefanya hivyo kwa kushusha bei ambayo ni tofauti na bei iliyoko sokoni. Kwa mfano Mbegu za *OPV* za *STUKA M1* zinapatika kwa Sh.2,750 tofauti na bei ilivyo sokoni, lakini mbegu za *high breed* za *UH* 6303 inauzwa kwa Sh.4,000 tofauti na bei iliyoko sokoni ya Sh.7,000, kwa hiyo ni sehemu pia ya ruzuku.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Benki ya Kilimo Tanzania imekasimu madaraka yake kwa Benki mbalimbali ikiwemo *CRDB* pamoja na *NMB* kwa ajili ya utoaji mikopo, lakini masharti yaliyokuwepo katika ukopaji huo ni magumu sana ikiwepo na kutoa asilimia ishirini na tano ya kile unachotaka kukopa, kutoa dhamana ya nyumba pamoja na *cash flow* ambayo inaelea katika benki ya mwaka mmoja. Je, ni lini sasa Serikali itapunguza masharti haya ili wakulima wapate nafuu kwa ajili ya kilimo na hasa wakulima wangu wa Bagamoyo ambao ni maskini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikiri ni kweli kumekuwa na changamoto ya wakulima wetu kukopesheka kirahisi na ndiyo maana Serikali tumechukua hatua madhubuti za kuhakikisha kwamba tunakaa na taasisi za fedha waelewe mfumo wa ukopeshaji katika kilimo ambao ni tofauti na maeneo mengine. Kwa hivi sasa tumekuja na mfumo mzuri

ambao tumeu–*design* mikataba ya utatu ambayo imetusaidia sana kupunguza masharti mengi ambapo anakaa mkulima, anakaa *off taker*, anakaa na benki kwa upande mmoja ili mkulima aweze kukopesheka kutumia mikataba aliyonayo pasipo kutumia hati za nyumba na sababu zingine ambazo zinamfanya asiweze kufikia kwenye ukopeshwaji huo. Kwa hiyo nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge, kama Serikali tumeliona hilo na tunaendelea na mikakati hii kuhakikisha kwamba mkulima wetu anakopesheka kirahisi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anne Kilango Malecela.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naipongeza sana Serikali, naishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi kutupatia mbolea ya ruzuku kipindi hiki. Hata hivyo, mbolea ile Jimboni kwangu ilifikia tu kwenye Makao Makuu ya Jimbo na wananchi wote kwenye Jimbo zima walikuwa wanasafiri kuifuata Mbungu. Je, Serikali ina mpango gani wa uhakika kwamba kipindi kijacho mbolea hii itafika sehemu zote ambako wananchi wanalima? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli wakati tunaanza mfumo huu kwa mara ya kwanza, tumepitia changamoto hizo, lakini kama Wizara tumekaa, tumetafakari na kuzipitia changamoto zote na kuja na mkakati wa kudumu wa kuhakikisha kwamba mbolea hizi zinawafikia wakulima katika maeneo yao pasipo kutembea umbali mrefu. Mkakati huo ni kama ifuatavyo:-

(i) Hivi sasa tumeshawaagiza *TFRA* kuendele kusajili vituo vya mawakala karibu na maeneo ya wakulima;

(ii) Tutatumia pia Vyama vya Ushirika kwa ajili ya usambazaji wa mbolea; na

(iii) Tunatumia maghala ya Serikali yaliyoko katika maeneo mbalimbali kuhakikisha kwamba mbolea inafika katika maeneo ya uzalishaji ili wakulima wasitembee umbali mrefu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, Naibu Waziri, Wizara ya Kilimo, nakushukuru sana kwa majibu hayo.

Tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo, Mbunge wa Kishapu aulize swali lake.

Na. 43

**Mradi wa umeme wa nguvu ya jua Kata ya Talaga – Kishapu**

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO** aliuliza:-

Je, ni lini Mradi wa Umeme wa Nguvu ya Jua utaanza kutekelezwa katika Kata ya Talaga Wilayani Kishapu?

**MWENYEKITI:**Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo, Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa Mradi wa Umeme wa Jua katika Kijiji cha Ngunga, Kata ya Talaga, Wilayani Kishapu unalenga kuzalisha umeme kwa kutumia jua kiasi cha megawati 150 kwa gharama za *Euro* milioni 115.30 ambayo itakuwa ni megawatli 50 na *Euro* milioni 42 kwa awamu ya kwanza na megawati 100 kwa *Euro* milioni 62 kwa awamu ya pili. Fedha za awamu ya kwanza tayari zimepatikana, taratibu za kumpata Mkandarasi Mshauri na Mjenzi zipo katika hatua za mwisho. Fedha ya awamu ya pili inaendelea kutafutwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malipo kwa ajili ya fidia kwa wananchi wa Kijiji cha Ngunga watakaoathirika na mradi, kiasi cha shilingi bilioni 1,825 kitaanza kulipwa mwishoni mwa mwezi Aprili, 2023 na Ujenzi wa Mradi huu (awamu ya kwanza) utatekelezwa kwa kipindi cha miezi kumi na nne (14) kuanzia mwezi Juni, 2023, baada ya kukamilisha taratibu za manunuzi ya wakandarasi na malipo ya fidia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Boniphace Butondo.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napongeza Serikali kwa majibu mazuri juu ya hatua ya mwendelezo wa Mradi huu muhimu wa uzalishaji wa umeme wa jua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni moja tu la nyongeza, kwamba ni kwa namna gani zana ya ushirikishwaji wa jamii inayohusika na hasa juu ya masuala ya fidia, imekuwa ikizingatiwa lakini pia suala zima la uongozi hasa wa ngazi za chini Serikali za Mitaa umekuwa ukihusishwa hili kuona kwamba michakato ya haki na tathmini iliyo halali kwa ajili ya malipo kwa wananchi inazingatiwa? Naomba kujibiwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Butondo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Butondo kwa kulifuatilia jambo hili mara kwa mara, lakini namhakikishia kwamba kama anavyofahamu na anavyoona limefikia mwisho na mambo yanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye jibu la msingi nimesema malipo ya fidia yataanza kufanyika mwishoni mwa mwezi huu, lakini taratibu zote zote za fidia zimepitiwa kama ambavyo zinaelekezwa na sheria. Kwa hiyo wale wataoathirika wote tayari wamebainishwa na wameshirikishwa katika mchakato huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo jambo zuri sana ambalo naomba kulisema kwa sababu ya uhitaji mkubwa wa umeme tuliokuwanao tumekubaliana na wenzetu wa *TANESCO* na Serikali imewaagiza watoe pesa zao kwanza kuanza kulipa fidia haraka kama mkopo, halafu badae Wizara ya Fedha itakapokuwa imelipwa watarudishiwa kwenye eneo lao. Kwa hiyo wiki hii ambayo tumeianza jana wananchi kule wataanza kulipwa fidia katika mazingira yao ili kuhakikisha kwamba mradi hii unakimbizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaelekeza wenzetu wa *TANESCO* watakapoenda kulipa fidia kupitia halmashauri, kupitia Serikali za Vijiji na Viongozi wetu wa Serikali waliokuwa nao washirikiane hili kuwabaini wale ambao ni waathirika halisi na waweze kupewa haki yao stahiki kwa mujibu wa sheria hili mradi uweze kutkelezwa bila tatizo lolote.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Selemani Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwa kunipa nafasi. Mradi wa *REA* wa vijiji 26 Wilaya

ya Tanganyika ambao Mheshimiwa Naibu Waziri, alikuja akauzindia mpaka sasa haujakamilika. Je, ni lini Serikali itakamilisha ule mradi ili uweze kuleta tija kwa wananchi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Selemani Kakoso, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nilienda kuzindua Mradi huo mimi mwenyewe na Mkandarasi anayetekeleza Mradi huo Mkandarasi wa ITIBIKO bado anaendelea na kazi *site* na makubaliano tuliyokuwanayo ni kufikia Desemba mwaka huu mradi huu pamoja na miradi mingine yote ya kupeleka umeme vijijini iwe imekamilika. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Kakoso kwamba jambo hili tunalifuatilia na kabla ya mwaka huu kwisha tutahakikisha ya kwamba kazi hiyo inakamilika katika eneo lake la Wilaya ya Tanganyika lakini na maeneo mengine.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum. *(Makofi)*

Na. 44

**Kufungua vituo vya kuuza gesi asilia**

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufungua vituo vingi zaidi vya kuuza gesi asilia?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiachana na usambazaji wa gesi asilia kwa kutumia bomba la kusafirisha gesi Mtwara, Lindi, Pwani na Dar es Salaam, kuna vituo vitatu vya kugandamiza na kuuza gesi asilia nchini *(Compressed Natural Gas (CNG) Stations)* ambapo Dar es Salaam viko viwili (2) na Mtwara kipo kimoja (1). Vituo viwili vinamilikiwa na wawekezaji binafsi na kimoja ni ubia wa Serikali na Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2022/2023, Serikali imempata Mkandarasi wa ujenzi wa vituo vitatu (3) vya *(CNG)* na kazi hiyo itaanza kabla ya mwaka huu wa fedha kwisha. Vilevile, kituo kimoja (1) kitajengwa na mwekezaji binafsi (Dangote) eneo la Mkuranga, Pwani. Aidha, Serikali imeshatoa idhini kwa kampuni binafsi 20 kujenga vituo vya kujaza gesi katika magari. Kampuni hizo zipo katika hatua mbalimbali za kupata vibali vya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Serikali imepanga kujenga vituo vya *CNG* katika Bohari Kuu za Serikali za Dar es Salaam na Dodoma ili kuwezesha magari ya Serikali na watu binafsi yanayoendelea kuunganishwa na mfumo wa kutumia gesi asilia kuweza kupata nishati hiyo. Taratibu za utekelezaji wa mradi huu zinakamilishwa Serikalini ili utekelezaji uanze mara moja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bupe Mwakang'ta.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; Serikali sasa ina mpango gani wa

kuendelea kujenga vituo hivyo vya kuuza gesi asilia katika mikoa ya mingi Tanzania hususani Mkoa wa Rukwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Serikali sasa imejipangaje kupunguza bei ya vifaa vinavyotumika kurekebishia mfumo wa magari kwenye mafuta na kwenye *kit* ya kujazia gesi? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Bupe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwenye jibu la msingi kama nilivyosema Serikali imejipanga vipi kuongeza Vituo vya Kujaza *(CNG),* tayari vibali kwa wakandarasi na wawekezaji 20 vimetolewa kwa ajili ya kwenda katika maeneo mbalimbali kuweza kuongeza wigo wa eneo hili. Tunaendelea kuvutia wawekezaji mbalimbali waje kuwekeza katika eneo hili la gesi asili ambalo litakuwa linatumika katika maeneo mbalimbali. Kwa hiyo michakato hiyo inaendelea na Serikali katika mwaka huu wa fedha itajenga hivyo vituo vyetu viwili ambao tunaamini kabla ya mwaka huu wa fedha kwisha vitaanza utekelezaji wake maeneo ya Mlimani *City* na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali la pili, Serikali inafanya nini kuhakikisha bei ya hizi zinazoitwa *conversion kits* zinapungua. Mojawapo ya kitu tunachokifanya tunahamasisha watu wengi wanaoweza kuja katika biashara hii ya kutengeneza *conversion kits* waje, biashara ikisha kuwa na watu wengi wanaoshiriki *automatically* ushawishi utakuwa ni mkubwa na gharama tunatarajia zitapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile pia tumewaza namna ambayo tunaweza tukashirikiana na wenzetu wa Wizara

nyingine za Kisekta, Wizara ya Fedha na wengine kuona namna ya kuweka fedha au punguzo la kodi kwenye vifaa hivi kwa watalam watakavyoshauri ili tuone namna ambavyo tunaweza tukapunguza gharama za hizi *conversion kits* ili kuweza kuvutia watu wengi zaidi kuweza kuingia katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo la mwisho, tayari vituo vinavyouza gesi vimeweka utaratibu wa kukopesha wale wanaokuwa na haya magari wanaotaka kufanya *conversion kit* wanawakopesha na wanakuwa wanalipa kidogo kidogo kwa sharti la kwenda kuchukua gesi katika kituo chake hizo zote ni mbinu katika kuhakikisha kwamba gharama zinapungua na watumiaji wanaweza kupatikana kwa wingi.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Nancy Hassan Nyalusi, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 45

**Hitaji la umeme kwa vijiji nane vya Mufindi Kusini**

**MHE. NANCY H. NYALUSI** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itakamilisha usambazaji wa umeme katika Vijiji Nane vya Wilaya ya Mufindi ambavyo havijapata umeme?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nancy Hassan Nyalusi, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Mufindi ina jumla ya vijiji kumi tu ambavyo havina umeme na vinapatiwa umeme kupitia Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini, Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili, kupitia Mkandarasi anayeitwa *OK Electrical Services Limited.* Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 vijiji vinane vilikuwa vimeshapatiwa umeme na vijiji viwili (2) vijulikanavyo kwa majina ya Itika na Mpangatazara bado havijapatiwa umeme. Vijiji vyote vinatarajiwa kupatiwa umeme ifikapo mwezi Juni, 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nancy Hassan Nyalusi, swali la nyongeza.

**MHE. NANCY H. NYALUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Tunaishukuru Serikali kwa utekelezaji, hata hivyo, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, ni lini Serikali itakamilisha kupeleka umeme katika Kijiji cha Idunda na Funuti, Kata ya Kimara katika Wilaya ya Kilolo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; je, ni lini Serikali itaanza kusambaza umeme katika Vitongoji Mkoani Iringa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili nyongeza la Mheshimiwa Nancy Nyalusi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika jibu la msingi Vijiji vya Mufindi vitakamilika mwezi wa Sita mwaka huu kwa mujibu wa Mkataba, lakini vijiji vingine vyote nchini kama alivyovitaja yeye vya Kilolo kabla ya Desemba mwaka huu vitakuwa vimefikishiwa umeme kwa mujibu wa mkataba

wetu tuliokuwa nao kwenye *REA three, round two*. Kwa hiyo nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Nyalusi pamoja na Waheshimiwa wengine, kwamba jambo hili tunalisimamia kwa karibu zaidi kuhakikisha kwamba umeme unafika katika Vijiji vyote kabla ya mwaka huu kuisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la pili, tunaendelea kutafuta pesa ambayo itatuwezesha kupeleka umeme katika vitongoji vyote karibu 36,000 tulivyokuwa navyo nchi nzima katika miaka minne, mitano inayokuja kwa gharama ya Sh.6,500,000,000,000. Taratibu za kutafuta fedha hizi zinaendelea na zitakapokuwa tayari, basi zitaletwa kwa umma hili kazi hii iweze kufanyika na kuhakikisha vitongoji vyote vinapata umeme. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jackson Kiswaga na Mheshimiwa Deus Sangu, nimewaona.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mwezi Desemba Meneja Mkoa wa Iringa ndugu yangu Jumbe aliniahidi kupeleka umeme katika Kijiji cha Usengerenidete, mpaka sasa nimeshapelekwa kwenye vyombo vya habari mara nne, je, ni lini sasa *TANESCO* watatoa angalau fedha za dharura kutoka Makao Makuu watupelekee hili hao wananchi wapate umeme?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jackson Kiswaga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ameomba yeye mwenyewe fedha za dharura na jambo hili nilikuwa sijalipata naomba baada ya *session* hii ya maswali, niende kwake

tukajadiliane, nijue tatizo ni nini na tuweze kulitatua tatizo hilo ili wananchi waendelee kupata huduma hiyo ya umeme. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deus Sangu nilikutaja, Mheshimiwa Stanslaus Mabula atafuata.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa fursa ya swali dogo la nyongeza. Mkandarasi anayetekeleza Mradi wa *REA* ndani ya Mkoa wa Rukwa *speed* yake ni ya kusuasua sana, hususani ndani ya Jimbo langu la Kwela kufikia mwezi Machi katika vijiji 54 alikuwa amewasha vijiji tisa. Nataka kujua *comittment* ya Serikali leo ili wana Rukwa na Jimbo la Kwera wajue nini hatima yao kupata umeme? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Deus Sangu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe *comittment* ya Serikali kwamba ile mikataba yote ambayo ilitakiwa kwisha Desemba mwaka huu kwa wale wakandarasi ambao wanaendelea na kazi hizi, tutaendelea kuwasimamia kwa karibu zaidi. Tumeshawekeana *deadline* na *timeline* za mambo mbalimbali na wale ambao wanaendelea kuzikiuka taratibu ambazo tunazichukua za kisheria watazipata muda si mrefu. Kwa hiyo niwahakikishie kwamba watapata umeme kabla ya muda wa mkataba kwisha na wale ambao watashindwa tutachukua hatua mapema ili tuweze ku–*rescue situations* kupata wakandarasi wengine ambao watakamilisha upelekaji wa umeme katika miradi ambayo tumekubaliana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stanslaus Mabula.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa, zoezi la upelekaji umeme kwenye Miji na maeneo yanayofanana na Vijiji bado haijakamilika kama inavyotakiwa.

Je, ni lini, Serikali itahakikisha maeneo yote yaliyoko Mijini hasa kwenye Kata za Buhongwa, Runhima na Kishili yanapata umeme uliokusudiwa kwa wakati na wananchi waweze kufaidi matunda hayo?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Stanslaus Mabula, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli zimekuwepo awamu mbili za kupeleka umeme kwenye maeneo ya Mijini yenye picha ya Vijiji ambayo tunaita miradi ya *peri-urban,* katika Jiji letu la Mwanza awamu ya kwanza ilifika ambayo iligusa pia, maeneo ya Dar es Salaam, Arusha na Mwanza. Ipo awamu ya pili ambayo ilikuja Dodoma na Mbeya na sasa iko awamu ya tatu ambayo kuna baadhi ya maeneo tayari imeshaanza kufanyika, Mkoa wa Kagera Jimbo la Bukoba Mjini likiwa ni mojawapo Geita, Mbeya tena Tanga na maeneo mengine ambayo yana uso wa Vijiji lakini yako Mjini yanaendelea kupelekewa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuahidi Mheshimiwa Mabula pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine ambao Majimbo yao yako Mjini kwamba miradi hii inaendelea kufanyika kadri ya upatikanaji wa fedha awamu kwa awamu. Pale ambapo tunapambana kuhakikisha kwamba *REA III round II* inakamiliishwa kwenye vijiji, vivyo hivyo ndivyo

tunavyopambana kutafuta pesa kwa ajili ya kupeleka umeme katika maeneo ya Mijini lakini yenye uso wa Vijiji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Emmanuel Cherehani.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Serikali ina mkakati gani wa kuongeza Mkandarasi katika Wilaya ya Kahama yenye Halmashauri mbili Ushetu pamoja na Msalala kutokana na aliyepo kupeleka umeme kwa kusuasua sana?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cherehani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkandarasi anaepeleka umeme katika Wilaya ya Kahama ni Mkandarasi anayeitwa *Tontan* ambaye tunakiri ana mapungufu na hasa katika kazi yake anayoifanya Tanga na tumewekeana masharti ya kutimiza, akishindwa kuyatimiza mwezi huu wa Nne hautaisha ataondoka *site* zetu ili tuweze kupata Mkandarasi mwingine wa kupeleka umeme katika maeneo hayo. Kwa hiyo wananchi wa Kahama ninawaahidi kabisa kwamba umeme katika maeneo yao utapelekwa na utakamilika kwa wakati kwa sababu ni jambo linalotakiwa kukamilika kwa wakati.

**MWENYEKITI:** Tunamalizia na Mheshimiwa Flatei Massay.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali. Pamoja na Mkandarasi anayetekeleza kazi kwa Jimbo la Mbulu Vijijini kusuasua, sasa ameanza kuweka nguzo katika kila Kijiji, vingine nguzo 12, 13 na 15.

Je, ni kiasi gani cha nguzo kinatakiwa kiwekwe kila Kijiji ili sisi tusimamie?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Flatei, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa iliyokuwa imepatikana katika awamu ya kwanza ya *REA III round II* ilikuwa unawezesha nguzo takribani 20 kupelekwa katika kila Kijiji, lakini tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, alisikia kilio cha Watanzania na akatafuta pesa ya ziada na kuongeza, kwa hiyo kila Kijiji kitapata takribani kilomea Tatu ambazo ni 20 mara Tatu maana yake karibia nguzo 60 katika awamu hiyo inayokuja ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninawaahidi Waheshimiwa Wabunge wote kwamba kutoka nguzo 20 sasa tutapata nguzo 60 katika kila Kijiji kwa ajili ya kuongeza wigo wa upelekaji wa umeme katika maeneo hayo. Tunakamilisha taratibu za kusaini mikataba kwa Wakandarasi ambao wanaonekana wanaweza wakaongezewa kazi katika maeneo yao ili waongezewe katika kilometa Mbili ambazo wanatakiwa kuzifanya katika vijiji vyote ambavyo tunavimalizia katika mradi huu wa mwisho wa *REA III round II.*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Stephen Byabato, Naibu Waziri wa Nishati kwa majibu hayo. Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Robert Chacha Maboto, Mbunge wa Bunda Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 46

**Ujenzi wa Chuo cha VETA – Bunda**

**MHE. ROBERT C. MABOTO** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itajenga Chuo cha *VETA* katika Halmashauri ya Mji Bunda?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mhehsimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Robert Chacha Maboto, Mbunge wa Jimbo la Bunda Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni azma ya Serikali kujenga Chuo cha Ufundi Stadi katika kila Mkoa na Wilaya nchini. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imetenga kiasi cha Shilingi za Kitanzania Bilioni 100 kwa ajili ya kujenga Vyuo vya Ufundi Stadi katika Wilaya 64 ambazo zilikuwa hazijajengewa vyuo hivyo. Tayari Serikali imeshakamilisha kuandaa michoro na upatikanaji wa maeneo kwa ajili ya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Bunda ni miongoni mwa Wilaya 64 ambazo zipo katika mpango wa kuanza kujengewa Vyuo vya Ufundi Stadi katika mwaka huu wa fedha ambapo tayari kiasi cha Shilingi Milioni 45 kimetolewa mwezi Machi, 2023 kwa ajili ya shughuli za awali ikiwemo upimaji wa udongo kwa ajili ya uhimilivu pamoja na tathmini ya athari za mazingira na jamii wakati wa ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mhehsimiwa Robert Chacha Maboto, swali la nyongeza.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kutokana na majibu mazuri ya Serikali, sina swali la nyongeza isipokuwa namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuliona hilo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Catherine Magige, nilikuona.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakshukuru. Je, udahili wa wanafunzi kuingia *VETA* mpya iliyojengwa Wilayani Longido Mkoa wa Arusha unaanza lini?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mhehsimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vyuo 25 vya Wilaya, vile ambavyo tulijenga katika mwaka uliopita wa fedha, ambapo ukamilishaji wake hivi sasa ndio tunakwenda kukamilisha, tunatarajia udahili ule wa kozi zile za muda mrefu kuanza mwezi wa Kumi mwaka huu, ila zile kozi za muda mfupi muda wowote kuanzia mwezi wa Sita zinaweza zikaanza rasmi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Furaha Matondo.

**MHE. FURAHA N. MATONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa kila Wilaya imeandikiwa kupata chuo cha *VETA*. Je, ni lini Serikali itaboresha chuo cha *VETA* Buhongwa ili kiwe na hadhi ya chuo cha *VETA* katika Wilaya ya Nyamagana?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mhehsimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Matondo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni azma ya Serikali kuhakikisha kwanza tunakwenda kujenga kwenye maeneo ambayo hayana huduma au hayana vyuo hivyo, lakini kwenye maeneo ambayo vyuo tayari vipo ni azma vilevile ya Serikali kuhakikisha kwamba, vyuo vile tunakwenda kuviboresha kwa maana ya kufanya ukarabati lakini vilevile kuongeza miundombinu. Nimuondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu, kwamba Serikali inaandaa bajeti kila mwaka ile ya kufanya maendelezo kwenye maeneo mbalimbali ikiwemo na chuo hiki ambacho amekitaja Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, nimekuona.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi.

Kwa kuwa, Serikali yetu na nchi yetu inajikita zaidi katika matumizi ya teknolojia na TEHAMA. Je, Serikali ni lini itaona ni wakati muafaka wa kuongeza masomo haya ya sayansi ikiwemo hisabati kwa wanafunzi wanaofanya masomo ya HGKL. Ni ni lini ili kuwafanya watu hawa wawe tayari katika soko la ulimwengu na Tanzania?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Asha Mshua kama ifuatavyo: -

Mhehsimiwa Mwenyekiti, masomo ya hisabati pamoja na teknolojia tayari yapo kwenye mitaala yetu lakini naomba tu nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge, hivi sasa tunafanya mapitio ya mitaala katika ngazi zote za elimu ambapo tutazingatia hasahasa kwenye maeneo haya ya sayansi pamoja na teknolojia na tunaamini kabisa kwa mwendo huo tunaokwenda nao swali lake litakuwa limepata majibu ya jumla na ya moja kwa moja.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 47

**Elimu inayotolewa kuendana na mahitaji ya sasa**

**MHE. SYLVIA F. SIGULA** aliuliza: -

Je, ni nini mpango wa Serikali kuhakikisha elimu inayotolewa inaendana na mahitaji ya sasa?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali inaendelea na mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, sambamba na mapitio ya Mitaala ya Elimu katika ngazi zote.

Mabadiliko haya ya Sera na Mitaala yamelenga kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za kazi, stadi za maisha za karne ya 21 ambazo ni fikra tunduizi, ubunifu, ushirikiano, uongozi pamoja na stadi za mawasiliano na teknolojia ya habari kwa lengo la kuwajengea uwezo wahitimu kukabiliana na mabadiliko mbalimbali yanayotokea katika jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali upande wa Vyuo vya Kati na Vyuo vya Ufundi Stadi, Baraza la Elimu ya Ufundi *(NACTVET)* linaendelea na maandalizi ya *Occupational/Professional Standards* ambazo zitatoa mwogozo katika mabadiliko na maandalizi ya mitaala inayokidhi mahitaji ya sasa na baadae. Vilevile, kwa upande wa Elimu ya Juu tayari Tume ya Vyuo Vikuu *(TCU)* inaendelea kukusanya maoni ya wadau kuhusu ubora wa elimu inayotolewa na Vyuo Vikuu pamoja na kutoa mafunzo kwa Wahadhiri katika maandalizi ya mitaala inayozingatia mahitaji ya ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu suala la elimu ni suala nyeti katika Taifa letu, ni muda sasa Serikali imesema ipo kwenye mchakato wa mapitio na watoto wetu wanaendelea kutumia mtaala huu ambao hauna tija kwao. Ni lini hasa utekelezaji utaanza rasmi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, vijana wengi wameathiriwa na mfumo huu ambao hauna tija, wengi wapo mtaani na wanashindwa afanye nini kwa elimu walioipata. Je, ni upi mkakati wa Serikali wa kuwasaidia

vijana hawa ambao tayari ni wahanga wa mfumo wetu huu wa elimu pale tutakapobadilisha mfumo rasmi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Sylvia, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokwishaeleza kwenye majibu ya swali la msingi kwamba kwa upande wa upitiaji wa mitaala Serikali tayari tumekamilisha rasimu ya mitaala pamoja na sera yetu, hivi sasa tupo katika hatua za kurudisha tena kwa wadau lakini vilevile katika mamlaka mbalimbali ambazo zitathibitisha au zita- *approve* mitaala hiyo. Mara tu mchakato huo utakapokuwa umekamilika tunataraji mitaala hii itaanza kutumika rasmi kwenye ngazi zote za elimu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali lake la pili, anazungumzia kwamba tayari kuna wananfunzi ambao walitumia mitaala ile ya zamani. Naomba nimuhakiishie tu Mheshimiwa Mbunge, utaratibu wa upitiaji wa mitaala pamoja na sera ni suala endelevu ni suala ambalo linatokea mara kwa mara pale tunapoona tu kuna mahitajji ya mabadiliko ya mitaala pamoja na sera, Serikali imekua ikifanya hivyo ili elimu inayotolewa ilingane au iendane na mazingira halisi ya kazi au mazingira halisi ya dunia inavyokwenda. Vilevile utaratibu wetu au sera yetu ya elimu inampa wasaha yule mhitimu kuweza kujiendeleza au kwenda maeneo mengine na kupata elimu zaidi ambayo itaendana na mazingira yale ambayo anafanyia kazi. Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mhehsimiwa Noah Lemburis, nimekuona.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, kwa kuwa kumekuwepo na changamoto katika Shule za Msingi na Sekondari kwa ajili ya watoto kupata chakula shuleni. Nini kauli ya Serikali kuhusu watoto kupata chakula shuleni kwa ajili ya kuhakikisha kwamba watoto wanakuwa kwenye ufanisi mzuri kiakili na kimwili?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli suala la chakula shuleni kwa watoto ni jambo ambalo ni muhimu, bado kuna changamoto kubwa sana ya upatikanaji chakula mashuleni kwa ajili ya watoto wetu. Serikali tulishatoa mwongozo wa namna gani wazazi au walezi wanaweza kushirikiana na Serikali kuhakikisha kwamba watoto wetu wanapata chakula shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia mwongozo ule unadadavua na unatoa maelekezo mazuri kabisa kwamba kila upande ni namna gani unaweza kushiriki ili wanafunzi wetu waweze kupata chakula wanapokuwa shuleni. Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Omari Juma Kipanga, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa majibu hayo. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa John Marko Sallu, Mbunge wa Handeni Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 48

**Ujenzi wa barabara ya Turiani – Handeni kilometa 104**

**MHE. JOHN M. SALLU** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itamalizia ujenzi kwa kiwango cha lami kipande cha barabara ya Turiani hadi Handeni kilometa 104?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa John Marko Sallu, Mbunge wa Handeni Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa barabara hii inayoanzia Magole, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* imekamilisha ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya kuanzia Magole hadi Turiani yenye urefu wa kilometa 45.27, katika mwaka wa fedha 2022/2023 jumla ya shilingi bilioni moja zimetengwa kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ujenzi wa sehemu iliyobaki kati ya Turiani – Mziha hadi Handeni kilometa 104 kwa awamu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa John Marko Sallu.

**MHE. JOHN M. SALLU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, kwa hiyo wananchi wa Handeni tunategemea hivi karibuni michakato itaanza, nina swali moja la nyongeza.

Barabara itokayo Chalinze mpaka Segera, hasa kile kipande kinachoanzia Manga mpaka Segera zinatokea ajali nyingi sana na kupoteza nguvu kazi kubwa sana ya nchi hii,

na sababu kubwa ni wembamba wa barabara na kona nyingi.

Je, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kufanya maboresho kwenye barabara hiyo ili tuweze kuondoa vifo hivi vya wananchi wa kitanzania na majeruhi? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mhehsimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa John Marko Sallu, Mbunge wa Handeni Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mhshimia Mwenyekiti, barabara ya Chalinze hadi Segera ni barabara ambazo ni barabara *standard* kwa maana ina upana wa mita 6.5 kwa maana kila upande mita 3.25 na hizo ndiyo barabara zilizo nyingi. Ninatambua kwamba ni kweli kuna ajali nyingi zinataokea lakini ambacho tumekifanya tumetenga fedha kwa ajili ya kufanya *economic study* na usanifu wa barabara hiyo kwenye maeneo ya miinuko, kona na kuhakikisha kwamba barabara hii ipanuliwe hasa kwenye maeneo ambayo watu wameongezeka kwenye vijiji na kuongeza upana wa mabega.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafanya *economic study* na *feasibility study* ambayo tutaanza mara moja kwa ajili ya kupunguza ajali ili watu waweze kuonana kwa umbali, ni barabara ambayo imeinuka sana, ukilinganisha na yaani *embankment* yake ni ya juu. Kwa hiyo, hilo tumeshaliona na Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kufanya hiyo *study* na *economic study*. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, nimekuona.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa barabara ya *Kibosho Shine,* Kwa Raphael hadi *International School* kwa kiwango cha lami kwani ni kipande kidogo kimebakia?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo fupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema kipande kilichobaki kidogo nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua kazi kubwa imeshafanyika na tunatafuta fedha kuweza kukikamilisha hicho kipande kilichobaki cha barabara ili wananchi waweze kupata huduma ambayo imekusudiwa na Serikali. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam kisangi nimekuona.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga au kuboresha barabara inayotoka Chuo cha Diplomasia Kurasini kupitia *Tom Estate* kupitia Msikitini ka Mzuzuri mpaka kuunganisha na barabara ya Mandela? Kipande hicho ni korofi, makontena yanapita kwa shida sana ukiwa na gari ndogo unaweza ukafikiria sasa kontena linaniangukia, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa niaba ya

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kisangi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri tu kwamba sijaielewa vizuri hiyo barabara aliyoitaja lakini nimuombe pia Mheshimiwa Mbunge, kama ataridhia basi niweze kukutana naye ili niweze kuielewa hiyo barabara ili niweze kumpa hasa majibu sahihi badala ya kujibu tu. Sijaielewa vizuri hiyo barabara, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jesca nakuona.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumWuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, hiyo barabara ya *Iringa Bypass* ni mwaka wa tatu sasa tangu imejengwa na imeanza kubomoka.

Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa *Iringa Bypass*?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. *ENG.* GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, Mbunge wa Iringa Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii yenye urefu wa kilometa saba tumeshaanza kuijenga. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Iringa na watu wote wanaopita hiyo barabara, Serikali inatambua ni barabara muhimu sana kwani, pale kwenye barabara pakifunga, hatuna njia. Namwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira, kwenye

bajeti hii tuna hakika tutaendelea kuijenga kwa awamu ili tuweze kuikamilisha na tuwe na barabara ambayo ni *bypass* kwa Mji wa Iringa, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera ya Wizara hii inaelekeza kuunganisha barabara ya Mkoa mmoja na Mkoa mwingine kwa kiwango cha lami. Tuna barabara mbili kutoka Karatu kwenda Mbulu ambapo ni Mkoa wa Manyara na Mkoa wa Arusha; na kuna barabara inayotoka Karatu – Njiapanda – Mang'ola – Lalago ambayo inaunganisha Mkoa wa Arusha na Mkoa wa Simiyu, zote hizi hazijajengwa kwa kiwango cha lami: Je, lini Serikali mtakamilisha barabara hizi au mtajenga barabara hizi kwa kiwango cha lami ikiwa sera yenu inaelekeza hivyo?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. *ENG.* GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Paresso, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli sera ni kuunganisha barabara kwa kiwango cha lami Mkoa na Mkoa, lakini kipaumbele pia ni kuhakikisha kwamba, kama barabara ambazo zinakwenda *parallel* tutaanza na moja halafu itafuata nyingine kulingana na upatikanaji wa fedha. Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kwamba barabara ya Oldeani – Mang'ola kwenda Matala - Sibiti inakwenda

kama *parallel,* yaani sambamba na barabara ya Karatu – Mbulu – Hydom – Kidarafa hadi Sibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo barabara ambayo tunaita *Serengere Southern Bypass* imeingizwa kwenye mpango wa kuijenga kwa *EPC + F,* lakini Serikali inafikiria kuijenga barabara kuanzia Oldeani hadi Mang'ola kwa kiwango cha lami kabla ya kupita Mang'ola kwenda Sibiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa David Kihenzile.

**MHE. DAVID M. KIHENZILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Serikali iliahidi kuanza kujenga barabara ya Mafinga – Mgololo ambayo ni muhimu sana kwa uchumi wa Taifa letu. Tunashukuru kwa sababu, tayari wamesema itaanza kujengwa:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali ni: Je, ni lini mchakato wa *EPC + F* utakamilika ili barabara ya Mafinga – Mgololo ianze kujengwa kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. *ENG.* GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kihenzile, Mbunge wa Mufindi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Mafinga kwenda Mgololo imeingizwa kwenye Mpango wa *EPC + F*. Kama Wizara, upande wa ufundi kwa maana ya *engineering,* yaani *Engingeering Procurement* na *Construction,* tumeshakamilisha, na sasa ziko zinachakatwa na Wizara ya Fedha, na baada ya hapo basi taratibu zinazofuata za manunuzi zitaanza, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maimuna Mtanda.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia fursa hii. Swali langu kwa Wizara ni kwamba, Mkoa wa Mtwara na Barabara yake ya kiuchumi kilometa 210 kutoka Mtwara – Tandahimba – Newala – Masasi ambayo tayari imeshajengwa kilometa 50 na fedha zimeshapatikana kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika muda mrefu, lakini kila tukiuliza tunaambiwa Serikali ipo kwenye mchakato wa manunuzi. Sasa tunataka kujua, ni lini mchakato wa manunuzi utakamilika ili barabara hii ya kiuchumi ianze kujengwa? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. *ENG.* GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Newala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli barabara ya Mnivata – Tandahimba – Newala hadi Masasi, kilometa 160 ipo kwenye taratibu za manunuzi. *ADB* wameshakubali, tumepata *no objection;* kwa hiyo, kinachoendelea sasa hivi ni taratibu za kawaida za manunuzi na hasa tunapokuwa tunashirikiana na wenzetu wahisani kwamba, tutakapokamilisha *lot* hizi mbili, zitaanza kujengwa. Tuna uhakika kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha huu, shughuli nyingi zitakuwa zimeanza katika hiyo barabara, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dorothy Kilave.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kuuliza: Je, ni lini sasa Serikali itamaliza ujenzi wa barabara ya Chang'ombe inayoanzia mataa ya Chang'ombe kuelekea barabara ya Kilwa; ukilinganisha kwamba, sasa hivi kuna foleni kubwa sana na ile barabara ni kubwa na hasa ukizingatia wananchi wengi

wanapita; na hasa kipindi ambacho kuna michezo kwenye uwanja ule wa Taifa, hasa Simba na Yanga?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. *ENG.* GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kilave, Mbunge wa Temeke, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Chang'ombe kwenda Kilwa ni sehemu ya barabara za *BRT* Awamu ya Pili. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, naye atakuwa shahidi kwamba kasi imeongezeka sana. Tuna uhakika, kwa mujibu wa kazi anavyoendelea mkandarasi huyu, barabara hii itakamilishwa kama tulivyokubaliananaye kwenye mkataba, ahsante.

**MWENYEKITI:** TUnaendelea na swali la Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 49

**Fidia kwa wananchi wa Makole na Mkonze – Dodoma**

**MHE. KUNTI Y. MAJALA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itamaliza kulipa fidia Wananchi wa Makole waliopisha upanuzi wa Uwanja wa Ndege na Mkonze waliopisha ujenzi wa *SGR*?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kunti Yusuph Majalla, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya ndege Tanzania *(TAA)* imekamilisha malipo ya fidia kwa wananchi kutoka kaya 14 za Mtaa wa Chaduru B, Kata ya Makole, Dodoma Mjini, zilizopisha upanuzi wa Kiwanja cha Ndege Dodoma. Fidia hiyo, iligharimu kiasi cha shilingi 1,900,000,000, ilihusu upanuzi wa kiwanja kwa mita 150 zilizohitajika. Serikali haitahitaji kupanua zaidi Kiwanja cha Ndege cha Dodoma kwa kuwa imeanza kujenga Kiwanja cha Ndege cha Msalato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania *(TRC)* imekamilisha tathmini ya fedia kwa wananchi wote wa Mkonze ambao maeneo yao yatatwaliwa kwa ajili ya ujenzi wa *SGR*. Zoezi la ulipaji wa fidia lilianza kufanyika kuanzia tarehe 4 Aprili, mwaka huu 2023. Naomba wananchi ambao bado hawajalipwa wawe na subira wakati zoezi la malipo likiendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, naomba kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kuwa, ujenzi wa reli ya *SGR* unafanyika kwa utaratibu wa Sanifu na Jenga *(Design and Build),* hivyo utwaaji wa maeneo ya nyongeza utaendelea kufanyika kwa kadiri ya mahitaji, kwa mujibu wa sheria, na taratibu za nchi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunti Majalla.

**MHE. KUNTI Y. MAJALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba pamoja na hayo majibu ambayo hayaridhishi, nina maswali mawili madogo ya nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwanja wa ndege, awali upanuzi ulikuwa ni mita 300 na upanuzi huo umeanza mwaka 2016. Mpaka tunavyozungumza sasa, ni miaka saba, wamepanua mita 150. Mita nyingine 150 waliwazuia wananchi wa Kata ya Makole kutokuendeleza maeneo yao, na mpaka sasa tunavyoongea nyumba zile zimekuwa ni magofu, watu walihama mle: Je, Serikali haioni wana sababu ya kuwalipa wananchi wa Kata ya Makole, kaya 50 zilizobaki kifuta jasho, ili waweze kufanya ukarabati wa nyumba zao na warudi kwenye makazi yao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Ni sera ya Serikali kwamba, inapotwaa maeneo ya wananchi, inatakiwa ilipe fidia kwanza ndipo iendelee na utekelezaji wa miradi. Imekuwa ni kawaida ama ni tabia ya Serikali kuendelea kutwaa maeneo ya wananchi bila kuwalipa fidia na kuendeleza utekelezaji wa miradi, na matokeo yake wananchi wengi wamekuwa wakidhulumiwa. Hivi tunavyoongea…

**MWENYEKITI:** Uliza swali Mheshimiwa Kunti?

**MHE. KUNTI Y. MAJALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, watu 46 walioko Mkonze hawajafanyiwa uthamini na Waziri hapa anasema waendelee kuvuta subira. Ni lini wananchi 46 waliobaki Mkonze watalipwa fidia yao kwa sababu tayari maeneo yao yameshachukuliwa na mradi umeshatekelezwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kunti Yusuph Majalla, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba mwaka 2016 Serikali ilikuwa na nia kwa ajili ya ujenzi ama upanuzi wa uwanja wetu wa ndege wa hapa Dodoma, lakini Serikali ilipoanza ujenzi mwingine mpya, hususan katika kiwanja cha Msalato, ikaona haina sababu ya kuendelea kupanua uwanja mkubwa zaidi wakati uwanja mkubwa wa Kiwanja cha Msalato unaendelea kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, ilipofika mwaka 2018 na kupitia Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa aliyekuwepo pamoja na timu yake na wataalamu wetu kutoka *TAA* walipewa taarifa wananchi hawa kwamba eneo hilo, na kusudio la Serikali kuendelea kuupanua uwanja huu halitakuwepo tena, bali tutalipa zile fidia za mita 150 ambazo tayari tumeshalipa kwa kiasi cha Shilingi 1,900,000,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa swali lake la pili, kuhusu Mkonze, ni kweli kwamba, katika ujenzi wa *TRC,* kawaida unapojenga *SGR,* tunasema ni *Design and Build,* maana yake huwezi kufanya tathmini yote na ukalipa wananchi wote. Maana yake, inafanyika tathmini na wakati huo huo ulipaji unaendelea. Kwa maana hiyo basi, ifikapo tarehe 17 ya mwezi huu wa Aprili, wananchi wote wa eneo la Mkonze ambao hawajalipwa fidia zao tukutane eneo la *SGR Station* hapa Mkonze na waje na nyaraka zao, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa Mwaifunga.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Jimbo la Tabora Mjini ni moja kati ya majimbo ambayo reli ya *SGR* imepita kwenye maeneo ya Ndevelwa. Wananchi wamefanyiwa tathmini ndogo, lakini pamoja na udogo wa tathmini hiyo, bado hizo fedha mpaka sasa tunavyozungumza wananchi hao hawajalipwa fedha zao: Ni lini Serikali itawalipa wananchi hawa fedha zao ili watafute maeneo mengine ya kuweza kujihifadhi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Namwomba Mheshimiwa Mbunge kwa suala la fidia katika eneo hili la *SGR* mara baada ya maswali na majibu tuonane ili tuweze kuwasiliana na wale wote ambao wanafanya zoezi hili la ulipaji kwa sababu, tunaendelea kulipa katika eneo hili, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Naibu Waziri; Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibete pamoja na *Eng.* Godfrey kwa majibu ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi.

Tunaendelea na Wizara ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 50

**Umuhimu wa mtandao wa *Wi-Fi* kwenye maeneo yote**

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA** aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja ya kufunga mtandao wa Wi-Fi maeneo yote nchini kufuatia jamii kuhamasika na matumizi ya teknolojia?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, napenda kujibu swali la

Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kufunga mtandao wa *Wi-Fi* maeneo yote ya umma nchini kufuatia jamii kuhamasika na matumizi ya teknolojia katika shughuli mbalimbali za kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa utekelezaji wa kufunga mtandao wa *Wi-Fi* umefanyika katika vituo sita ambavyo vinatoa huduma ya *internet* ya wazi *(Internet hotspot)* katika maeneo mbalimbali. Maeneo hayo ni Stendi ya Nanenane, Dodoma; Buhongwa, Mwanza; Kiembesamaki, Unguja; Chuo Kikuu cha Dodoma, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu *(CIVE)* na Soko la Tabora, na Chuo cha Ustawi wa Jamii Lungemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji huo utaendelea kufanyika katika maeneo mbalimbali nchini kwa kutegemea upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, swali la nyongeza.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali madogo mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia hamasa kubwa iliyofanywa na Serikali kuhusu matumizi ya teknolojia iliyosababisha wananchi wengi kutumia mtandao wa *internet:* Je, Serikali haioni haja sasa ya kuwa na *bundle* maalum kwa ajili ya wajasiriamali wadogo litakalowasaidia kutafuta masoko kwa njia ya mtandao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili: Ni lini sasa Serikali itahakikisha taasisi zote za elimu zinakuwa na huduma ya *Wi-Fi* itayaowasaidia walimu na wanafunzi kuongeza maarifa, na vilevile kutoa mchango wao katika ulimwengu wa elimu duniani? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa Mheshimiwa Mbunge alishaleta maombi yake kuhusu vikundi na vikoba kwa ajili ya kupata *bundle* maalum. Ni kweli kabisa kwamba, huwa tuna utaratibu kama maeneo ya vyuoni, na maeneo mbalimbali ambayo huwa yanapata *special offer*. Hilo tumeshalipokea na Serikali bado inalifanyia kazi, na pale ambapo tutakuwa tumekamilisha, basi tutamjulisha Mheshimiwa Mbunge kwa ajili ya hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele cha pili; ni wazi kabisa kwamba huu ni utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Ibara ya 61 (h), inayotutaka kuanzisha huduma ya mawasiliano ya *internet* ya kasi katika maeneo yote ya umma *(Public Place)* ikiwemo maeneo ya hospitali, taasisi za elimu na vituo vya usafiri hadi kufikia asilimia 40 mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari Serikali imeshaanza. Kama ambavyo nimejibu katika swali la msingi, tumeshajenga vituo sita, na mwaka huu tayari kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa wote, tumejipanga kwa ajili ya kwenda kufikisha huduma ya *internet* ya *Wi-Fi* katika maeneo 20 na tutaendelea kufanya hivyo mpaka tutakapofikia katika lengo la Serikali

ambalo ni utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi kufikia asilimia 40.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa *Eng.* Andrew Mathew Kundo kwa majibu hayo kutoka Wizara ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

Tunaendelea na Wizara ya maji, Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 51

**Kupanda mazao yanayopendwa na wanyama hifadhini**

**MHE. SUMA I. FYANDOMO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya kukamilisha Ujenzi wa Mradi wa maji Tukuyu Mjini?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya maji. Mheshimiwa *Eng.* Maryprisca Mahundi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba wa ujenzi wa Mradi wa Maji Tukuyu Mjini ni wa miaka miwili na ulianza mwezi Agosti, 2021 na unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2023. Hadi sasa utekelezaji unaendelea na umefikia asilimia 82. Kazi zilizokamilika ni pamoja na ujenzi wa banio katika chanzo, ulazaji wa bomba kuu lenye urefu Kilomita 9.5, ujenzi tanki

moja lenye ujanzo wa lita milioni 1.5 na ulazaji wa mtandao wa bomba wa umbali kilomita 20.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, kuna mradi wa Kiwira ambao naweza kusema ni mradi mama kwa sababu utawatua ndoo kichwani wanawake wengi wa Mkoa wa Mbeya. Mkandarasi alishasaini mkataba, lakini mpaka sasa hivi hajaanza kazi ya ujenzi wa mradi huo. Sasa je, ni lini mkandarasi huyo ataanza kazi rasmi ya ujenzi huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Tunaishukuru sana Serikali kwamba ilitoa ahadi ya kuleta fedha zaidi ya Shilingi bilioni nane kwenye mradi wa Kyela Kasumulu, mradi huo ambao utawasaidia wananchi wa Kata ya Nkuyu, Ndandalo, Mbugani, Kajunjumele, Bondeni, Serengeti, Kyela Mjini, Ikolosheni, Itungi na Ipyana: Je, ni lini Serikali itapeleka fedha ili mradi huo uanze kujengwa? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Maryprisca.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Suma Fyandomo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mradi wa Kiwira, tayari umeanza kushughulikiwa. Kuhusu mkandarasi kutoonekana *site,* lakini kuna kazi za awali tayari zimeshaanza na suala la kupeleka hela kwenye mradi wa Kyela Kasumulu, huu mradi

tumeshaupelekea hela mara nyingi na tutaendelea kuupelekea kadiri tunavyopata fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Innocent Bilakwate, nimekuona.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafsi ya kuuliza swali la nyongeza. Mradi wa Lunyinya – Chanya na Mradi wa Kilela – Rutungu – Lusungiro, miradi hii imesimama kwa muda mrefu kwa sababu mkandarasi hajalipwa. Ni lini mkandarasi atalipwa ili miradi hii iweze kukamilika? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji hivi vyote alivyovitaja vina miradi miwili, hii miradi ni kweli tayari imeanza kufanyiwa kazi na malipo yanaendelea kufanyiwa kazi. Tayari fedha zimepatikana wiki iliyopita, baadhi ya wakandarasi tunaanza kuwapunguza, kuwalipa. Hivyo, mkandarasi huyu pia tunatarajia aweze kulipwa fedha yake.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Maryprisca kwa majibu hayo.

Tunaendelea na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara; Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 52

**Kuanzisha *Special Economic Zone* – Njombe**

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaanzisha *Special Economic Zone* ili kuchochea viwanda vya uchakataji Njombe Mjini?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika, Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Programu ya *Special Economic Zones* na *Export Processing Zones* ina jumla ya maeneo ishirini na nne ambayo yametangazwa kuwa Maeneo Maalum ya Uwekezaji *(Special Economic Zones)*. Serikali imeendelea na jitihada za kuanzisha Kanda Maalum za Kiuchumi katika maeneo mbalimbali nchini kwa ajili ya kuchochea ukuaji wa uchumi. Katika kufanikisha azma hiyo, Mamlaka ya *EPZ* imekuwa ikizihamasisha Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kutenga na kuwezesha uendelezaji wa maeneo ya *Special Economic Zones.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya *EPZA* iko tayari kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge wa Njombe Mjini na Uongozi wa Mkoa wa Njombe kufanikisha uanzishaji wa Kanda Maalum ya Kiuchumi katika Mkoa huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika, swali la nyongeza.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu ya Serikali ambayo ni majibu ya kawaida *(generic answers)*. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, Mkoa wa Njombe na Halmashauri ya Mji wa Njombe ndiyo ina uzalishaji mkubwa sana wa zao la parachichi. Kwa bahati mbaya sana uzalishaji huo ni mkubwa lakini asilimia 90 mpaka 99 ya mazao ya matunda ya parachichi yote yanasafirishwa nje bila kuongezwa thamani kwa maana halisi ya uongezaji wa thamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali langu; Mheshimiwa Waziri anaweza kutoa *commitment* hapa leo kwamba watachukua suala la Mji wa Njombe na Mkoa wa Njombe kama *special case* ili waweze kuanzisha maeneo maalum kwa ajili ya uzalishaji na uchakataji wa parachichi tuache kupeleka maparachichi zikiwa ghafi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kama ataitoa *commitment* hiyo na atakubaliana nami na sioni kwa nini asikubaliane nami. Je, kuonesha umuhimu wa suala hilo, Waziri yuko tayari twende pamoja Njombe baada ya kusoma bajeti yake ili tukaanze majadiliano ya awali ya kuanzisha mchakato huo wa kuanzisha viwanda vya kuchakata parachichi badala ya kusafisha, kupaki na kusafirisha ambayo inatupotezea sisi mapato? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya

nyongeza ya Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli moja ya vigezo ambavyo vinatakiwa kwa ajili ya kuanzishwa maeneo ya uwekezaji kwa ajili ya kuzalisha bidhaa kuuza nje *(Special Economic Zones)* ni uwepo wa malighafi; pili ni uwepo wa ardhi; zaidi ni miundombinu wezeshi kwa ajili ya kuzalisha bidhaa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe *commitment* ya Serikali na niwaagize Mamlaka ya *EPZA* waanze mchakato mara moja wa kuwasiliana na Mkoa wa Njombe, na kutafuta wadau wengine. Kwa sababu katika maeneo haya ya uwekezaji kwa ajili ya mauzo nje tunashirikiana pia na sekta binafsi ili kuhakikisha mkoa huu sasa unakuwa na eneo kwa ajili ya kuzalisha bidhaa au kuzalisha maparachichi ambayo yatauzwa nje ikiwa ni bidhaa zake au maparachichi yenyewe ili kuongeza uchumi wa Mkoa wa Njombe na azma ya kupunguza kuuza malighafi nje, yakiwemo na maparachichi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya *commitment* hiyo na *EPZA* wataanza kufuatilia, na mimi nikubaliane naye, nitakwenda Mkoa wa Njombe ili tuweze kuona namna ya kujadiliana na wadau ukiwemo mkoa, kupata ardhi na wadau wengine kwa ajili ya kuwekeza au kuanzisha maeneo huru ya uwekezaji katika Mkoa huo wa Njombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru kwa maswali na majibu ya Waheshimiwa Mawaziri. Sasa ni wakati wa matangazo. Kuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge

ambao wapo kwa siku hii ya leo, wametutembelea hapa Bungeni.

Kuna wageni wanne wa Mheshimiwa Esther Malleko ambao ni familia yake kutoka Jijini Dodoma, karibu sana; kuna Ndugu Ahmed John, kaka yake; Ndugu Darel Charles, mtoto wake; Ndugu Denzel Charles, mtoto wake na Ndugu Bless Solomon, mtoto wake pia, karibu sana wageni wa Mheshimiwa Esther. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni 39 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni Wanamaombi kutoka Jijini Dodoma; karibu sana Wanamaombi katika Bunge letu. *(Makofi)*

Tuna wageni 32 wa Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu ambao ni viongozi na Wanakwaya wa Uinjilisti Usharika wa Sokoni II ya KKKT Dayosisi ya Kaskazini Kati kutoka Jijini Arusha, karibu sana kwenye Bunge letu. *(Makofi)*

Tuna wageni ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; tuna wanafunzi na walimu 35 kutoka Taasisi ya Uhasibu Singida, karibu sana. *(Makofi)*

Tuna wanafunzi 20 kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wanaosomea uchumi *(DUEA),* karibu sana. *(Makofi)*

Tangazo lingine kwa Waheshimiwa Wabunge; ujumbe wa Benki ya CRDB umetembelea Bunge leo siku ya tarehe 11 Aprili, 2023, ukiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wake Ndugu Abdulmajid Nsekela; wako pale kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

Amefuatana na Ndugu Frederick Nshekanabo, Afisa Mkuu wa Fedha; Ndugu Chabu Mishwaro, Meneja wa Kanda ya Kati; Ndugu Rashid Rashid, Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Benki ya Kiislamu; Ndugu Chabba Madaha, Mkuu wa

Kitengo cha Malipo na Udhibiti; Ndugu Emmanuel Kiondo, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano. Ndugu Grace Adam, Meneja wa Tawi la Bunge. *(Makofi)*

Hongera sana Ndugu Grace kwa makofi hayo yanaashiria jambo zuri, karibu sana katika Bunge letu. Makofi hayo kwa kweli ni ishara nzuri. Hongera sana na Mwenyezi Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

Pia tuna Ndugu Andrew Mheziwa, Meneja Mahusiano Huduma kwa Serikali na Ndugu Imani Chassama, Msaidizi wa Mkurugenzi Mtendaji. *(Makofi)*

Aidha, ujumbe huu wa CRDB umeandaa futari maalum kwa ajili ya Waheshimiwa Wabunge na watumishi wa Bunge katika viwanja vya Bunge, leo siku ya Jumatano, tarehe 11 Aprili, 2023 kuanzia saa kumi na mbili jioni na mgeni rasmi atakuwa Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson ambaye ni Spika wa Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, na watumishi wote mnaalikwa katika *Iftar* hii ambayo pia itahudhuriwa na viongozi wa dini wa mkoa pamoja na viongozi wengine wa Serikali.

Katibu tuendelee.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mjadala wetu toka Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ajili ya makadirio

ya mapato na matumizi ya ofisi hiyo kwa mwaka 2023/2024. Tutaanza na Mheshimiwa Livingstone Lusinde, Mheshimiwa Charles Kimei na Mheshimiwa Oran Njeza wajiandae.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kupata nafasi ya kufungua dimba asubuhi ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mungu sana kwa ajili ya kutuzawadia zawadi ya uhai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nishukuru kupata nafasi ya kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, ambayo imewasilishwa mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, tunampelekea shukrani zetu kutoka kwa wananchi wa Jimbo la Mvumi, kwa kazi kubwa anazozifanya. Majuzi hapa tulimsikia Mheshimiwa mama Kilango akipiga hesabu ya fedha zilizokwenda jimboni kwake. Kila Mbunge ukimsimamisha hapa atazungumzia pesa zilizokwenda kwenye jimbo lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Jimbo la Mvumi Mheshimiwa Rais Dkt. Samia majuzi tu ametuteremshia shilingi bilioni tatu na milioni 700 kwa ajili ya ujenzi wa chuo cha *VETA* lakini hapo kabla tulishapata pesa kwa ajili ya mradi wa *booster,* pesa chungu mzima, karibu bilioni sita ukijumlisha, zote zimeingia kwenye Jimbo la Mvumi; haya ni maajabu. Lazima tumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayotufanyia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata miradi ya maji katika Jimbo la Mvumi, karibu ya bilioni mbili inaendelea kujengwa katika Kata ya Mvumi *Mission* pamoja na Kata ya Handali; hii

tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi njema anayotufanyia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo kubwa ambalo limezungumzwa katika bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nataka niende kwenye suala la amani na utulivu, amani na utulivu ndio msingi wa kuendesha Tanzania. Lakini Mheshimiwa Rais ameidumisha amani na utulivu kwa kuileta nchi pamoja; amekusanya makundi yote kukaa mezani pamoja ili tuzungumze namna gani tutatoka hapa tulipo kuisogeza nchi pamoja; hongera sana Dkt. Samia Suluhu Hassan. Hili siyo jambo dogo, hili ni jambo kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumemuona Rais namna anavyohangaika kutafuta pesa. Waheshimiwa Wabunge ambao tumekaa hapa muda mrefu mtakubaliana nami, sasa hivi mimi ni kipindi cha tatu hapa; bajeti ya mwaka 2021/2022 tulipitisha hapa bajeti Mheshimiwa Rais akaenda kutafuta fedha mpaka zikapita ile bajeti; sijawahi kuona tangu tumekuwa Wabunge humu, wote, akina Mheshimiwa Ole-Sendeka mko hapa. Tumepata pesa zinazovuka bajeti kwa mara ya kwanza. Rais Dkt. Samia anafanya kazi kubwa, tusimkatishe tamaa, lazima tumsaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ninyi Waheshimiwa Mawaziri, Tanzania tumebahatika kupata Rais anayewapa uhuru mkubwa wa kufanya kazi; fanyeni kazi ya kumsaidia Rais. Rais anatafuta pesa, mnataka yeye mwenyewe aingie tena kupiga hesabu; haiwezekani. Lazima muwasimamie watu wetu. Tuwasimamie Makatibu Wakuu, tuwasimamie wahasibu, ili waweze kujibu hoja kabla hazijaletwa hapa Bungeni. Tunachokifanya hatumtendei haki Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Mawaziri, si sawa, hili jambo Mheshimiwa Waziri Mkuu, si sawa. Tunataka Rais afanye kazi ya kutafuta fedha za ujumla lakini haya

mambo madogo madogo myamalize ninyi. Tumalize kero za wananchi, tumalize matatizo ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vihoja vidogovidogo tunashindwa kuvijibu. Unashindwaje kumaliza tatizo katika Wizara yako wakati unajua kabisa *CAG* anapokuja anakuja kuhoji watu wako; wasimamie. Hizi hoja nyingine zinajibika kabisa, ndiyo maana unaona Bunge sasa tunatolewa kwenye mstari tunapelekwa sehemu kujadili hoja kabla ya wakati, kitu ambacho siyo sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka kupitisha bajeti ya nchi, tunataka kupitisha bajeti ya wananchi wa Tanzania. Hili ni jambo kubwa, lakini kwa sababu kuna baadhi ya Wizara zilizembea kushughulika na hoja za Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali, ndiyo maana mnaona sasa Bunge linasukumwa pembeni tuanze kujadili kabla ya wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taratibu zinafahamika kwamba ile ripoti ikishapokelewa na Mheshimiwa Spika inakabidhiwa kwa Kamati ya *PAC* (Hesabu za Serikali), Kamati ya *PAC* inakwenda kuchakata kwa kuwaita wote. Tunaliita jicho, wataitwa na watu wanaotuhumiwa watatoa majibu, halafu ndio Wabunge tunakuja kuamua. Sasa tukianza kuamua mapema, huo mwezi Novemba wakati *PAC* wamechakata tutatoa uamuzi gani tena? Tutakuwa tunajikanyaga wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu, kwa hiyo, tusifanye jambo kwa mihemko. Tuna Spika mzuri, mwanasheria, anatuongoza vizuri, kwa hiyo, nina uhakika kabisa Bunge hili litaamua sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema; Mheshimiwa Rais ametoa uwazi mkubwa. Unajua hata hii ripoti yenyewe kama Rais angekuwa hataki itoke, ingetoka? Ni Rais ndio

anataka, Rais ameweka mambo kwa uwazi, hataki kificho, anataka sisi tumsaidie wapi panavuja, wapi tuzibe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutapata wapi Rais kama huyu ambaye anaiongezea bajeti Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; utampata wapi? Ili aweze kukagua kila kona. Rais anataka nchi yetu tuwe wawazi ili tuweze kujua wapi kuna tatizo tusughulike nalo; wapi kuna shida tushughulike nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Waheshimiwa Mawaziri, tusimamie kwenye Wizara zetu. Mnafanya kazi vizuri, msinyongee, hakuna Waziri ametajwa mahali popote katika hii ripoti. Wasiwasi wenu uko wapi? Chapeni kazi za maendeleo ya wananchi. Tusimamie barabara, tusimamie maji, tusimamie maendeleo kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalia kwenye kada ya afya, juzi Mheshimiwa Rais amefanya kufuru hapa; ameleta magari ya kuchimba visima vya maji karibu nchi nzima. Kwa hiyo, sasa hivi maana yake kila jimbo likipangiwa ratibu vitatobolewa visima virefu vya maji na kuondoa matatizo yote ya maji; hii ni kazi inayofanywa na Mheshimiwa Dkt. Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tumeona madarasa yalivyojengwa nchi nzima, kila jimbo limeguswa. Zamani kabla ya Mheshimiwa Samia, wananchi wetu tulichangishana mpaka wengine wangefungwa; uongo kweli? Kuna watu wangekimbia kwenye majimbo. Lakini Mheshimiwa Samia akasema hapana, tutatafuta fedha tuwapunguzie mzigo wananchi ili watu waweze kusoma shule, na sasa hivi tuna tatizo la kupeleka wanafunzi, siyo tena madawati. Madawati yapo, madarasa yapo, ila sasa watoto hawataki kwenda shule. Tumpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kazi hii nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawaomba sana tunapomuunga mkono Mheshimiwa Rais tumuunge kwa vitendo. Mawaziri fanyeni kazi sisi Wabunge tupo. Ukifika wakati wa kujadili Taarifa ya *CAG* tutaijadili kwa nguvu zote. Lakini kwa sasa tupitishe bajeti ya Serikali ambayo iko mbele yetu. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Ole-Sendeka.

**T A A R I F A**

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kutumia nafasi hii kutoa taarifa kwa Mheshimiwa Mbunge, rafiki yangu Lusinde. Kusema kwamba jambo hili liendelee kusubiri mpaka wakati mwingine kwa maana ya kufuata ratiba mpaka Novemba ilihali mnaujua upepo uliopo nje, Watanzania wamekerwa na hatua hii ya ufisadi uliokithiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo chochote cha kuchelewesha uchukuaji wa hatua dhidi ya wahusika wa ufisadi huu wa matrilioni, mabilioni ya fedha, na bila Bunge lako kuchukua hatua ya kuunda Kamati teule au kufanya maamuzi kwa ripoti iliyokamilika ni kuchelewesha kutoa haki kwa Watanzania na huko ni kufifisha jitihada za kumuunga mkono Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayofanya ya kukusanya fedha na kwamba hata hasira yake Bunge hili litakuwa halijamtendea haki Samia wala Watanzania kama hamtachukua hatua sasa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lusinde, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei kwa sababu anachangia kwenye hotuba yangu. Nilichosema ni kwamba tufuate taratibu, taratibu ni taratibu. Tumejipangia taratibu na sheria zimepangwa. Jamani eh, kuku anatotoa baada ya siku 21. Sasa Mheshimiwa Mzee Ole-Sendeka anataka atotoe kesho, yaani mayai atage leo, atotoe kesho; itawezekana jamani? Wabunge tusijidanganye, tusifikiri kwamba hapo ndiyo tunamsaidia Rais, kumsaidia Rais kwa kuvunja sheria, kwa kuvunja Bunge, kwa kuvunja kanuni itakuwa siyo sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi maafisa masuhuli wote wako pale, wamekuja kuleta bajeti. Utawaitaje? *PAC* itawaitaje kwenda kushughulikia mambo yao? Kwa hiyo, ninashauri sisi wakati tunajadili hukatazwi kuligusa kaka, lakini lazima lifuate ratiba ya Kibunge. Na likifuata ratiba ya Kibunge ndiyo litakuwa na majibu sahihi ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakushukuru sana; ahsante sana. naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Livingstone Lusinde. Tunaendelea na Mheshimiwa Charles Kimei. Mheshimiwa Oran Njeza na Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa wajiandae.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Pia nimpongeze Spika wetu pamoja na Naibu Spika na Wenyeviti wote ambao wamechaguliwa kwa namna ambavyo mnaendesha shughuli za Bunge hili kwa uwazi na kwa namna ambayo tunapata tija. Pia nichukue fursa hii kutoa shukrani za pekee na pongezi ambazo zinatoka kwa wananchi wangu wa Vunjo kwa Mheshimiwa Rais wetu na Amiri Jeshi wetu Mkuu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Makamu wake na Waziri Mkuu pia kwa namna ambavyo wanaendesha nchi yetu tukabaki tukiwa na nchi iliyotulia kisiasa na kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kasi ya ukuaji wa Pato letu la Taifa bado linaridhisha ukilinganisha na sehemu nyingine ambapo tunaanza kuona *recession* ikitokea, mporomoko ukitokea lakini hapa kwetu tunaona kwamba pato linakua kwa takribani asilimia tano. Vilevile mfumuko wa bei uko chini kuliko kwa majirani zetu, pia na riba zimeanza kushuka, ingawa si sana lakini zimeanza kushuka; jambo ambalo linatuonesha kwamba pengine hapa tunapokwenda ni pazuri zaidi kama hali ya dunia nayo itarudi kwenye hali ambayo ni tulivu kutoka hii ya sasa ambayo mambo yanakuwa magumu. Naamini kwamba kwa wanavyotabiri wenzetu ni kwamba ndani ya mwaka huu wataona mafanikio sana kwa sababu vita vinaendelea na kuna mkanganyiko kwenye soko la kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti,sasa niseme hivi, kusema kweli wana-Vunjo wamemshukuru Mheshimiwa Rais pamoja na Serikali yake kwa ujumla kwa miradi mingi kama wengine wanavyosema. Tumepata miradi mingi kama vile mradi wa maji kule Njia Panda ambao umeshakamilika, shilingi bilioni 2.3 zimekwenda huko. Vilevile kuna miradi ya maji kwenye Kata za Mwika Kaskazini, Mwika Kusini, Mamba Kaskazini, Mamba Kusini, Marangu Mashariki na Magharibi, Kilema Kati na Kilema Kusini na yote inaendelea. Miradi yote ina takribani shilingi bilioni tatu, haijakamilika. Hata hivyo Mheshimiwa Waziri nilikutana naye na ameniahidi kwamba fedha zitakwenda kukamilisha miradi hii kabla ya mwisho wa bajeti inayoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumepata vituo viwili vya afya, kituo kimoja tumepata kule Kirua Vunjo ambacho kilikuwepo lakini kikainuliwa hadhi ya kuwa kituo cha afya na kimepata vifaa vyote ambavyo vinastahili. Pia tumepata Kituo cha Afya Malangu Mashariki. Vyote hivi tunazungumza zaidi ya bilioni moja ambazo zimetumika na Serikali.

Mheshimiwa Spika, vilevile tumepata madarasa; kila mtu anayafahamu madarasa ya UVICO pamoja na madarasa mengine. Tumepata madarasa shule nzima ambayo ni ya wasichana pale Njia Panda. Kwa hiyo nataka niseme kwamba Serikali imewekeza vizuri na Mungu awajalie wote ambao wamewezesha miradi hii kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuseme pia kwamba *TARURA* wamepata pesa, tumepata barabara, zimechimbwa vizuri. Hata hivyo ninachosema ni kwamba barabara nyingi sasa hivi zimeharibika tena. Hii ni kwa sababu barabara zinazopitishwa *grader* mvua zikinyesha, na kwa sababu kule kwetu ni mwinuko basi zitakuwa zimepoteza hadhi. Lazima sasa tuombe *TARURA* wapate fedha ya ziada kwenda kukarabati hizi barabara ambazo zimeharibika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naweza nikatumia muda mwingi sana kuzungumzia mambo ya jimbo, lakini nasema kwamba wote tunashukuru; tunajua kwamba fedha imetafutwa na Mheshimiwa Rais. Mimi sitazungumzia juu ya *CAG* kwa sababu nitatoa machozi hapa nikianza kuizungumzia *CAG*. Mngeacha nimalize haya kwanza na baadaye tutaanza kuzungumza, kama mwenzetu alivyosema, pengine tutakuja kwa wakati mwafaka.

Mheshimiwa Spika, lakini nitumie fursa hii kuzungumzia mambo mengine ya kitaifa ambayo si lazima yawe ya kijimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza unajua kwamba Sensa imetoka, takwimu zimeanza kutoka na takwimu muhimu zimeshaanza kutoka lakini nashangaa sana hatujaona hii mipango inayokuja ikigusia na kuonesha kwamba kuna namna gani tunaenda kujipanga upya ili tutoe miradi na huduma zetu hasa za jamii kwa kuzingatia idadi ya watu kwenye majimbo.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano kwenye Serikali kuna baadhi ya halmashauri yenye majimbo zaidi ya moja, zinayo majimbo matatu. Sasa inapofika kwamba wakati Serikali inapoanza kugawa keki hii wanasema tunapeleka kwenye halmashauri, halmashauri inakuwa na majimbo mawili tunaanza kugombana na majimbo yote ni makubwa. Kwa mfano Jimbo la Vunjo lina idadi zaidi ya watu 255,000, Jimbo la Mheshimiwa Ndakidemi, Moshi Vijijini lina watu 284,000 halafu unatoa ambulance moja. Tunaanza kugombana na mwenzangu hapa, kwamba sasa zitaenda wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naamini ni vyema kwamba mzingatie kuwa kuna halmashauri zina majimbo zaidi ya mawili, na aidha muangalie ukubwa wa hayo majimbo. Kuna halmashauri ambazo idadi ya watu ni nusu ya hao tulio nao sisi lakini wao wanakuwa *treated* kama halmashauri wanapata kama sisi tunavyopata mpaka tunabakia kupigana huko bila sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, nataka nizungumzie suala zima la kutengeneza bajeti hii ya mwaka huu. Bajeti tunayotengeneza sasa hivi haikuzingatia uhalisia wa hali ya uchumi wa dunia, na ndiyo maana tunaona kwamba fedha zilizopokelewa katika Wizara nyingi kwenye upande wa miradi ya maendeleo zimekuwa zinaenda kwa kusuasua sana. Sehemu nyingi zimepata chini ya asilimia 50 ya bajeti ya maendeleo; na sababu ni nini; tulitegemea kwamba tutapata fedha nyingi kutoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nawaambia kwamba kwa hali ilivyo sasa hivi kwenye uchumi wa wenzetu ambaoo unapata matatizo ya *recession* inakuwa vigumu sana wahisani kuja kwa kasi hiyo waliyokuwa wanatumia mwaka uliopita. Kwa hiyo ni lazima tujaribu kwa kuona tutafanyaje na ili mwaka huu tuweze kuzingatia. Kusema kweli riba zimepanda juu kwenye soko la kimataifa; na kwa vile zinapanda juu inakuwa vigumu sana kupata mikopo. Wale wawekezaji wetu

wanapeleka fedha Marekani kwa sababu riba za Marekani zimepanda hadi kufikia asilimia tano. Kwa hiyo wanapeleka fedha badala ya kutukopesha sisi; na wakitukopesha riba itakuwa juu sana kwahiyo itakuwa si himilivu na hivyo Deni la Taifa linaweza likaanza kuwa si himilivu. Kwa hiyo nataka niseme kwamba hilo ni jambo ambalo tunahitaji kuliangalia sana tuvyoelekea mbele, na ninaamini tutaona kwamba hali itakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti,naomba niishie hapo, lakini naendelea kutoa shukrani kwa nafasi niliyopewa. Ninaamini kwamba Serikali itazingatia ushauri tunaoutoa kwa sababu ninamini una uhalisia na itatuwezesha kuwa na mpango ambao unatekelezeka bila kulaumiana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei. Tunaendea na Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa ajiandae.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa fursa na mimi ya kuchangia kwenye hii Hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti,nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na timu yake kwa hotuba yake nzuri ambayo imeonesha ni kiasi gani kulikuwa na mafanikio makubwa ya utendaji wa Serikali hasa ukizingatia hiki kipindi tunachopitia. Tanzania si Kisiwa; sisi wenyewe tumeshuhudia kiasi gani ambavyo mtikisiko wa dunia umeathirika kutokana na UVIKO-19 pamoja na vita vya Urusi na Ukraine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mataifa makubwa yametikisika kikubwa. Wenzetu huko ukiangalia mfumuko wa bei ni zaidi ya tarakimu mbili na kuna wengine wanakaribia tarakimu

tatu. Sasa, ukiangalia hotuba ya Waziri Mkuu inaonesha sisi tuko chini ya asilimia tano ambayo ni asilimia 4.7 kwa mwaka huu. Vilevile tunategemea hata hali itakuwa nzuri kwenye bajeti ijayo. Sasa utaona ni maajabu kiasi gani kwa nchi kama Tanzania tunafanya vizuri ukilinganisha na mataifa makubwa. Leo hii kuna benki kubwa za dunia ambazo tulikuwa tunaziamini, nazo zimetikisika. Kwa hiyo hili si jambo dogo, ni jambo la kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa aliyoifanya katika kuhakikisha kuwa Tanzania tunakuwa katika hali hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiangalia hata ukuaji katika repoti ya Waziri Mkuu inaonesha kuwa ukuaji wa uchumi kwa Tanzania bado ni mzuri ukilinganisha na wenzetu. Ukiangalia ukusanyaji wa mapato bado ni mzuri ukilinganisha na wenzetu. Kwa nini tunajilinganisha na wenzetu? Ni kwa vile mpango wetu ni wa ushindani kiuchumi, ambao unahitaji kuonesha kiasi gani Tanzania tufanye vizuri ukilinganisha na mataifa mengine. Nchi jirani hapa tumeona mtikisiko wa uchumi, ukuaji wa uchumi umekuwa hasi. Vilevile leo hii hata ukusanyaji wa mapato wenzetu majirani wameshindwa kukusanya kiasi ambacho umepelekea hata kushindwa kulipa mishahara ya wafanyakazi wao. Sisi tunajivunia kwa Mheshimiwa Rais wetu pamoja na timu yake nzima ambavyo wameendelea kufanya vizuri na hali inakuwa na matumaini mazuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti,namshukuru Mheshimiwa Rais vile vile kwa jimbo langu na Wilaya yangu ya Mbeya, ametutendea mengi mno. Kwenye maji kwa kweli hata nikiuliza swali hapa litakuwa ni swali la kupongeza kwa sababu miradi mingi ya maji imeenda vizuri na inaendelea kutekelezwa. Hivi juzi Serikali imesaini mkataba wa mradi mkubwa wa maji ambao ni kwa Wilaya nzima ya Mbeya, likiwemo jimbo langu, pamoja na Mkoa wa Songwe, Mradi wa Kiwila.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye barabara vilevile kilikuwa ni kilio kikubwa. Mheshimiwa Rais naye ameidhinisha ujenzi wa barabara ya njia nne kuanzia Nsalaga ambayo iko jimbo la Mbeya Mjini mpaka Songwe ambayo iko Jimbo la Mbeya Vijijini. Hii ni hatua kubwa kwa sababu pamoja na changamoto zote, lakini Watanzania wengi wamepoteza maisha kwa ajili ya ufinyu na barabara ilivyokuwa mbovu, hii barabara yetu ya *TANZAM*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kumalizia ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Songwe, kwa kweli Mbeya ni ya kimkakati. Uwanja wa Ndege wa Songwe ambao ni mahsusi utakuwa wa kimataifa kwa ajili ya kusomba mizigo kupeleka nchi za kigeni. Mheshimiwa Rais amefanya jambo hili katika wakati mwafaka ambao tunategemea kuwa sasa Tanzania, badala ya mazao yetu kuoneshwa yanatoka nchi jirani, sasa hivi kwakweli tutakuwa hatuna sababu tena kuona maparachichi au kahawa zinatoka nchi jirani badala ya kwamba zinatokea Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika hili naomba Serikali, iangalie ni namna gani sasa ule uwanja uzungukwe na eneo maalumu la viwanda *(industrial park)* au *EPZ,* kama alivyozungumza mwenzangu. Pale tunahitaji tuwe na *cold rooms* za kutosha. Ule uwanja si kwa ajili ya Mbeya peke yake, ni kwa ajili ya Nyanda za Juu Kusini. Wenzetu wanalalamika kuhusu maparachichi yanaharibika; lakini huwezi kupeleka maparachichi, lazima yaandaliwe. Pia tunazalisha mazao mengi, matunda mengi na mboga mboga. Sasa tujiandae wakati huu ambao tumenunua ndege ya mizigo iweze kufanya kazi ya kusafirisha mizigo ambayo itakwenda kiushindani kwenye masoko ya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Rais vilevile kwa miradi ya umeme. Tumeenda vizuri na sasa hivi tunamalizia vijiji 40 vya mwisho ambapo nategemea

kabla ya mwaka huu vijiji vyote vitakuwa vimeguswa ili tuendelee na utekelezaji kwenye vitongoji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote hayo ili tuweze kustahimili na kukaa katika utulivu kwenye nchi yetu tunahitaji haya mambo yaweze kuendelea kama ilivyo sasa na yaboreshwe. Naomba Serikali iendelee kujenga barabara. Barabara ya *TANZAM* ni muhimu sana. Kipande cha kuanzia Igawa mpaka Tunduma kiko kwenye hali mbaya sana. Naomba Serikali ichukue hatua za haraka kwa sababu hii barabara inatuweka katika ushindani na Bandari yetu ya Dar Es Salaam ili iweze kushindana na bandari za nje. Kwa hiyo hili suala siyo la barabara ni suala la kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hiyo barabara napendekeza vilevile barabara ya Mbalizi-Shigamba, Mheshimiwa Waziri Mkuu uliahidi wewe mwenyewe hii barabara na ukasema hutaki tena usikie nauliza swali wala niongelee kuhusu hii barabara. Nakuomba mwaka huu kwenye bajeti hii, hii barabara iweze kujengwa kwa kiwango cha lami. Pia Barabara ya Isyonje-Ikondo nayo ni barabara muhimu kwa ajili ya kulisha uwanja wa Songwe. Vilevile barabara ya Mbalizi-Gadula naomba nayo ikamilishwe haraka kwenye bajeti ya mwaka huu. Pia *by pass* ambayo inaanzia Uyole mpaka Songwe nayo ni muhimu ikakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yote haya tunahitaji Serikali iboreshe reli ya *TAZARA*. Reli ya *TAZARA* ni muhimu; na mimi naweza kusema uboreshaji wake ni *quick wins,* haiitaji mambo makubwa. Nina imani Serikali ikitenga angalau bilioni 300 ile reli inaweza kuboreshwa. Kwa sababu ukiboresha reli ya *TAZARA* unakuwa umeweka mizigo asilimia zaidi ya 70 ambayo inapita Bandari ya Dar es Salaam kwa ajili ya soko la nje itapitia kwenye Reli ya *TAZARA* na bandari yetu itakuwa *competitive.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bandari yetu sasa hivi iko kwenye ushindani mkubwa na inawezekana tukashindwa kushindana kwa vile kuna Lobito ambazo ziko Angola. Wale wenzetu wametengeneza mpaka barabara za kuja kwenye masoko yetu. Vilevile kuna bandari za Afrika…

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa, inatoka wapi taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe taarifa kuhusu hoja inayozungumzwa sasa. Shirika la Reli la *TAZARA* ni shirika ambalo lilianzishwa kwa ubia wa Tanzania na Zambia sasa katika mgawanyo wa hisa ilikuwa ni kwamba Tanzania ina hisa 50 na Zambia asilimia 50. Sasa kuna changamoto ya kisheria, kwamba hakuna yeyote anayeweza kuongeza mtaji au akaboresha hiyo Reli akaongeza gharama kwa sababu bado atabaki na asilimia ile ile asilimia 50. Kwa hiyo namuunga mkono mzungumzaji ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa unapokea taarifa hiyo.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa mwenyekiti, naipokea hiyo taarifa, hayo ni mojawapo ya maboresha ambayo yanatakiwa yafanyike kwenye reli ya *TAZARA*. Ni kweli inahitaji maboresho kwenye mkataba na nina imani kwa vile Mheshimiwa Rais pamoja na Rais wa Zambia walikutana hivi karibuni na katika ajenda yao ilikuwa ni namna gani wanaweza kuboresha reli ya *TAZARA* kwa hiyo nina imani kwamba kwenye kipande cha Tanzania sisi tuchukue hatua zaidi ili twende mbele zaidi kwa sababu hili ni suala la ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwenye suala la umeme ninaomba Serikali ikamilishe haraka Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, lakini kwenye suala la kilimo ninaomba Serikali iangalie ni namna gani tukitumie kilimo kuleta fedha nyingi za kigeni, hasa kwa kuongeza uzalishaji tija ili bidhaa zetu ziweze kufika kwenye masoko ya kigeni. Leo bidhaa zetu nyingi zikiwemo kahawa na maparachichi zinauzwa kwa *label* za mataifa mengine. Huo ni upotevu wa fedha za kigeni. Na tunahitaji pesa za kigeni kwa sababu sasa hivi tuna matatizo ya urali wa biashara. Urali wa biashara sisi hatuko vizuri sana, bidhaa tunazoagiza nje ni kubwa kuliko bidhaa tunazopeleka nje. Hii maana yake nini…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umemalizika.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti,nashukuru sana naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Nilimtaja Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mheshimiwa Yahaya Omary Massare na Mheshimiwa Aloyce Andrew Kwezi ajiandaa.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kunipa fursa hii. Kwanza naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake aliyoitoa iliyosheheni mambo mengi sana. Katika hotuba yake Mheshimiwa alizungumzia uchumi wa dunia umeendelea kuyumba kama alivyoainisha katika ukurasa wa 15 aya ya 20 mpaka aya ya 25 ukurasa wa 18. Hata hivyo Tanzania chini ya uongozi wa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan imeendelea kuchukua hatua madhubuti kabisa na wote tunazijua zimefanya uchumi wetu usiendelee kuyumba. Ukuaji wa uchumi Duniani umeonesha umeshuka kutoka 6.2 asilimia mwaka 2021 mpaka 6.4 mwaka 2022. Lakini pamoja na

kuteteleka kwa uchumi duniani, sisi Tanzania tumeweza kujiimarisha kutekeleza mambo ya msingi kwa ajili ya jamii yetu kama kutengeneza mazingira ya shule, *infrastructure* za shule, zahanati, vituo vya afya, miradi ya maji, barabara, miradi ya umeme na treni ya mwendokasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali imeweza kutoa ruzuku katika maeneo ya makubwa ya mafuta na mbolea ili kuhimili mfumuko wa bei ambao tuliweza kufanikiwa kwani mwaka 2022 ilifikia wastani wa asilimia 4.3 kutoka kwenye asilimia 3.7 ya mfumuko wa bei kwa mwaka 2021. Kwa hiyo, hatua hizi zote zilizochukuliwa si kazi rahisi na watu wengine wanaweza kuwa hawayaoni haya au hawayafahamu, lakini wenzetu wa nje huko waliofanya tafiti kama hawa *Numbeo Business Inside Africa* imeripoti kuwa katika tafiti yao Tanzania kati ya nchi kumi Afrika ni nchi ya nane miongoni mwa nchi zenye gharama nafuu na ambayo imevutia wawekezaji kuja kuwekeza katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii si kazi ndogo, ni kazi ambayo Rais Samia ameifanya. Tunaposema anaupiga mwingi, ameifungua Tanzania ndio tunazungumzia mambo haya. Kwa hiyo, ili tuweze kuendelea kuimarisha uchumi wetu na kukuza uchumi wetu hatuna budi kuendelea kuhakikisha kwamba gharama za maisha tunaendelea kuzidhibiti, ndio kazi inayofanywa na Serikali yetu mpaka tumefikia hapo tulipofika.  Wote tunafahamu wawekezaji wowote katika nchi zetu hizi wanakuja kuona nchi ambayo ina gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kutokana na taarifa mbalimbali pia za *Business Insider* inasema kwamba *Tanzania is one of the first becoming the best investment destination in the world*. Hii ndio ripoti ya wenzetu na hii ni kwa sababu ya hali inayofanywa na imejidhihirisha katika miradi iliyoandikishwa na *TAC* katika mwaka 2023 Februari, imeongezeka *by hundred and twenty eight percent*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaonesha *significant potential growth* ya uchumi wetu nchini. Kwa hiyo, *TIC* imeorodhesha miradi hii gharama yake ni *million dollars* 339 sawa na zaidi ya Shilingi Bilioni 780 na itaenda kuajiri watu 7,370. Kwa hiyo ni kazi kubwa sana hii ambayo inafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudi nyumbani Namtumbo. Kwanza tunaomba tuishukuru sana Serikali, katika kipindi hiki Serikali imeweza kutusaidia sisi zaidi ya shilingi 15,820,000,000 kutekeleza miradi mbalimbali. Katika afya tuliweza kupata shilingi 5,318,000,000 ambayo tumejenga majengo ya upasuaji katika hospitali ya Wilaya, wodi na tumejenga majengo ya Mama ngojea, katika kipindi hiki tumejenga *mortuary* na jengo la mama na mtoto zenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni tano tulizozipokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumejenga vituo vya afya katika Kata ya Magazini, Kata ya Ligela na miundombinu ya uboreshaji wa maji katika vituo vyetu vya afya. Vile vile tumeweza ukamilishaji wa zahanati na tumemaliza kuzijenga Ukiwayuyu, Misufini, Songambele, Naholo, Mhangazi, Luhangano na tunaendelea na zahanati zingine kama Namanguli, Nhamali, Ulamboni na Chengena katika kipindi hiki chote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki tumepata vifaa tiba vya thamani ya shilingi 758,848,000. Vilevile tumeweza kupata katika elimu, Serikali imetuletea shilingi 7,564,000,000 katika kuendeleza ujenzi. tumejenga shule ya sekondari ya wasichana kati ya shule kumi zilizojengwa nchini Tanzania, moja iko Namtumbo tumejenga kwa shilingi bilioni nne na shule hiyo iko mwishoni kukamilika. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuja kuitembelea na kuweka jiwe la msingi katika shule ambayo tumeiita *Dr. Samia Suluhu Hassan Secondary School.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejenga pia Shule ya Sekondari katika Kata ya Mzizima, lakini vilevile tumejenga madarasa 86 yenye thamani ya zaidi ya shilingi 1,720,000,000. Vile vile tumeweza kujenga maabara katika shule zetu za sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sekta ya maji; tumeweza kupata zaidi ya shilingi bilioni mbili na milioni mia tisa katika miradi mbalimbali ambayo tumeweza kukamilisha Mradi wa Maji Namtumbo Mjini, tumeweka *line* mpya na leo imepunguza adha waliyokuwa wanapata wananchi, walikuwa wanapata maji siku saba mara moja kwenye mgao, lakini leo angalau imepunguza adha hii. Kuna maji Litola-Kumbala tumeweza kufanikisha kupata maji lakini Luhimbalilo na Ikesi nayo kazi inaendelea. Vilevile maji Masugulu nayo shilingi milioni 578 kazi imekamilika na maji watu wanakunywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika barabara; tulipata zaidi ya shilingi bilioni mbili na milioni mia tano, tumeweza kujenga daraja kubwa Mto Luwegu. Mto Luwegu unatokea Namtumbo, kwa hiyo tumejenga pale daraja kubwa ambalo sasa hivi linawasaidia wananchi kuvuka. Vile vile tumejenga barabara za vijijini, fedha hizi tulizipata za *TARURA* ila tunaweza kuiomba Serikali tuna changamoto, tunaomba kwenye barabara, tuna barabara yetu ya Mtwara Pachani kupita Mkongo – Lusewa – Magazini mpaka Tunduru, hii barabara ni ya kiusalama, lakini vile vile ina eneo ambalo wanakaa watu wengi sana. Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali ifikirie kuitekeleza Ilani ya Uchaguzi, ipo katika ukurasa wa 73, ahadi ya Ilani wa Uchaguzi wa 2020 - 2025. Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali ifanye ifanyavyo iweze kutekeleza ahadi yake ya kujenga kwa kiwango cha Lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru barabara ya kutoka Lumecha – Kitanda mpaka Malinyi iko katika hatua

nzuri ambayo tuko katika hatua za manunuzi, tunaamini kabisa tutaweza kufanikiwa kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia changamoto tuliyonayo ni Kilimo. Kilimo tunashukuru sana mwaka 2022 tumepata mbolea za ruzuku, lakini mbolea hizi hazikufika katika maeneo ya vijiji vyetu. Tunaomba kama alivyosema leo Naibu Waziri asubuhi kwenye swali aliloliuliza Mama Anne Kilango, tunaomba utaratibu wa mwaka huu uende kama ulivyopangwa. Mbolea ziwafikie wakulima mapema. Tunashauri taratibu za manunuzi ya mbolea zianze mwezi huu Aprili ili mpaka mwezi wa Julai au Agosti mbolea ziwe zimeshafika nchini, ziwe zimesambazwa ili kama kuna changamoto tuweze kuzitatua changamoto hizo kabla ya wakati wa msimu kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, naomba sana pia Serikali yetu isaidie, sisi tuna changamoto ya Kituo cha Mabasi katika Wilaya ya Namtumbo, tunaomba sana itufikirie. Hatuna kituo chenye hadhi ya Wilaya, vile vile hatuna soko. Sisi ni wakulima tuna mazao mengi lakini hatuna soko la mazao Namtumbo. Tunaomba Serikali itufikirie katika eneo hili. Hii ni changamoto mojawapo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tuna changamoto ya ukarabati wa Vituo vya Afya kongwe vitatu ambavyo vilijengwa miaka ya 1970; Mkongo, Lusewa na Mputa. Vituo hivi nasema ni kama zahanati, kwa hiyo vilijengwa miaka ile na vina upungufu wa majengo na vimechoka sana. Kwa hiyo, tunaiomba sana Serikali iweze kutusaidia katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwingiliano kati ya wakulima na wafugaji ni changamoto kubwa sana kwenye eneo letu. Sisi ni wakulima na nchi hii inategemea sana kilimo. Kwa hiyo tunaomba sana Serikali izingatie hili ije, haijawahi kuja toka nimeanza kuzungumza changamoto hizi hadi watu

wamekufa hajawahi kuja Waziri wa Mifugo. Tunaomba Waziri wa Mifugo aje aone changamoto tuliyokuwa nayo. Mifugo inatusumbua sana sisi wakulima na sisi katika maeneo yetu nchini kuna maeneo sasa hivi yana uhaba wa mvua lakini kwetu sisi tuna mvua nzuri na sisi ndio ghala la chakula kule. Kwa hiyo, kukiwa na mwingiliano wa wakulima na wafugaji tutashindwa kulima na tutashindwa kuzalisha nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba kuishauri Serikali, ili kuendeleza uchumi wa nchi yetu na kuulinda lazima tu-*focus* zaidi kwenye *export oriented industrialization* ili tuweze ku-*concetrate* kuzalisha mazao tutakayokuwa tunauza nje ya nchi. Tukiwa na mazao na viwanda vinavyozalisha mazao ya kuuza nje ya nchi itatusaidia kuuza nje kwa sana na kutoa *foreign exchange*. Kutoa mifano ya nchi wenzetu walioendelea ambao tuliuwa nao katika miaka ya 1960 nchi za Asia pale *Tiger* ambao wao miaka ile walianza ku-*concentrate* kwenye hivi viwanda vya kuzalisha vitu vya kuuza nje, leo wanauza nje sana na uchumi wao wa *Tiger* kule umekuwa mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu huo ulikuwa ni huo. Naomba sana kukushukuru ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Vita. Sasa tunaendelea na Mheshimiwa Yahya Massare, Mheshimiwa Aloyce Andrew Kwezi na Mheshimiwa Ester Bulaya wajiandae.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi hii. Nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri ambayo ina dhamira njema sana tu kwa nchi hii lakini imekuwa yenye dira nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuipongeza Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Rais wetu Mama yetu

Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa weledi mkubwa na kazi nzuri anazozifanywa katika majimbo yetu. Mheshimiwa Rais amekuwa kielelezo chema kwa utendaji wake wa kazi ambazo kule vijijini na hasa sisi majimbo ya vijijini tumenufaika sana kwa kiwango kikubwa mno. Vilevile pesa ambazo zimekuwa zikielekezwa chini kabisa kwenye halmashauri zetu ambako zimeenda kwenye afya, maji, elimu, miundombinu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya dakika hizi chache itoshe tu niseme kwamba kazi nzuri sana sana na wananchi wameona matunda makubwa kabisa. Wameona zahanati zetu, wameona vituo vya afya, wameona hospitali za halmashauri zetu lakini miradi ya maji kule vijijini pamoja na kuchimbwa visima ambavyo wanaendelea navyo. Pia katika elimu tumeona baadhi ya shule mpya kabisa zikijengwa, lakini madarasa yanaongezwa katika shule ambazo zilikuwa na upungufu mkubwa wa madarasa lakini sekondari zetu, kuna kiwango kikubwa sana cha pesa ambacho kimewekezwa kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoendelea kuipongeza Serikali, lakini tunapaswa pia kushauri yale mazuri ambayo tunadhani kwa maono yetu yanaweza kuwa na tija kwa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi hiki ni kipindi cha bajeti. Mwaka 2022 kipindi kama hiki pia tulipitisha bajeti mbalimbali za Serikali yetu. vile vile tunapokuja kwa mwaka mwingine tunatamani kuona matunda na matokeo mazuri, matokeo chanya ya bajeti zile ambazo tulizipitisha hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya bajeti ambayo watu walipiga sana makofi na kuisifu ni bajeti ya Kilimo. Serikali iliamua kuongeza kwa makusudi kwa kiasi kikubwa sana bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa zaidi ya asilimia 300 na ni bajeti ambayo tuliamini matokeo yake yatakuwa bora sana. Hata

hivyo, tuna mambo ambayo Watanzania watu wanatushangaa sana, tuko mbioni, tuko katika mchakato, karibu tu, yaani hatukamilishi mambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kilimo walikuja hapa katika *gallery* hizi Maafisa Ugani wakiwa wamevalishwa sare nzuri sana na sisi tukashangilia kwamba sasa kilimo chetu kinakwenda kukomboka, tunatoka katika kilimo hiki duni, tunakwenda sasa katika kilimo ambacho kitakuwa na maslahi mapana. Vile vile walipewa pikipiki, Mheshimiwa Rais wetu ndiye aliyewagawia wale watu na sisi tukishuhudia, walipewa vifaa vya kupimia udongo ambavyo naamini dhamira yetu iwe basi ni kwa msimu ule mmoja tuone matokeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wanagawiwa pikipiki, wanavalishwa magwanda hapa tunaona na tunapiga makofi, wakulima wetu ambao ni wakulima kabisa, wakulima *per se* walikuwa wanalima na wengine walikuwa wanavuna. Miongoni mwao baada ya muda mfupi walianza kuuza mazao yao kwa mashirika makubwa, Taasisi kama *NFRA,* Bodi ya Mazao Mchanganyiko lakini na watu binafsi ambao ni wajasiriamali wanaonunua dengu, kunde, choroko walienda kununua kwa wakulima wale ambao siku zote maisha yao ni ya kulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuja na mipango ambayo Mawaziri hao vijana wametupa mipango mizuri sana, lakini mashaka yangu, hatuoni manufaa ya mipango hii mizuri. Toka bajeti iliyokwisha mpaka tunaingia katika bajeti nyingine hakuna matokeo ya zile pesa ambazo zilitolewa nyingi kwamba zimesafisha shamba hekari ngapi? Watu mia ngapi wanakwenda kulima? Wamevuna kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango yetu ya bajeti ni ya mwaka mmoja mmoja. Ni mipango tu ndio huwa ya miaka mitano na dira zinakuwa za miaka 25 kwa maana

zinagawanywa 25 au 50 tulikuwa tuko pale kwenye maoteo nadhani ya dira ile ambayo baadaye itakuja tuichakate, lakini mipango ya miaka mitano huwa ni mipango ya mambo mengi, lakini Ilani za Uchaguzi nazo huchukua miaka mitano maana yake mpaka uchaguzi mwingine mtakuwa mmetimiza yale malengo yenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kilimo bado hili linanitatiza. Kilimo cha Tanzania asilimia kubwa ni cha mvua. Sasa kama tulitoa pesa nyingi na bado tuko katika dhamira ya kutegemea kilimo cha mvua maana yake tuwe na mipango ya mwaka mmoja mmoja, lakini kama ni kilimo cha umwagiliaji, basi tungekuja hapa kwamba tumeshachimba angalau mabwawa 20 katika halmashauri 20 au majimbo 20, lakini tuko katika mchakato, tuko mbioni, ndio mipango yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona wanachukua vijana, dhamira njema sana, lakini vijana watatu katika halmashauri au wanne au watano wale waliopendelewa, wana *impact* gani katika kilimo cha nchi hii ambacho tunategemea tuka-*achieve* nini? Tunaenda kupata kitu gani kwa vijana watatu katika Halmashauri ya Itigi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao wakulima ambao siku zote wanalima. Kwa nini tusiwapelekee pembejeo za kutosha zile pesa tukaingiza kwenye ruzuku za trekta, wale wale wanaolima kama ni kuwasafishia mashamba, tukawasafishia wale wale vijana ambao siku zote wanalima, kuliko kuwachukua vijana na Kuwafungia Bihawana kwa miezi minne wanajifunza nini wakati Maafisa Ugani tunao? Hao waliowaleta hapa kazi yao nini? Unamfundisha mkulima kwa miezi minne na huyo Afisa ugani anafanya kazi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vijana wetu walimaliza Vyuo vya Kilimo *SUA* na vyuo vingine, kwa nini tusichukue watu wenye weledi wa kutosha kama kweli tuna dhamira ya

kuajiri watu waajiriwe na kilimo? Kwa nini wale waliosoma kilimo tusiwape hiyo nafasi? Tukachukua mtu ambaye alikuwa amekaa nyumbani ambaye hajawahi kulima na kwa sababu unataka kumfundisha ili kwa sababu ana shida ya ajira, atakuja kusoma hilo somo ambalo unamfundiha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mfano mmoja ambao ume-*fail* hapa hapa Dodoma, shamba lile ambalo Mheshimiwa Rais alipita pale Chinangali lilikuwa Shamba la Ushirika wa Wakulima wa Zabibu waliwezeshwa na Halmashauri ya wilaya ya Chamwino, Benki ya *CRDB* iliwakopesha Dola Milioni moja kama Bilioni 1.6 wakati ule, lakini baada ya kulipa mkopo hakuna kilichoendelea, kwa sababu dhamira yao ilikuwa sio kilimo, ilikuwa ni fursa. Wangekuwa ni wakulima wangeendelea kulima kwa sababu walipewa mashamba bure na kwa sababu ilikuwa ni fursa ya ajira, walipomaliza kulipa ule mkopo na yule Meneja aliyekuwa anawasimamia, aliposema sasa nawaachieni basi lile shamba limekufa, leo tunalichukua katika utaratibu mwingine. Mfano huu ndio huu ambao tunakwenda kuuendeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali tukawezeshe wakulima ambao kila siku wanalima. Tusilenge zao moja, kama mkulima wa parachichi ajengewe uwezo kwenye zao lake, kama mkulima wa mpunga ajengewe uwezo kwenye shamba la mpunga, kama mkulima wa mahindi tumwekee uwekezaji wa kutosha katika kilimo cha mahindi ili tupate matokeo mazuri kwa muda mfupi. Vile vile mipango hii ya muda mrefu ya mchakato na tuko mbioni iendelee kwa sababu ndio mipango yetu mingi. Kwa nini tusiwe na matokeo ya haraka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wakulima ambao waliuzia *NFRA* chakula, chakula kikaanza hadi kupelekwa nchi jirani na sisi tumesema tutakuwa *hub* ya chakula nchi hii. Kwa nini tusiwasaidie hawa wakulima wa Meatu, wakulima kule

Iramba, wakulima wa kule Madaba, wakulima wa kule Itigi, pale alipo ardhi itengwe, kama ni hekari mia tano mia tano kila halmashauri halafu zikasimamiwa au kila jimbo. Hivi kweli ukimwezesha Mbunge kupitia halmashauri yake ile pesa atakula wakati anatengeneza kula zake? Inawezekana wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais hapa alileta shilingi bilioni moja za barabara kule Vijijini kwetu tulinufaika sana na mpaka leo watu wanasifia haya yanayootokea, kwa nini sasa na ninyi wa kilimo msiishushe kule chini? Hela hizi zikaenda kwa watu ambao moja kwa moja ni wakulima na wakafanye kazi za kilimo ili kilimo kiwe na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana nimeona umewasha *microphone,* naunga mkono hoja hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Massare. Nilimtaja Mheshimiwa Aloyce Andrew Kwezi, Mheshimiwa Ester Bulaya na Mheshimiwa Shamsia Mtanda wajiandae.

**MHE. ALOYCE A. KWEZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi njema anayoifanya katika nchi yetu ya kutuletea maendeleo ya kweli. Nitakuwa sijatenda haki endapo sitampongeza Mheshimwa Waziri Mkuu kwa ripoti yake nzuri sana, ripoti ya Waziri Mkuu na bajeti yake hapa kwa kweli ni ripoti ambayo imekwenda shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nianze kuchangia katika sekta ya Maliasili. Jimbo la Kaliua limepakana na Hifadhi ya Ugalla, Hifadhi ya Kigosi ambazo zote hizi ni *National Parks,* pia Jimbo linalo ofisi za *TAWA* na *TFS*. Nimesimama ili tuweze kujenga hoja na kushauriana mambo mbalimbali kwa ajili ya kuwashauri Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Mawaziri lilifanya maamuzi katika vijiji 975 katika Jimbo la Kaliua na katika Wilaya ya Kaliua liliachia vijiji na kuvitambua vijiji 29, walipokuja timu ya Mawaziri Nane, mimi ni miongoni mwa mashuhuda ambao nilishiriki mchakato mzima katika Jimbo la Kaliua, Mkuu wangu wa Mkoa Dkt. Batilda Buriani ameshiriki mwanzo mwisho, Mwenyekiti wa Chama wa Mkoa naye alishiriki mwanzo mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ambayo ninaijenga inahusiana na Kata inaitwa Ukumbisiganga. Katika Kata ya Ukumbisiganga kuna vijiji viwili, Kijiji kimoja kinaitwa Kumbikakoko na Kijiji cha pili kinaitwa Usinga, Vijiji hivi kwa sasa kumeibuka mgogoro mkubwa sana lakini mgogoro huu umetokana na tathmini iliyofanywa na wataalam. Baraza la Mheshimiwa Rais ameruhusu na kuvitambua vile vijiji ambavyo vipo pale toka mwaka 1974, walikuja wakatangaza wananchi kaeni, tulieni, Mheshimiwa Rais amesikia kilio chenu lakini bado amewaonea huruma na mimi nikashukuru kama Mbunge wao, bado chama kikashukuru kwa mapenzi mema ya Mheshimiwa Rais wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho kimekuja kutokea hivi sasa ni ile timu ya tathmini imekuja na mapendekezo ambayo ninaweza nikasema kwamba yale mapendekezo sijawahi kuona na nimeona ni kama vile hizi shule kwa kweli saa nyingine hazitusaidii. Hizi shule hazitusaidii kwa sababu gani? Agizo limesema wananchi wakae, wamegewe maeneo lakini badala ya kumegewa maeneo nini kimekuja kufanyika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wananchi kaya 318 kwenye Kijiji cha kwanza kinachoitwa Ukumbikakoko zimependekezwa zitoke Ukumbikakoko ambapo *almost* ni Kijiji kizima hicho, maana yake ni tofauti ninaona kama vile kijiji kinafutwa sasa, ziondolewe Ukumbikakoko ambayo ndiyo

mwisho jirani na Mpanda, kwa hiyo mtu anatoka Makao Makuu, kutoka Makao Makuu ya Kata mpaka ukafike Ukumbikakoko ni kilometa 38. Sasa mapendekezo badala wamegewe yale maeneo ambayo yalikuwa yamependekezwa na hakuna mgogoro wowote, wanasema kaya 318 zitoke pale Ukumbikakoko zivuke Kijiji cha Usinga, zivuke Makao Makuu ya Kata, zivuke Kijiji cha Lumbeyi ziende kuingia kwenye Kata nyingine inaitwa Zuginole kilomita 58 kutoka Kijiji kilipo, halafu zile kaya zinazohamishwa hizo 318 kila kaya iende ikapewe heka tano tano, nilicheka nikasema hii ndiyo shule haijasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kwenye vijiji tujiulize Waheshimiwa Wabunge wote tunatoka kwenye vijiji, mimi ukiniuliza katika Kijiji ambacho natoka kwenye eneo la Baba yangu ni zaidi ya heka 1,000 familia nzima tunalima pale, kwa hiyo kaya moja na kaya za kule ninavyowaambia Kaliua kwa Sensa iliyofanyika ina watu 668,000, badala tufikirie kwamba tutawasaidia hawa sasa hii ni *allocation* mbovu. Eneo lipo pale wazi badala waongeze lile eneo ambalo lipo jirani pale wanakwenda sasa wanavuka vijiji vinne mpaka wanakwenda kuwa-*dump* kwenye Kata nyingine, sasa unajiuliza kwa kweli hapa si ndiyo tunafuta, sasa kuna Kijiji pale? Hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kijiji cha pili kinaitwa Usinga. Kile Kijiji cha Usinga kina kaya 937 zilizopendekezwa kuondolewa kwenye kile Kijiji, hebu pigeni mahesabu ndugu zangu kaya 937 zitoke kwenye eneo lake sasa zinakwenda wapi? Zenyewe zinakwenda kilometa 42 kutoka zilipo, hizi kaya 937 ambazo Rais huku amesema ameona huruma kwa wananchi, wakalishwa na kiapo, Mbunge wao pia nikabebwa na Mawaziri kama Nane walikuwepo pale wakati wanatoa kila kitu, mwaka mmoja umeisha ni mambo mengine.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambie Serikali na kuwashauri, kwanza watambue yale maeneo tumeyatunza, mimi nimezaliwa Ukumbikakoko iko pale, Usinga ipo pale, lakini Mheshimiwa Rais kwa sababu anatupenda tunavyoongea kuna miradi ya maendeleo inaendelea pale. Upo mradi wa maji milioni 440 unaendelea, Stesheni ipo pale, pia jirani zetu wa Mpanda ninavyoongea *almost* ni mita 500 naianza Mpanda kuna kijiji pale, lakini unakuja kuona maelekezo ndiyo maana nikasema utaalam mwingine! Kwa kweli nimeshamuelewa sasa hivi Dkt. Musukuma namuita Daktari kabisa, kwa sababu sasa ile *informal education* ndiyo naiona umuhimu wake, mmenielewa ndugu zangu? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kama mtu umeenda shule unasema kwamba haya vijiji vyote vinaondoka, huku miradi Rais analeta pale inaendelea, zahanati zipo, shule zipo, stesheni zipo na sasa mmeanza kukarabati reli ya kutoka Kaliua kwenda Mpanda tayari wanajenga tena kulekule sasa hii ni nini? *The same Government* huku tuna-*argue* hiki hapa, huku mna-*argue* kitu kingine hiki hapa! Kiongozi mmoja naye anakuja anatamka kwamba msipeleke miradi ya maendeleo huku Rais ana miradi pale inaendelea, madarasa yanaendelea pale hivi ni kitu gani hiki? Miezi michache tu nyuma wametoka pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kwa kweli kwenye suala la Ukumbikakoko na Usinga ni suala ambalo mimi binafsi limeniuma sana, kwa sababu sikutarajia! Huku tamko ni hili hapa, agizo ni hili hapa lakini kinachokuja kutekelezwa ni tofauti kabisa na kile ambacho kiliamuliwa huko. Sasa maana yake nini? Tena wakanitania Viongozi wangu kule kwamba sasa nenda kawahamasishe kule nikawaambia siwezi kwenda kula matapishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliniambia pale Mheshimiwa Mbunge kazi imefanyika wakanipamba kweli kweli nikabebwa juu, sasa agizo bado lipo pale hiki kilichotokea ni kitu gani cha kubadilisha? Shida ni nini? Kama maendeleo yote haya yapo. Hivi kuna kaya ambayo hamuifahamu kabisa kwenye Kijiji kuna kaya ambayo ina heka 300, heka 400 mpaka unafikia eti heka tano tano au ndiyo zile Mheshimiwa Mbunge mmoja alisema humu kwamba tunapokuwa na zile *garden* zetu tunafikiri ni mashamba, tunawa- *frustrate* watu, umefanya maamuzi "A" leo unakuja kuyakataa maamuzi yako au unashauri vinginevyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali ipitie upya ile timu ya tathmini kama walikwenda pale tena na wahusika wakubwa ni *TFS* wa kule fuatilieni mtusaidie kufanya maamuzi sahihi, na hili nakuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu ulikuwa pale, hivi vijiji navitaja ulikuwa kwetu unatutumikia Baba tena mtiifu, mwadilifu naendeleza kazi yako, hebu tuoneeni huruma vijiji vya Kumbikakoko unavijua, mpaka sasa hivi tunavyoongea ndicho kinachoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hilo lifanyiwe kazi tena haraka ili kuondoa *frustration* kwa sababu wengine wanaanza kusema usipeleke hela, usipeleke hela kwa kigezo gani? Huku miradi ya umeme inaendelea kule maana yake nini? Tunashindwa kuwa na kauli moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema haya ambayo yalikuwa yanagusa vijiji viwili ningependa nichangie jambo jingine. Kule kuna kuna barabara inapita ya kutokea Mpanda – Kaliua – Uliankuru - Ushetu mpaka Kahama iko kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi na tayari wemeshafanya *detail design* kule na kwenye bajeti wamependekeza kujenga daraja la Ugalla, sasa mnajenga kwa ajili ya nani? Hizo Stesheni ambazo mnaboresha kwa ajili ya nani? Kama mnapendekeza wananchi huku kwamba kuna moja, mbili, tatu hakuna madhara tumetunza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo hifadhi mnaziona tumetunza, tumehangaika sisi na ndiyo maana maeneo yote tunapokaa hatuna hata mgogoro na mtu lakini kwa vijiji hivi nimeona kama maamuzi yanayofanywa, maamuzi yalifanywa sahihi na Rais wetu anayetupenda na timu yake yote ya Mawaziri huko chini huku kuna shida kinachotokea ni kingine, halafu agizo liko hivi kwamba Wilaya na Mikoa ishughulikie kuhamisha, wanahamisha wanawalipa nini? Hizo nyumba zao? Nikasema sasa hiki, yaani mimi nilichanganyikiwa! Kwa hiyo naomba tufikirie maamuzi sahihi kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wa Kaliua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuchabgia pia kwenye mradi mwingine, mimi nachangia kwenye barabara. Tunae Mkandarasi anaendelea kutoka Kazilambwa kwenda Chaya kilometa 36 ameshapita Usinge ile *bypass* ya Usinge shida bado nini, kwa sababu tayari mainjinia wetu wa Mkoa kila kitu wameshawasilisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini *bypass* ya Usinge ile kilometa Saba mliyoahidi Waziri wa Ujenzi kwa nini hamuanzi kuijenga mpaka muda mkandarasi uishe tuingie kwenye gharama na hoja zisizokuwa na msingi tuanze kuleta wakandarasi wengine, *mobilization ya material* na mambo mengine yaendelee. Mradi wa ufadhili hela ipo shida nini? Mimi kwa kweli napata wakati mgumu tunakuwa na kigugumizi kufanya maamuzi kwa sababu gani? Mkandarasi yupo na mambo yanaenda kwa nini tunakwama? Kwa hiyo, naomba ile *bypass* ya Usinge barabara ya kilometa saba ianze.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo ningependa kulichangia. Tabora ni wakulima wa tumbaku na tumbaku inayozalishwa karibu Tanzania ni kilo milioni 44, kilo milioni 22 inatoka katika Wilaya ya Kaliua, kuanzia tarehe 20 tunakwenda kwenye masoko, sasa kule kwenye masoko

nawaomba wale Wateuzi wa Serikali huwa wanafanya tathmini wakishatoka bei inayokuja wananchi wanakuja kupunjwa, haifuatwi ile bei ya wateuzi wa Serikali iliyofanyiwa tathmini, kwa hiyo masoko tarehe 20 niombe tuende vizuri, wananchi wauze tumbaku yao vizuri na mtuongeze mteuzi, mteuzi ni mmoja tu kwa Majimbo yote siyo sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti baada ya kuyasema haya ninaomba Serikali iyafanyie kazi kwa umakini ili tuondoe taharuki ambayo inajitokeza kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja naunga mkono Bajeti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Aloyce Andrew Kwezi, nilimtaja Mheshimiwa Ester Bulaya, Mheshimiwa Shamsia Mtamba, Mheshimiwa Ng'wasi Kamani na Mheshimiwa Festo Sanga wajiandae.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Amiri Jeshi Mkuu wa Nchi yetu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amekerekwa na ubadhilifu, mimi ni nani Ester Bulaya niuchekee? Kama Waziri Mkuu wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amesikia kwenye ziara zake mbalimbali akikemea ubadhilifu mimi Ester Bulaya mwakilishi wa wananchi ni nani niuchekee na hasa jicho likiwa limefanya kazi yake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumsaidia hivyo hivyo Rais kwa kuisaidia Serikali iweze kuchukua hatua lazima tuonyeshe kwenye mapungufu hatua zichukuliwe nchi yetu isonge, maendeleo ya Taifa yaonekane kwa wananchi wake.

Mheshimwa Mwenyekiti, kwa utangulizi naanza. Kikokotoo Wafanyakazi bado wanalia, tusitengeneze mgomo baridi, hawa ndiyo wanaoenda kutekeleza miradi ya maendeleo, najua mnasikia, najua mmeona na najua mkiamua kulifanyia jambo mnaweza, bado asilimia 33 si haki yao, maisha magumu Wafanyakazi wanalia wanafanya kazi kwa kinyongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 14 wa Waziri Mkuu, hotuba yake ameisoma vizuri tu hapa, kuzungumzia miradi ya kimkakati na anazungumzia mradi wa Mkulazi ambao amesema upo asilimia 75, tunataka majibu ya kina hapa kuna fedha za Mifuko zimewekezwa. Je tathmini ya kina ilifanyika? Maana ripoti mbalimbali za *CAG* zimeonesha hapa pametengeneza hasara ya bilioni 11 sawa na asilimia 21 ya mtaji uliowekezwa, Mkulazi hapa. Moja ya sababu inasemekana kulikuwa kuna ucheleweshaji wa mashine. Sasa ukienda ya mwaka huu inasema hiyo mashine aliyepewa tenda ya kununua mtambo wa kutengenezea Kiwanda cha Sukari ni Wakala wa Barabara *TANROADS,* wapi na wapi! Kwa nini haikuwa *TEMESA*, kwanini haikuwa wakala wa kuagiza vifaa Serikalini, *TANROADS,* barabara wa sukari wapi na wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kuna fedha za Kimarekani takribani milioni 50.8 na inasemekana mbali ya kwamba na huu mkataba ambao Mkulazi hawajashiriki hata kuweka Saini, kila kitu walifanya *TANROADS*. Kuna nyongeza ya bilioni 11 na hatujui kwamba Mwanasheria Mkuu alithibitisha kwa mujibu wa Kanuni ya 59(1) cha manunuzi. Tunataka majibu ya kina, haya tunayasema kwa sababu tunataka hatua zichukuliwe, watu wasiichukulie Serikali poa, watu watimize wajibu wao, hizi ni fedha za wastaafu wetu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni Mkulazi bado kiwanda cha Ngozi cha Kilimanjaro hasara Bilioni Nne, fedha za Mifuko

ya Hifadhi ya Jamii shilingi bilioni nne. Katika malengo yao hicho kiwanda kipya cha Kilimanjaro kilikuwa kimepanga kuzalisha jozi za viatu 1,200,000 wakazalisha 11,354, kilikuwa kimepanga kuzalisha jozi za sori za viatu 900,000 kikazalisha sifuri. Kilikuwa kimepanga kuzalisha bidhaa za ngozi 48,000 kikazalisha 224, kilikuwa kimepanga kuzalisha ajira 300 kikazalisha 79. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo hayajafikiwa usimamizi mbovu kwenye pesa za wastaafu zinazoenda kuwekezwa kwenye viwanda. Wakati haya yanafanyika bado mifuko iko hohehahe *PSSF* tena ripoti mpya ambayo tutaenda kushughulika nayo huko mwezi wa Agosti, *PSSF* imesema Mfuko ukwasi upo asilimia 22 kinyume na sheria cha asilimia 40. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana nimesema na leo narudia, wakati hizi pesa zinaendelea Trilioni 1.5 pesa za muda mrefu hamjalipa kwenye Mifuko tuliahidiwa na Waziri wa Fedha akalipa kwa Hati Fungani nyingine hamjatoa, wakati haya wanaendelea Mfuko wa *PSSF* umelipa bilioni 767 pesa za Wastaafu, kiinua mgongo chao zaidi ya mapato waliyonayo kuna mwaka walienda kukopa kwenye maeneo mengine, kiasi walicholipa ni kingi kulingana na mapato ya michango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati haya yanaendelea kuna mashirika manne hayajapeleka michango takribani bilioni 129 kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, wakati haya yanaendelea kuna Mamlaka ya Serikali za Mitaa 133 hazijapeleka takribani bilioni 119 maslahi ya mishahara na posho za wafanyakazi hazijalipwa. Wakati haya yanaendelea kuna mashirika nane hayajalipa malimbikizo ya mishahara ya watumishi na madeni mbalimbali takribani bilioni 5.8, bilioni 2.2 ni malimbikizo ya mishahara. Wakati haya yanaendelea kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuna

Mamlaka 76 hazilijalipa milioni 309 za mizigo za wastaafu 223. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayasema haya kwa sababu tunataka nchi yetu iende, haya mambo Bunge tumekuwa tukiyaongea mara kwa mara na Serikali haifuati maagizo ya Bunge. Niwaambie tu kwenye maagizo ya Bunge 892 ya Kamati ya *LAAC* yaliyofanyiwa kazi ni asilimia 26 tu, yamefanyiwa kazi maagizo 228. Kwa nini Hoja za Ukaguzi zisijirudierudie? Hapo kuna maagizo 159 ya Bunge lako Tukufu hayajafanyiwa kazi takribani miaka 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge lazima tutimize wajibu wetu, tuibane Serikali itimize wajibu wake, tumsaidie Mheshimiwa Rais ameonesha makasiriko yake ya kukerwa, lazima kama Wabunge, kama Taifa tusimame imara, hatumtafuti mtu hapa, tunataka tuwatendee haki Watanzania fedha zao ziende kwenye miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haya Maagizo ya Bunge hayafanyiwi kazi, kwa nini Wakurugezi kule wasifanye mambo wanayojitakia kwenye Halmashauri? Kwa nini pesa za vikundi zisipigwe takribani shilingi bilioni 88? Kwa nini asilimia 40 za kisheria zinazopaswa zikusanywe na Halmashauri hazikusanywi? Kwa sababu Bunge tunatoa maagizo, hamsikilizi. Tunaomba haya maagizo yakafanyiwe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua Mheshimiwa Waziri Mkuu ni mnyenyekevu, tunaomba watumishi watimize wajibu wao. Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, madeni yalipwe. Watumishi pesa zao kwa mujibu ya sheria, michango ipelekwe. Kwenye uwekezaji kuwe na tija. Ifanyike tathmini ya kina ili hizi pesa za hawa watumishi wa umma ambao ni wastaafu watarajiwa, huku wanapigana na *stress* za kikokotoo, huku pesa zao hawajui huko zilikoenda zitarudi kiasi gani? *Please!* Naomba sana tuwatendee haki Watanzania, tuwatendee haki

watumishi wa Taifa hili. Haya tunayopanga, wao ndio wanaenda kutekeleza, hawataenda kutekeleza wakiwa na *stress,* hawajui hatima yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ester Bulaya. Tunaendelea, nilimtaja Mheshimiwa Shamsia Mtamba, halafu Mheshimiwa Ng'wasi Kamani, na Mheshimiwa Festo Sanga, wajiandae.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kuchangia hotuba hii ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya nzuri na leo hii nikaweza kusimama katika Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nitaanza kwa kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuhakikisha Watanzania wa mijini na vijijini wanapata maendeleo. Kwa hakika wanawake tunaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze kwa dhati Waziri Mkuu kwa kuguswa katika Jimbo la Mtwara Vijijini, tulipopata maafa makubwa kweli ya mafuriko. Tunamshukuru sana kwa kuchukua hatua ya haraka kuwafikia wahanga wa mafuriko na kutupatia misaada ya kibinadamu. Kwa kweli Mheshimiwa Waziri Mkuu wananchi wa Jimbo langu hasa wa Kata ya Kivava, Kata Mahurunga, Kijiji cha Kivava wanakushukuru sana. Misaada imewafikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Mkuu wangu wa Mkoa wa Mtwara, Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, na

vyombo vya ulinzi na usalama vyote, kwa kweli wamefanya kazi kubwa ya kuhakikisha wahanga wa mafuriko wapo katika sehemu nzuri na wanapata huduma nzuri. Ninawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nitazungumzia sehemu tatu. Kwanza, nitaanza kuzungumzia kuhusu Wizara ya Uchukuzi. Tokea nimekuwa Mbunge katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nimekuwa nikizungumzia sana suala la barabara; barabara ya ulinzi na pia barabara ya uchumi inayotoka Mtwara Mjini kuelekea Msimbati ambako kuna mitambo na visima vya gesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna barabara yetu ya ulinzi, ina umuhimu mkubwa sana. Barabara hii ni muhimu Serikali iiangalie kwa macho mawili kwa sababu itaweza kulinda usalama wa watu wetu na kutoa urahisi kwa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kufika katika maeneo kwa uharaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tumekwenda kule kwa wahanga wa mafuriko, barabara hii ni mbovu na haipitiki kabisa. Sehemu ambayo tulitakiwa tutumie muda wa saa moja, tumetumia karibu masaa manne kutokana na ubovu wa barabara. Ninyi mnafahamu hali halisi iliyopo katika maeneo yetu kule mipakani, kwa hiyo, barabara hii ina umuhimu mkubwa sana wa kututengenezea kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye barabara ya uchumi ambayo inatoka Mtwara Mjini kuelekea Msimbati, ambako kuna mitambo na visima vya gesi kule. Ninaongea kwa masikitiko makubwa sana, ni aibu, sehemu ambayo tumewekeza uwekezaji mkubwa, barabara ni mbovu; sehemu ambayo kuna mitambo kule ya gesi, kuna visima vya gesi, barabara ni mbovu. Ninaiomba sana Serikali mwiangalie barabara hii kwa macho mawili na kwa umuhimu wake,

mtujengee kwa kiwango cha lami kwa uharaka kutokana na umuhimu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kuzungumzia kwenye suala la maji. Katika majimbo sugu yenye changamoto ya maji, ni Jimbo la Mtwara Vijijini. Bajeti iliyopita nilizungumza hapa katika maeneo ambayo bado hayajafikiwa vizuri kwenye huduma hii muhimu ya maji safi na salama, ni Jimbo langu la Mtwara Vijiji. Kuna maeneo mengi yana changamoto ya maji. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali, na Mheshimiwa Aweso nimekufuata mara nyingi, nakuomba kaka yangu utuone kwa macho mawili katika Jimbo langu Mtwara Vijijini, bado tuna changamoto kubwa ya maji katika maeneo mengi. Maeneo mengine toka tumepata uhuru wa nchi hii, hawajawahi kabisa kufuruhia huduma hii muhimu ya maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna mradi wa maji wa Mto Ruvuma. Kuna bomba limepita katika maeneo yale, na kuna wananchi walishafanyiwa uthamini tokea mwaka 2015, takribani miaka nane, mpaka leo hii wananchi wale hawajapewa fidia karibu vijiji 25; Kijiji cha Mayembe, Mitambo, Madimba, Kitaya, Kihamba, Kivava, Mahurunga, Kitunguli, Kihimika, Litembe mpaka Mtwara Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo haya wananchi wanashindwa kuendeleza maeneo yao kutokana na kutolipwa fidia. Kwa hiyo, naiomba Serikali iangalie maeneo haya, wananchi wanashindwa kufanya maendeleo kutokana na kulipwa fidia yao. Kama wameshindwa kuendeleza, Serikali naomba mtueleze ili maeneo haya wananchi waweze kufanya shughuli zao za maendeleo, waweze kufanya shughuli zao za kilimo, waweze kufanya shughuli zao za ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia suala la afya. Tunaishukuru sana Serikali kwa kutujengea majengo mengi

katika vijiji vyetu; zahanati na vituo vya afya, lakini kuna uhaba mkubwa wa watumishi katika maeneo yetu, hasa katika maeneo ya vijijini. Tunaiomba Serikali watuletee watumishi wa kutosha. Utakuta zahanati nyingi muuguzi yupo mmoja; mgawa dawa ni huyo huyo, mchoma sindano ni huyo huyo, mzalishaji ni huyo huyo. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali iangalie maeneo mengi ya vijijini, kuna uhaba mkubwa sana wa watumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa nitazungumzia kuhusu suala la kilimo. Sisi wananchi wa Mkoa wa Mtwara, kilimo chetu kikubwa ni zao la korosho, uchumi wetu mkubwa ni zao la korosho. Tunaomba msimu wa mwaka huu usiyumbishwe yumbishwe. Tunaiomba sana Serikali watuletee viuatilifu kwa wakati. Pia nilizungumza kwenye bajeti ya mwaka jana 2022, tunaiomba Serikali ifanye takwimu kwa kila mkulima wa korosho kwa ajili ya ugawaji wa viuatilifu ili kuondoa mikanganyiko inayojitokeza mara kwa mara katika ugawaji wa viuatilifu hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Shamshia Mtamba. Tunaendelea Mheshimiwa Ng'wasi Kamani, halafu Mheshimiwa Festo Sanga na Mheshimiwa Jacqueline Msongozi wajiandae.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana nami kupata nafasi leo ya kuchangia katika hotuba hii ya Waziri Mkuu. Nina machache tu ya kusema. Siku ya leo nitazungumzia mambo mawili, na muda ukiruhusu nitakwenda kwenye la tatu. Nitazungumzia suala la uzalendo kwa vijana, suala la maadili kwenye nchi yetu na muda ukiruhusu nitazungumzia utaratibu wa ujazaji wa nafasi za ajira zinazotangazwa Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala zima la uzalendo kwa vijana; kwanza kabisa, naomba kwa niaba ya vijana wote Watanzania, tufikishe salamu zetu za pongezi na shukrani za kutosha kabisa kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kwa sababu tangu ameingia madarakani Mheshimiwa Rais amekuwa nasi bega kwa bega, changamoto zetu amezivaa, amekuwa anazi-*address* kila siku na kuwasisitizia watendaji wake pia kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano. Tumekuwa na malalamiko ya muda mrefu sana sisi vijana kwamba tukianza biashara tunakuwa na msururu wa taratibu nyingi na urasimu mkubwa sana kabla ya kuja kusimama kwenye biashara zetu. Mheshimiwa Rais ameliona hili, na siku za hivi karibuni kupitia Waziri Viwanda na Biashara, ameondoa malipo ya kodi kwa kipindi cha mwaka mmoja kwa kijana aneyeanza biashara. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi hizi za Mheshimiwa Rais, tangu alipoingia katika kiti chake, kahakikisha anatulea sisi vijana na kutuaminisha kwamba tunaye mtu anayetuunga mkono katika juhudi zetu za kuchangia katika kujenga Taifa letu. Hata hivyo, bado tuna changamoto moja kubwa sana ambayo inatishia moyo wa uzalendo kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha pale ambapo vijana tunakuwa tunajifunga mikanda, shime kujenga nchi yetu pamoja na mazingira na changamoto zote tunazokutana nazo, halafu tunaona kuna baadhi ya watendaji ambao sisi vijana tumewaamini kupitia nafasi mbalimbali Serikalini, kufanya kazi yao kutuletea maendeleo kwa kodi tunazolipa, wanaiba pesa hizo na badala yake tunashindwa kupata maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata neno la Mungu limesema kwamba “toa boriti katika jicho lako, ndipo utoe boriti katika jicho la mwingine.” Tunapataje nguvu au Serikali itapata wapi *legality* ya kumwambia kijana uwe mzalendo, ukipewa nafasi fanya kazi na ujenge nchi yako ilhali kuna baadhi wamepewa nafasi hizo na wanayoyafanya tunayaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii vijana wanaohitimu tunawalaumu, kwamba kijana anahitimu, anataka ndani ya mwaka mmoja ama miwili aendeshe *Range,* ajenge ghorofa. Tunawalaumu, lakini haya hatujayatoa *from no where*, tunawaona. Kuna vijana wadogo, leo hii unamwona kapata kazi *TRA*, kapata kazi bandarini, mwaka mmoja ana ghorofa. Unaniambiaje mimi nisifanye yale kama anayoyafanya yule? Tunaua Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana sio Taifa la kesho tu, ni Taifa la leo. Kama tunataka vijana waendelee kuwa wazalendo, waendelee kuijenga nchi hii, tujenge nchi ambayo miaka 100, miaka 200 itasimama ikiwa na uchumi imara, tunahitaji mabadiliko makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishauri katika Bunge lililopita kwamba Serikali ituletee mabadiliko ya sheria ili tukuze uwajibikaji katika utumishi wa umma. Hawa wanaofanya mambo haya, tuwawajibishe. Leo hii kijana akiona kwamba mwizi au anayefanya ubadhilifu amewajibishwa, hata yeye kesho anazidi kuona kwamba Taifa linamlinda, Taifa linam-*support*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wahenga walisema, “mtoto wa mhunzi asiposana, hufukuta.” Maana yake ni nini? Maji hufuata mkondo. Sasa kama Serikali inatuonesha mkondo huu, kesho vijana watafuata mkondo upi? Tunaomba, tunaomba, tunaomba; haya yanayoendelea kule nje hayana afya kwa vijana, hayana afya kwa Taifa, hayana

afya kwa kesho yetu iliyo salama. Tunahitaji mabadiliko ya sheria na tunahitaji hatua za haraka zichukuliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala zima la maadili, wamezungumza Wabunge wenzangu hapa waliotangulia. Kuna kitu ambacho kinaendelea kwenye jamii yetu kinatushtua. Kimsingi kinatishia hata kesho ya nchi yetu na kinahusu bara zima kwa ujumla. Mapenzi ya jinsia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunajua kwamba kujihusisha na mambo haya, moja ya *effect* yake kubwa zaidi ni kukosekana kwa uendelevu wa vizazi. Hakuna kizazi kinachoweza kuendelea kwa mapenzi kati ya mwanaume na mwanaume au mwanamke na mwanamke. Mimi nitawarudisha nyuma kwenye historia. Karne ya 19, moja ya vitu vilivyoisaidia *Europe* ku-*develop* kwa kasi ilikuwa ni kitu kinachoitwa *demographic revolution*. Ongezeko kubwa la idadi ya watu, lakini ripoti za *IMF* na *World Bank* zinatuonesha nchi ya China imefika hapa ilipofika sababu kuu, ikiwa ni wingi wa watu walionao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii mambo haya yanaletwa, siyo kwamba wenzetu hawaoni juhudi za ukombozi ambao Bara la Afrika linajitahidi kufanya ili kufika mbele na kujiondoa katika lindi la umasikini tulionao, ni wazi. Pia ripoti ya *World Bank* inaonesha, *Africa is the youngest continent*. Maana yake ni nini? Afrika ndiyo bara pekee lenye nguvu kazi kubwa zaidi kuliko mabara mengine yote duniani. Afrika ndiyo ina vijana wadogo zaidi kuliko mabara mengine huko duniani. Maana yake miaka 10, 20, 30 ijayo Afrika leo haitakuwa hapa ilipo. Tuna vijana wenye nguvu na wenye uweledi wa kufanya kazi. Uchumi wetu utakuwa umeimarika, umeimarika, umeimarika zaidi. Kimsingi hicho ni tishio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi wamechangia kwa maana ya kwamba hii ni tishio tu kwa maadili yetu, lakini mimi naenda mbele nasema, hili ni tishio dhidi ya ukombozi wa kiuchumi ambao Afrika na Tanzania inajaribu kufanya. Ni ukweli usiopingika kwamba sisi Watanzania zaidi ya asilimia 80 tunategemea kufanya kazi za ngumu ili kujipatia kipato, lakini tafiti zinaonesha kwamba kibiolojia, watu wanaojihusisha na mambo hayo, hasa wanaume wanapungukiwa na nguvu ya kufanya kazi kwa zaidi ya asilimia 30. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipoziba ufa, tutajenga ukuta. Miaka 20 ijayo tutapata wapi vijana wa kufanya kazi za nguvu za nchi hii, kuijenga nchi hii? Tunahitaji hatua za haraka zichukuliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashangaa kwa sababu Mheshimiwa Rais amezungumza, Mheshimiwa Makamu wa Rais amezungumza, Mheshimiwa Waziri Mkuu amezungumza, Wabunge mbalimbali wamezungumza, viongozi wetu wa dini wamezungumza, Watanzania kila sehemu wanazungumza, kwa nini hatua hazichukuliwi? Sheria ipo wazi, hiki kitu ni *criminal offence*. Mheshimiwa Saashisha alisoma hapa sheria ndani ya Bunge hili, kwamba ni miaka 30 ukionekana umefanya mambo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii siyo kesi ya nani atamfunga paka kengele? Kwa nini? Kwa sababu watu hawa wanajinasibu, na wako wazi hata kwenye mitandao ya kijamii. Kwa nini hatuoni hatua zikichukuliwa? Tunahitaji kuona hatua za haraka zinachukuliwa kunusuru vizazi vyetu, kunusuru nchi yetu lakini kunusuru uchumi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, lakini siyo kwa umuhimu mdogo, nitaongelea suala la utaratibu wa ujazaji wa nafasi za ajira kwenye nchi yetu. Tunashukuru sana tangu Mheshimiwa Rais ameingia madarakani, ametangaza nafasi

nyingi sana za ajira na vijana wengi wamejipatia ajira. Kwenye hilo tunashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo tuna walakini kidogo katika utaratibu unaotumiaka kujaza nafasi hizi. Kwanza kabisa, tukiangalia *ratio ya applicants* kwa nafasi zile ambazo zinazozatangazwa, inaonesha namna gani tuna tatizo kubwa sana la ajira kwenye nchi yetu. Tunaipongeza Wizara kwa sababu tulitoa maoni nayo ikapokea, ikaanzisha vituo mbalimbali ambapo watu sasa wanaweza kwenda kufanya *interview* tofauti na zamani ambapo lazima waje sehemu moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto inayokuja ni kwamba, unakuta zinahitajika nafasi 100, lakini idadi ya watu wanaoitwa kwenye *interview* unakuta *ratio* yake ni hata *50:1*. Unajiuliza, kama hawa watu kwenye ku-*apply* walitoa vyeti vyao, wali-*submit* vielelezo vyote vilivyotakiwa. Kwa nini waitwe watu wengi kiasi hiki kwa nafasi chache ilhali tunajua fika kwamba hawa vijana wana changamoto huko waliko? Wengi hata akiitwa hata kwenye kufanya *interview* wanakwambia hata nauli sina, sijui nitafikia wapi? Sijui nitakula nini kwa hizi siku ninazoenda kufanya *interview?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta nafasi moja wanaigombania vijana 50. Kuna haja ya kufanya hayo? Pili, vijana hawa wakifika kwenye *interview,* kumekuwa na *tendency;* unaambiwa *interview* inaanza saa 3.00, lakini vijana watakaa pale mpaka saa 8.00 hamna *interview* iliyofanyika. Hawajui wala hawajapewa utaratibu wowote. Kwa nini kama Serikali inakuwa imejiaandaa kufanya *interview* na kusaili vijana hawa, kwa nini wasijipange, utaratibu ufanyike, vijana wafanye *interview* warudi majumbani? Inakuwa ni kama hawajajipanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, tumeambiwa kwamba mnafanya *interview,* kuna baadhi yenu

wanawekwa kwenye kanzidata ili nafasi nyingine zikija, wasifanye tena usaili wachukuliwe kwenye kanzidata. Hilo ni jambo zuri, lakini lazima tuwe na *transparency*. Vijana watajiuliza kwamba tuna uhakika gani kwamba hawa waliowekwa sasa hivi ndiyo wale waliokuwa kwenye kanzidata? Tuna uhakika gani kwamba hawa hawajachukuliwa kutoka mifukoni mwa watu wakawekwa kwenye nafasi zile? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali. Naomba, kama kuna kanzidata, iwe wazi, kila mtu ajue kwamba mimi kwenye kanzidata ni Na. 3, zikitangazwa nafasi 10 maana yake na mimi nimo; zikitangazwa nafasi 20 nami nimo, au simo nasubiri kipindi kijacho, ili kuondoa sintofahamau kwa vijana kwenye suala hili la ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ng'wasi Kamani. Nilimtaja Mheshimiwa Festo Sanga, halafu Mheshimiwa Jacqueline Msongozi na Mheshimiwa Constantine Kanyasu wajiandae.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Jambo la kwanza naomba niunge mkono hoja iliyoko mezani. Naunga mkono hoja kwa sababu ripoti inaonyesha mambo mengi yamefanyika ni mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa na mambo machache sana ya kuzungumza. Jambo la kwanza ni kumpongeza Mheshimiwa Rais. Kwa niaba ya Wananchi wa Makete tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi ambazo anazifanya na hata kwa hatua ambazo anazichukua dhidi ya watu ambao wanaonyesha kabisa wakimvuta shati na kumrudisha nyuma hasa hasa haya

mambo ambayo yamekuwa yakijitokeza kwenye taifa letu. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi anayofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwa miradi ambayo anaileta kwenye Jimbo langu la Makete. Sasa hivi tuna mradi wa Barabara ya kutoka Mbeya kuelekea Makete, barabara ya kiwango cha lami na mkandarasi alishasaini tayari barabara ile lakini niombe tu kwamba Serikali hii mikataba ambayo imeshasainiwa Serikali iweze kutoa *advance payment* kwa wakandarasi ili ziweze kujengwa kwa kasi kwa sababu barabara hii hadi sasa mkandarasi bado anasua sua kutokana na kwamba hajalipwa *advance payment* ili aweze kuanza kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali iweze kushughulikia hilo jambo ili barabara ile iweze kujengwa kwa sababu ni barabara ya kiuchumi na ni barabara ya kimkakati na ni barabara ambayo kwa Jimbo la Makete wananchi wangu wanaisubiri kwa hamu sana ili iweze kutekelezeka na shughuli za kiuchumi ziweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nataka kuzungumzia nataka kuzungumzia kwenye suala moja linalohusu Kariakoo. Naizungumzia Kariakoo kwa sababu karibia 50% ya wafanyabiashara wa Kariakoo ni Wananchi wa Wilaya ya Makete na ni wananchi ambao wanafanya kazi pale lakini pia Kariakoo ni moja kati ya kitovu cha uchumi cha Taifa letu. Kwa hiyo, nazungumzia Kariakoo kwa mantiki hii hapa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimeiita hii; *how TRA is trying to kill Kariakoo,* yaani nimejaribu kuielezea jinsi gani *TRA* wanajaribu kuimeza na kuiua Kariakoo sehemu ambapo tunategemea kama Taifa tunapata mapato yetu mengi kwenye ukusanyaji wa mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nina mambo matatu makubwa ya kuizungumzia Kariakoo; jambo la kwanza, Kariakoo ilikuwa inafanya vizuri sana kwenye soko la vitenge. Katika ukanda wa Afrika Mashariki Kariakoo ilikuwa inaongoza kwenye soko la kitenge lakini leo ninavyozungumza soko la kitenge Kariakoo limekufa. Kwa nini limekufa? Limekufa kwa sababu ilipitishwa Sheria hapa ya Ongezeko ya mita moja ya kitenge kutoka dola 0.4 kwenda 0.8 kwa maana kwamba 100% ya ongezeko kwa minajili ya kwamba tunalinda viwanda vya ndani lakini nikuelezee tu leo hii ukienda Zambia, ukienda Congo, ukienda Malawi ndiko vitenge vinakouzwa zaidi kuliko Dar es Salaam – Kariakoo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wafanyabiashara wa Kariakoo wengi wamepoteza vitenge, wamepoteza mitaji tumeua Soko la Kariakoo. Kwa hiyo, *TRA* kwa kulinda viwanda vya ndani ambavyo pia havitoshelezi soko wameweza kuizamisha Kariakoo kwenye soko la vitenge leo hii mapato kupitia vitenge hatuwezi kuvipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la tatu, Kariakoo inakufa, kwa nini inakufa? Ukienda leo hii kuna suala la wafanyabiashara wa kigeni. Wafanyabiashara wa kigeni wananunua sana mizigo kwenye Soko la Kariakoo, mizigo yao mingi ni *whole sale*. Wakinunua *TRA* wamekaa kuvizia, wanavizia kwa ajili ya kuwakamata, wakiwakamata wanasema mzigo wako ulionekana ni mkubwa risiti ni ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali ni vyema wakatafuta utaratibu mwema jinsi ya ku-*deal* na suala la ukusanyaji wa mapato kwenye Kariakoo. Wafanyabiashara wengi wamepungua wa kigeni wanakimbia, wako ndani, bidhaa zao zimeshikwa wanashindwa tena kurudi kufanya kazi kwenye Soko la Kariakoo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti niiombe *TRA* na Mheshimiwa Waziri Mkuu anatusikia, ni vyema kuweka kikosi kazi maalum

cha kwanza kuangalia jinsi gani wafanyabiashara wanavyoweza kufanya kazi hasa hasa hawa wafanyabiashara wanaotoka nje kuja kununua mizigo kwenye Soko letu la Kariakoo ili Kariakoo iendelee kubaki salama iweze kuendelea kuilisha Taifa letu tubaki kwa na *brand* kwenye nchi yetu. Tofauti na hapo kuendelea kuvizia wafanyabiashara wa kigeni, wamenunua mizigo uwakamate tunaendelea kuiumiza taifa, tunaendelea kuiumiza Kariakoo ambacho sisi kwetu ni kitovu cha uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili niombe sana Serikali ilichukue katika uzito mpana sana. Hatuyasemi haya kwamba labda tunalengo baya na *TRA,* tunayasema haya tuna malengo mazuri. Ng'ombe yoyote unayemlisha lazima akutolee maziwa vizuri. Sasa hawa wanakamua tu, wanakamua tu lakini hawatengenezi mazingira mazuri ya kuiona Kariakoo inazidi kuwa salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine juzi *TRA* wametoa waraka kuhusu *consolidation.* Utaratibu wa nyuma wote ulikuwa unaonyesha nina bidhaa naenda kununua China kwa mfano. Naungana na mwenzangu labda wawili, watatu tunaagiza mzigo kwenye *container* moja tunalileta Kariakoo. Watu wa *cargo consolidation* wanaweza kulishughulikia *container* na mizigo nikapata. Juzi umetoka waraka wa kwamba wafanyabiashara wote mnaoagiza mizigo China ni lazima mizigo yenu ikifika hapa kila mtu alipie kwa mzigo wake pale bandarini. Kwa maana ya kwamba mizigo ikifika inamwagwa, mfanyabiashara analipia pale mzigo wake ndiyo atoe aende nao kwenye soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu hiki kinaenda kuimaliza Kariakoo kabisa. Ninalisema leo hapa na kesho kutwa yatakuja kutokea. Nimeagiza *piece* 500 za mzigo, siweze kwenda tena bandarini nikaanze kusema jamani mzigo wangu ni huu hapa naomba nilipie. Tuna *manpower* gani

bandari yetu ya kwamba imwage *container* mfanyabiashara aanze kuchagua mzigo pale ili aweze kulipia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hizi zote ni *bureaucracy* za kutengeneza za kuiba, *bureaucracy* za kupoteza mizigo ya wateja, *bureaucracy* ya kuhakikisha wafanyabiashara hawakui, *bureaucracy* ya kuhakikisha Kariakoo inakufa, *bureaucracy* ya kuhakikisha kwamba watu wanajilimbikizia mali wanatafuta kupitia Soko la Kariakoo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana Wizara iangalie hili jambo. Ni jambo ambalo linaenda kuua wafanyabiashara kwa sababu hatuna *manpower* ya kutosha ya bandari yetu kumwaga mzigo chini ili kila mfanyabiashara aanze kulipia mzigo wake aliouchukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ruhusuni *cargo,* hizi *cargo* hawa Watanzania wenzetu wamefungua *cargo* ziweze ku-*facilitate* hilo jambo. Kutengeneza hizi *bureaucracy* ni kuendelea kulifanya Taifa letu liendelee kudidimia. Kwa hiyo, haya mambo matatu *if you don't take care* kwenye haya tunaenda kuizamisha Kariakoo. *Kariakoo is our brand,* Kariakoo ni chanzo chetu, Kariakoo ni eneo letu, *TRA* inafanya kazi vizuri ya kukusanya mapato lakini watendaji wao wa chini wanaenda kuizamisha Kariakoo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu lingine ni suala la maadili na malezi. Kama kuna mambo makubwa mawili kwenye nchi yanayotikisa kwa wakati huu ni suala la maadili na mmomonyoko wa malezi ya watoto wetu. Sisi ni Bunge hapa leo tunazungumza mambo mengi sana ya msingi kwa ajili ya Taifa letu lakini nakuhakikishia miaka 30 ijayo, miaka 40 ijayo kama suala la mapenzi ya jinsia moja hatutaipigia kelele, sisi Wabunge hapa miaka 30 ijayo, miaka 50 ijayo, tunaweza kuja kuwa na viongozi ambao wako kwenye sekta hiyo ya mashoga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo…

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa.

**T A A R I F A**

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mchangiaji wakati anaifikiria miaka 30 ijayo na siye Wabunge tupo, si tukubaliane tu hapa kwamba tukipima mtu akaonekana anafanya mambo yale anyongwe tumalize kabisa? Tutakuwa tumekomesha kuliko haya ya kusubiri miaka 30. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anaongea jambo la msingi sana na tuna sheria zetu kwa maana ya kwamba kuna sheria zinazosema ni miaka 30 au kifungo cha maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukijidai kama hapa sisi ni vipofu hatuoni kinachoendelea kwamba kwa sababu ni Mbunge ninauwezo wa kum-*protect* mtoto wangu akawa anaishi mazingira mazuri anasoma shule nzuri. *I am telling you,* ubunge wetu ni sisi ni kwa sababu ya wananchi walioko kule mtaani ambapo haya wanayashuhudia yanatokea na sisi tuko kimya. Ni vyema kama nchi tukaanza kuchukua hatua *immediately.* Huu siyo utamaduni wa Kiafrika hata Biblia inakataa, hata *Qurani* inakataa. Miaka 30 ijayo nusu ya Bunge inaweza ikawa mashoga wamekaa hatuwezi kuwa na Taifa kama hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunajenga *SGR,* tunajenga hizo *airport,* Mheshimiwa Rais ana-*invest* fedha nyingi kwenye miradi. Tunakuja ku-*invest* kwa ajili ya kizazi kipi? Leo nina

watoto wangu. Watoto wangu nisipowalinda, watakuja kudondokea kwenye huu mtego.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana lazima tuanze *ultimatum* kama nchi ya kwamba Taifa letu kwenye suala la malezi ya watoto limebadilika. Lazima tuanze mfumo wa tofauti kuhakikisha kwamba tuna-*protect* kizazi chetu. Tofauti na hapo kwa sababu ya misaada, kwa sababu tunapewa fedha, kwa sababu ya nini tuwe tayari kuachia damu zetu ziingie kwenye Sodoma na Gomora. Hiyo ni kitu ambacho hakiweze kuruhusiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama makanisa hayatasimama, kama Bunge halitasimama, kama misikiti haitasimama kuna siku misikiti na makanisa na Bunge vitaongozwa na watu ambao wako kwenye upande huo. Niombe tuchukue hatua kali dhidi ya watu hawa. Nimshukuru sana Mkuu wa Wilaya mmoja amefuta taasisi mojawapo. Juzi kuna kesi imetokea kule Mtwara mtu amefungwa. Tuanze Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa, Wakurugenzi kila mmoja kwa nafasi yake alipo tutakuja kupata viongozi wa Jeshi, niliona ile takwimu imetoka jeshini wamepima waliokwenda jeshini wamekuta wengine wako kwenye upande huo. Tutakuja kupata jambo gani? Lazima tushughulike na jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe kama Mbunge kwa niaba ya Wananchi wa Makete, sisi Wanamakete suala la ushoga tunasema *no,* suala la mapenzi ya jinsia moja tunasema *no,* Biblia na *Quran* havijatutuma huko, msingi wetu ni kuhakikisha kwamba tunazaliana. Na mnajua kwamba vita yote hii ni kwa sababu Afrika tunazidi kuwa wengi, Wazungu wanajaribu ku-*impose* taasisi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuamini kwamba adui ameonyesha mlango aliopo na sisi tuonyeshe silaha

tulizonazo kuukataa ushoga. Msaada wowote wenye *element* hizo Serikali tunaomba isiwe sehemu kwa sababu hautakuwa na baraka katika Taifa letu. Hatuwezi kuruhusu kizazi chetu kikapotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo niende kuunga mkono hoja, niishukuru Serikali kwa ajili ya Jimbo la Makete na miradi ya maendeleo inayokuja. Niseme, tunawakati wa kuilinda Kariakoo lakini pia maadili na malezi kwa watoto wetu lazima tusimamie. Sisi kama Wabunge lazima tuonyeshe upande wetu ni upi nalitetee Taifa letu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Festo Sanga. Nilimtaja Mheshimiwa Jacqueline Msongozi; Mheshimiwa Constantine Kanyasu, Mheshimiwa Abubakari Asenga ajiandae.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuipa fursa hii. Kwanza kabisa naomba niende kwenye suala la mifugo. Wakati ninakwenda kuchangia Bajeti hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania naomba moja kwa moja nianze na Wizara ya Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia suala la ufugaji wa samaki kwa maana ya vizimba. Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan ametenga fedha shilingi bilioni 20 kwa ajili ya uwezeshaji kwenye eneo hilo la suala la ufugaji wa samaki kwenye vizimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tarehe 5 niliuliza swali linalohusisha ufugaji wa samaki hao na ikaonekana kwamba fedha hii imetengewa Shilingi bilioni hizo nilizozitaja na kwamba inakwenda kupelekwa kwenye Ziwa Victoria. Swali langu la pili la nyongeza nilikuwa nimeiomba Serikali kwamba

ipeleke gawio sawa na maziwa mengine. Isiende shilingi bilioni 20 hii yote katika Ziwa Victoria bali iende na kwenye maziwa mengine ikiwemo Tanganyika, Ziwa Nyasa na Ziwa Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kumshukuru sana Waziri wa Mifugo Mheshimiwa Abdallah Ulega baada ya swali langu aliniita ofisini kwake na akaniambia ameshazungumza na timu yake sasa tunapata gawio, Ziwa Nyasa tunapata gawio la shilingi bilioni tatu ambayo itapelekwa kwenye suala la ufugaji wa vizimba katika Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala jingine naomba niende kwenye suala la viwanda na biashara. Kwenye suala la viwanda na biashara naomba niende moja kwa moja katika Kata ya Mwengemshindo katika Manispaa ya Songea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *EPZ* walichukua maeneo ya Kata hiyo ya Mwengemshindo ni miaka 15 sasa tangu maeneo hayo yamechukuliwa na wananchi bado wanalia hawajalipwa fidia, hawaelewi hatma ya maisha yao. Wanashindwa kuendeleza aidha kuongeza kama ujenzi wa nyumba au kufanya shughuli nyingine zozote zile za maendeleo. Fedha hii Shilingi bilioni 3.9 leo hii nimesimama hapa katika Bunge lako tukufu ninataka Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapokuja ku-*windup* hapa aniambie ni lini Serikali itapeleka fedha hii shilingi bilioni 3.9 kwa wananchi wa Kata ya Mwengemshindo katika Manispaa ya Songea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niende kwenye miundombinu, naomba nizungumzie barabara ya kilometa 28 ambayo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais. Barabara hii inatoka Mbinga mjini inapita katika Kata ya Ruwaita, inapita Kindimba, Mahenge, Litembo ambayo barabara hii ni barabara ya kimkakati. Mheshimiwa Rais alikuja pale na akatoa ahadi, Rais wa Awamu ya Sita akiwa Makamu wa

Rais alitoa ahadi pale kwamba barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami. Sasa ni wakati muafaka, ninaomba fedha hii itengwe ili barabara hii iweze kujengwa kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika naomba niende kwenye barabara ya kilometa 35 ambayo inatoka Kigonsera kwenda Matili yenye urefu kilometa 35 ambayo inapita Kitumbalomo, Lukalasi. Matili ni kata ambayo ndiyo inabeba uzalishaji mkubwa wa mazao ya nafaka katika Mkoa wetu wa Ruvuma. Kwa hiyo, ninaomba barabara hii sasa ni wakati muafaka fedha ipelekwe ili ianze kujengwa kwa kiwango cha lami na Mheshimiwa Benaya Kapinga amekuwa akizungumzia sana barabara hii. Naomba sasa kwa heshima hiyo ya Mheshimiwa Kapinga na mimi Jacqueline Ngonyani Msongozi, barabara hii sasa iweze kutengewa fedha na iweze kujengwa kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye Barabara ya Likulufusi – Mkenda yenye urefu wa kilometa 124. Hii ni barabara ambayo inaunganisha Nchi yetu ya Tanzania na Nchi ya Mozambique na barabara hii nimekuwa nikiimba kila nikiamka kwenye Bajeti ya Serikali ya mwaka husika lazima niisemee barabara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama ambaye ndiye inapita kwenye jimbo lake amekuwa akiizungumzia sana hii barabara na sasa mimi pamoja na yeye kwa heshima hiyo tunaomba barabara hii ianze kujengwa haraka sana kwa sababu barabara hii ni barabara ambayo itaunganisha hizi nchi mbili. Manufaa ya barabara hii ni kwamba itasaidia kuchochea uchumi katika Nchi yetu ya Tanzania, itasaidia kuimarisha soko ambalo limjengwa kwenye Mpaka wa Tanzania na Mozambique pale Mkenda. Tuna soko ambalo limejengwa mpaka sasa fedha ya Serikali

imetumika lakini bado halitumiki kwa sababu miundombinu ya barabara pande zote mbili haijakaa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii itaongeza biashara kwenye eneo hilo la mpaka. Itaongeza mzunguko wa fedha katika Manispaa ya Songea na Jimbo la Songea Vijijini, Jimbo la Peramiho kama nilivyosema. Pia wananchi wa kutoka Mozambique watatumia uwanja ule wa ndege wa Songea ili kuweza kusafiri kwenda kwenye maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kabisa barabara hii itatengewa fedha kwa maana ya heshima hiyo lakini pia mumpe heshima *Chief Whip* wetu ambaye amekuwa akifanya kazi hapo wakati mwingine anakosa fursa ya kusema kama ninavyosema basi mpeni hiyo fursa ya hiyo barabara ni barabara muhimu sana ili tuweze kufikia malengo tunayokusudia kama nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ukarabati wa shule kongwe. Iko Shule ya Sekondari ya Msindo iliyopo katika Wilaya ya Namtumbo katika Mkoa wa Ruvuma. Hii shule ni kongwe, shule hii imechakaa sana inahitaji ukarabati, halikadhalika katika shule hiyo hiyo kunahitajika *hostel* ya watoto wa kiume. Kimsingi wamekuwa wakilala kwenye jengo ambalo halifai na wala jengo hilo ni kama vile ghala. Kwa hiyo, tunaomba Serikali ifanye jitihada za makusudi ili kuokoa ustawi wa watoto wale mwisho wa siku tunahisi kwamba wanaweza wakapata magonjwa mengine kwa sababu jengo hilo wanalokaa vidirisha ni vidogo sana kwa sababu ni ghala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika sekondari hiyo hiyo kuna hitaji la bwalo la chakula la shule hiyo. Sasa hivi wanapikia kwenye eneo la wazi, kwenye mti nje wanapikia chakula hapo. Kwa hiyo, ninaamini bwalo likishajengwa maana yake hata ustawi wa afya zao wale watoto wetu zitakuwa ni njema. Kwa hiyo, niiombe Serikali ifanye hivyo

haraka sana ili kuokoa hali halisi na mazingira halisi yanayojitokeza kwenye shule hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la afya, Wananchi wa Kata ya Msindo wamejenga jengo la upasuaji katika eneo la jengo ambalo lilianza awali kabla ya kituo cha afya hakijajengwa. Jengo lile wananchi wamejitolea wamefikia kiwango cha kuezeka lakini hawawezi kuendeleza kwa sababu hawana fedha ndiyo wameishia hapo. Tunaomba msaada wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ipelekwe fedha pale ili waweze kwenda kumalizia jengo lile la upasuaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka sasa niendelee kwenye suala hilo hilo la afya. Tarafa ya Mbuji katika Wilaya ya Mbinga, Jimbo la Mbinga Vijijini ni tarafa ambayo inabebwa na Kijiji cha Mpaka, Unyoni, Litembo, Mbuji, Kitulo. Tarafa hii yenye vijiji hivyo vikubwa bado haina kituo cha afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu wewe unafahamu vizuri Mkoa wa Ruvuma, tunaomba sasa upeleke kituo cha afya kikajengwe kwa ajili ya kuokoa maisha ya wananchi ambao wanaizunguka tarafa ile, kwa maana ya kata tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu zahanati. Katika jimbo hilo hilo, wilaya hiyo hiyo ya Mbinga bado kuna tatizo la zahanati, zahanati hakuna. Nilipokuwa nazungumzia kituo cha afya maana yake hata zahanati huko chini hakuna. Kuna uhitaji wa zahanati 38 katika eneo hilo. Mheshimiwa Banaya amekuwa akipiga kelele hapa kila siku anaomba zahanati zijengwe katika maeneo haya. Sasa na mimi kama mama nimesimama hapa katika Bunge lako kulisemea hilo hilo. Nipaze sauti, labda kwa sababu ni mama, ili wananchi hawa waweze kupata fursa ya kujengewa zahanati na nitataja baadhi siwezi kutaja maeneo yote 38;

basi nitataja baadhi itakuwa ni wakilishi kwa maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zahanati hizo zinazotakiwa zijengwe ni katika Kijiji cha Likoho, Lugavi, Njombe, Kizota, Ukata, Lisao, Mzuzu, Mhagawa, Mtaya, Liyombo, Liuhula na nyinginezo. Naomba maeneo haya yatengewe fedha ili zianze kujenga. Safari ni hatua, hata ukitutengea 10 tu itakuwa ni hatua nzuri kwa mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka niliongelee ni suala la mmomonyoko wa maadili…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jacqueline nakuongezea dakika moja tu malizia hilo kwa sababu ni la maadili.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwenye suala la mmomonyoko wa maadili naomba tu niseme kwamba tuna kila sababu sisi kama Wabunge kuhakikisha kwamba tunaleta sheria iwe ya mkazo hapa Bungeni, itengenezwe sheria na sisi tuipitishe kama Bunge ili kuweka utaratibu mzuri ambao utawafanya wale wanaoshughulika na mambo haya waweze kubanwa kwa namna moja au nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kabisa kwa kuwa wewe ulikuwa Makamu Mwenyekiti naomba upendeleo wa dakika moja. Naomba nitumie nafasi hii kuwapongeza sana viongozi wa dini ambao wamejitokeza kuzungumzia suala la mmomonyoko wa maadili katika nchi yetu. Tumeona Shehe Mkuu wa Tanzania amesema, tumeona maandamano kule Arusha, na tumeona viongozi wa madhehebu mbalimbali wanazungumza sana kuhusiana na kukemea kuhusu jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona pia viongozi hawa wa dini wa madhehebu mbalimbali wote ambao wanakemea, lakini nampongeza sana Apostle Buludoza Boniphace Godwin Mwamposa. Yeye kabla ya kuanza ibada kila jumapili anaanza kukemea jambo hilo na wote wafanye hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jacqueline.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri mwenye dhamana…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jacqueline…

**MHE. HACQUELINE N. MSONGOZI:…** wa maendeleo na ustawi wa jamii hatujamsikia sauti yake akikemea jambo hili hatumwelewi tunaomba atoke na aseme kuhusu jambo hili.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri amekusikia. Tunaendelea na nilimtaja Mheshimiwa Constantine Kanyasu, Mheshimiwa Abubakar Asenga, Mheshimiwa Fakharia Shomar na Mheshimiwa Riziki Lulida wajiandae.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi na naomba nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kupata nafasi ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kazi nzuri ambayo inaendelea kufanya. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi ambazo anaendelea kufanya; na wananchi na watu wema wa Jimbo la Geita Mjini wanamkumbuka na wanamshukuru kwa ziara yake ambayo aliifanya mwaka jana na wanaendelea kuitakia mema Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu wa taarifa yake nzuri kwenye bajeti aliyoisoma kwa utekelezaji wa shughuli mbalimbali. Wananchi wa Geita wanaishukuru Serikali kwa kukamilika kwa hospitali yao ya mkoa ambayo imeanza sasa kufanya kazi za nje, kazi za *OPD,* wanaomba tu ikamilike ili iweze kuingia kufanya kazi kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru sana Serikali kwa mradi wa maji wa takribani bilioni 100 ambazo Mheshimiwa Rais alitupatia, na mkandarasi yuko *site* na anafanya kazi. Tunashukuru Serikali kwa fedha za barabara kupitia mradi wa *TACTIC* ambao tayari wakandarasi wametangazwa na wanaanza kufanya kazi. Wananchi wa Geita wanaishukuru sana Serikali kwa fedha za stendi ambazo taratibu za TAMISEMI zinaendelea. Wananchi wa Geita wamenituma nikuombe Mheshimiwa Waziri Mkuu ombi lao la Mji wa Geita kuwa Manispaa, taratibu takriban zote zilikwishakamilika wanakuomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu jambo hili likamilike kwenye mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati wa ziara ya Mheshimiwa Rais kule Kagera akizungumza kuhusu kuhamasisha watu kuwekeza na kulipa kodi alitoa maelekezo kwa *TRA* kuachana na madeni ya zamani na kuhangaika na kuhamasisha watu katika kukusanya kodi kwenye makadirio mapya. Sasa ilikuwa ni ombi langu Mheshimiwa Waziri Mkuu; tunayo shida kidogo pale Geita. Mfanyabiashara anapofanya biashara na Mgodi wa *GGM* anapotoa *invoice* anatoa na risiti, anapotoa risiti inakuwa ina *VAT* lakini walipaji wanaweza kuchukua siku 30 mpaka 90 na wakati mwingine ikitokea *dispute* hawalipwi kabisa. Mfanyabiashara anaingia kwenye deni la *TRA,* inatokea mfanyabiashara anakamatwa wanawekwa ndani wanashtakiwa kwa fedha ambayo hajawahi kukusanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili likienda sambamba na maagizo ya Mheshimiwa Rais; na ndiyo maana kuna madeni mengine yana miaka miwili miaka mitatu, wako wanye kesi mahakamani lakini kimsingi watu hawa hawajawahi kulipwa na *GGM*. Kwa hiyo ni ombi langu agizo hili la Mheshimiwa Rais liweze kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili limezungumzwa hapa suala la BBT. Kwanza naipongeza sana Wizara kwa kuja na huo mkakati wa hayo makundi maalum kwa ajili ya kilimo. Nimeangalia malengi mahususi, kwamba ni kutoa mafunzo, kutoa mitaji, kutoa mashamba na kutafuta masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napata tabu kidogo juu ya *sustainability* ya zoezi hili. Kwanza, tumetenga heka 400, tumeziona pale Dodoma tunaanza. Natamani kujua kwenye mpango kila mwaka tutatenga shilingi ngapi ambazo zitakuwa zimetengwa kwa zoezi hili kwa nchi nzima? tunataka kuona katika halmashauri zote pana mashamba; kama alivyosema mchangiaji mwenzangu kutoka Itigi. Kwamba tunakuwa na mfumo ambao tutapata hao vijana katika halmashauri zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kinachofanyika ni *collaboration ambayoo* nina uhakika *sustainability* haiwezi kudumu kwa sababu tumekusanya watu waliokuwa wanatafuta ajira, tukawapa kazi lakini wamevutiwa wakiamini kwamba Serikali itaendelea kutoa pesa kwenye zoezi hili. Pale ambapo mrija huu wa Serikali utakapokatika hawa watu watarudi kwenye vijiji vyao. Nimeangalia kwenye orodha nzima watu walioko kwenye halmashauri yangu ni watatu, kule kwangu mashamba haya yako wapi? Kule kwangu mkakati wa kuja ukoje na mkakati wao umepangwa kudumu kwa muda gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe mfano; zimeandaliwa takribani heka 47,000 lakini tatizo la ajira lipo

leo, liko mwakani na liko mwaka unaofata. Kwa nini mashamba haya yasingebaki kuwa ya Serikali tukawa na vijana wanaofundishwa labda kwa *program* maalum kwa miaka mitatu, halafu wana-*graduate* wanaondoka wanakuja wengine kwenye kila halmashauri? Sasa hao uliowapa hizi ya miaka 60 au 90; kwanza sasa hivi wana miaka 30, sasa baada ya miaka 30 watakuwa wazee kuliko karibu watu wote tulioko humu ndani, halafu maeneo ya mashamba ya kuwapa vijana wengine itakuwa hayapo. Huo mpango uliopo wa kuwapa *lease* ya kudumu unawapa na hati halafu baadaye watakuwa na miaka 100 itakuwa shamba moja linamilikiwa na wajukuu 200 na hao wajukuu 200 wametoka Tanzania nzima kwa sababu bahati mbaya tunawachanganya kutoka mikoa yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni maoni yangu kwamba jambo hili ni zuri lakini liandaliwe katika mfumo ambapo litapelekwa kwenye kila halmashauri na halmashauri zile zitumiwe kama mashamba darasa lakini kuwe na mpango endelevu. Naitazama hii kama tulipoanza na ile kilimo kwanza ikaja *big result*. Vilikuja na presha sana halafu baadaye ikapita kwa sababu hatukuangalia *sustainability*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifikiri jambo hili ni la msingi sana na liangaliwe vizuri. Kwenye ajira; ukiingia kwenye mfumo wa usajili wa ajira.com ukijaza zile *credential* zako zile za kwamba wewe una *bachelor,* ukirudi siku nyingine na umesema *degree* nyingine ule mfumo hakukubalii. Ukiwa umesoma diploma ule mfumo hakukubalii. Kwa hiyo siku ukijaza ule mfumo kwa mara ya kwanza ule mfumo kila unapotaka kuingia kurekebisha zile taarifa ulizonazo wewe mfumo unakataa. Vijana wengi kwenye soko la ajira ni *mult-professional.* Wanachokifanya, akisoma *procurement,* akasoma ualimu, akasoma *project management* akakosa anaamua kusoma *profession* nyingi. Sasa, ukishaingia mara moja ukajisajili ukirudi mara ya pili mfumo unakataa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa hiyo ombi langu ni kwamba mfumo huu uruhusu mtu kuingiza *credentials* zake hata kama ziko saba; kama amesoma *certificate,* diploma au amesoma digrii tatu aweze kuingia mle ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu *VETA*. Pale Geita Mjini tumejenga *VETA,* naishukuru sana Serikali. Mradi huu ulianza mwaka 2017/2018, leo ni 2023 Mheshimiwa Waziri Mkuu *VETA* haijakamilika. Majengo yapo, nyasi zimejaa na hakuna mwanafunzi. Tulio-*target* mwaka 2018 alipokuwa anamaliza *form four,* darasa la saba; sasa mwingine amemaliza chuo kuu, na kama yuko uraiani amekwishakata tamaa. Hivi mpango gani huu wa Serikali ambao hauna *timeframe?* Yaani mnataka tu kujenga tu ilimradi tu mnajenga haijulikani itafunguliwa lini, haijulikani vifaa vitakwenda lini, haijulikani *training* itaanza lini; ilimradi tuna taarifa tumejenga *VETA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali; tulikuwa tunajenga mwanzo kwa mkopo wa *African Development Bank* hela ikarudi, tukachukua hela za Uviko tukapeleka fine, tumebadilisha *design* na mambo mengine. Naomba bajeti hii ije na bajeti ya vifaa ili chuo kile kianze. Kuna vijana wengi sana pale ambao wanatafuta kazi, wanakosa kazi kwenye migodi mbalimbali kwa sababu tuliazimia kuwa na *VETA* tuweze kufundisha zile *skills* ambazo zinatakiwa na mgodi pale na migodi mingine inayozunguka maeneo yale. Sasa leo mwaka wa sita tunazungumzia chuo ambacho hakikamiliki. Naomba sana jambo hili liweze kukamilika, lakini isiwe tu kukamilika iweze kukamilika kwa *design* iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la nne; juzi nilikuwepo kwenye uzinduzi wa upandaji miti ambao umeratibiwa na watu wa *STAMICO,* nawapongeza sana. Siku ile pia walikuwa wana-*advocate* makaa yao ya mawe ya *Rafiki Briquettes*. Kwanza napongeza sana juhudi hizo za watu wa *COSTECH* ambazo zimeendelea, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, shida yangu ni moja *Rafiki Briquettes* ni inatokana na mawe ambayo ni Wizara ya Nishati, watu wa *STAMICO* wanayo; lakini wanafanya kazi hiyo kwa ajili ya kusaidia kuongeza nishati, watu wa nishati wamo, wanasaidia kupunguza ukataji miti; watu wa misitu wapo kwa ajili ya kuokoa mazingira. Kwa hiyo jambo hilo linahusisha wizara nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ombi langu, hizi wizara nne zingetafuta namna ya kuli-*coordinate* hili jambo kusudi likapata mtu mmoja wa kulisimamia. Namna lilivyo sasa litapotea hewani halafu utabaki kuwa mtaa wa maonesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Constantine Kanyasu nilimtaja Mheshimiwa Abubakar Asenga, Mheshimiwa Fakharia Shomar na Mheshimiwa Riziki Lulida wajiandae.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru sana kwa nafasi ya kuchangia hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa kuanza na mimi nimpongeze Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mambo makubwa anayoyafanya katika nchi yetu. Uongozi wake unalifanya Taifa letu limeendelea kuwa tulivu sana, na hata pale tunapopata changamoto kubwa hizi za mijadala ya kisiasa bado nchi yetu imetulia sana. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhusu Hassan kwa miradi mikubwa ambayo amatuletea katika Jimbo la Kilimbero; na hasa hasa ametuletea viongozi makini wa Mkoa wa Morogoro. Ametuletea Mkuu wetu wa Mkoa Mama Fatma Mwasa na Mkuu wa Wilaya mpya Wakili Dunstan Kiobya; kwa kweli wanafanya kazi kubwa nzuri. Tunawaombea afya ili waendelee kumsaidia Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni Bunge la Bajeti tunajadili mambo ya bajeti, na katika bajeti ni mipango na matumizi. Kama nilivyosema awali, ni kwamba kuna aina nyingi za bajeti lakini katika nchi yetu tuna bajeti ambayo tunapanga matumizi mengi halafu baadaye tunatafuta vyanzo vya fedha. Sasa katika Hotuba ya Mheshimiwa Rais juzi akipokea taarifa ya *CAG* ametuonesha njia Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwambakuna sehemu tukiwekeza, tukiacha uoga tutapata takriban 50% ya bajeti ya nchi yetu. Mheshimiwa Rais anasema tuache uoga katika uwekezaji wa bandari; 50% anayosema Mheshimiwa Rais tuna bajeti takriban ya trilioni 40 hapo. Mheshimiwa Rais anazungumzia trilioni 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi kama Wabunge katika vitu ambavyo tulitakiwa tuvikimbize ni kuhakikisha hii trilioni 20 ya bandari tunaipata kwa wakati. Kwa sababu mambo mengi tunayozungumza hapa, tunaomba na mimi nitasema mengine ya kuomba hapa. Kwa hiyo naishauri Serikali, namshauri Mheshimiwa Waziri Mkuu, leteni marekebisho kama ya Sheria ya Ununuzi ya kukaribisha hawa wawekezaji wanaotakiwa. Wabunge tumetembea hapa tumeona nchi za wenzetu wanavyowekeza katika bandari na matrilioni ya fedha wanazopata. Sasa kama una gari sasa hivi pale inatupa trilioni moja, kuna mtu anaweza akaja akatupa trilioni 10 ama 20 ni kitu cha kufanya haraka; trilioni si fedha ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeenda India; pale Mundra miaka 20 iliyopita ilikuwa pori, sasa hivi wana *port* ambayo inaongoza kwa mapato India na Asia. Sisi tuna Bagamoyo pale tunajadiliana tu, waoga, bandari isibinafsishwe. Mheshimiwa Rais amefafanua vizuri sana; tuache uoga, tuwekeze, tuwape watu wenye mifano ya kuendesha bandari duniani tupate pesa. Wabunge tunalalamika hapa kituo cha afya, mama ana-*click* tu unapata kituo cha afya. Mimi namshukuru sana Mheshimiwa Rais pale sasa hivi ameteua wakurugenzi wa bandari ile vijana wadogo kama

mimi hivi lakini ukiwasiiliza unajua hawa ni watu wa biashara na hawataki mchezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba sana. Kabla sijalalamika mambo mengine huko na kuomba fedha anzeni mambo pale, sheria zije hapa kama za ununuzi zina mchakato mrefu zibadilishwe ili uwekezaji ufanyike tupate fedha; hilo la kwanza la mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili nilitaka kuzungumza kuhusu maadili kama wenzangu walivyosema hapa. Kuhusu hili jambo la maadili nafikiri sidhani kama sisi Wabunge tunapata muda wa kuzungukazunguka Dar es Salaam tu peke yake. Mimi nilikuwepo wakati ule Makonda anaanza kufanya yale mambo ya kupambana na hawa watu na jambo hili. Najiuliza kwa nini Tanzania sisi hatunyooshewi vidole na nchi hizi ambazo zina-*support* ushoga duniani. Kuna sehemu hatujafanya vizuri, ni kama jambo hili linachekewachekewa. Mimi nina watoto wawili wa kiume nikiwaangalia watoto wangu nikisoma vyombo vya habari, ni jambo la hatari; na viongozi wetu muwe makini sana kwenye harusi mnazokwenda. Mnaenda kwenye harusi mnasherekea harusi, mnacheza pale unashangaa wale watu wanakuzunguka pale picha inarekodiwa zinasambazwa huku mnaonekana na ninyi viongozi mna-*support* jambo hilo. Jambo la hovyo la mambo mabovu ya maadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, katika *East Africa* tukigawanyika katika kutetea jambo hili tumeumia. Tazameni Uganda kinatokea nini kwa Museveni. Museveni alivyoanza ku-*fight* jambo hili nini kinampata? *East Africa* sisi tumekaa tunaziangalia namna gani. sasa kuna mwanasheria mmoja ametushauri Wabunge, ameandika hapa amesema sheria yetu peke yake itakuwa ngumu sana ku-*fight* mambo haya ya ushoga na mambo ya jinsia moja. Akasema kifungu 154 cha sheria kinazuia kuingilia kinyume cha maumbile, hakizuii ushoga mwandishi kafafanua kwa ufupi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba dakika moja nisome. Anasema kifungu cha 154 cha Kanuni za Adhabu kinazuia mwanaume kumwingilia mwanamke kinyume cha maumbile na mwanamume kumwingilia mwanamke kinyume cha maumbile. Adhabu ya kosa hili ni kifungu cha miaka 30 yamkini kifungu hiki hakiwezi kuzuia ushoga kwa sababu ili mtu apatikane na hatia ni hadi athibitishe kuingilia, *anus penetration.* Sasa nani atathibitisha kuingilia kati ya aliyeingiliwa na aliyeingilia wakati wote wanafanya kwa hiari. Kifungo hicho kinashindwa kuanzia hapo, hii maana yake hata ukiwaona wanafanya bado unashindwa kuthibitisha kuingilia hata hivyo utawaona wapi wakifanya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uganda adhabu ya kuingilia ni hadi miaka 10 wakati kwetu ni maisha ama miaka 30. Hata hivyo Uganda wanafanikiwa kuzuia matendo haya kwa sababu sheria yao haijaishia kwenye kuingilia watu wao wanashughulikia matendo ya ushoga na usagaji kwa ujumla wake wakati huku tunashughulikia kuingilia ni maelekezo mawili tofauti. Mwanasheria anasema; na ndio hii sababu unaona sisi tuna adhabu kubwa lakini hatupingwi, hatupigiwi kelele za kimataifa na wanaotetea ushoga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, anaendelea kusema ni kwa sababu wanajua kuwa sheria ya Uganda inaweza kufuta janga hili wakati ya kwetu haiwezi. Uganda kuingilia kinyume cha maumbile ni kosa, kuonesha ama kuvaa au kufanya kiashiria chochote cha ushoga na usagaji ni kosa, kujitangaza kuwa ni shoga ama msagaji ni kosa. Mwenye nyumba, mwenye hoteli, lodge, gesti kumpangisha shoga na msagaji ni kosa. Kuvaa mavazi yanayoashiria mwanamme kuwa shoga au mwanamke kuwa msagaji ni kosa, kaka zetu wanabinukabinuka huko mtaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chombo chochote cha habari ama mtandao wa kijamii kumtangaza katika namna yoyote kukubali vitendo hivyo ni kosa na mengine mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uganda ushahidi wa kimazingira unaweza kukuwajibisha kuwa ni shoga. Hatuwezi kuishia kuzungumza kuwa hata wanyama hawafanyi hivyo halafu ushoga ukaisha, tunahitaji hatua za kisheria za kushughulika na watu hawa. Wako huko kwenye maharusi, wako huko mjini watoto wa kiume wanavaa blauzi, wanabinuka binuka, wawakamate, watengeneze jopo la Madaktari, wathibitishe, wawafunge. Waziri Mkuu ni Muislamu, Rais Muislamu, Dkt. Mpango Mkristo, Mwenyezi Mungu, atawauliza wakati wamepewa madaraka ya kuongoza nchi hii walichukua hatua gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipata semina moja ya Mzee Kinana anasema kuna namna nyingi, ninyi ambao mna *machine tools* za ku–*deal* na mambo hayo wanaweza wakafanya wakapotea watoto wa kiume wanaovaa magauni na kubinuka mjini. Waende kwenye maduka Sinza watazame watoto wa kiume wanabinuka binuka hovyo, wanavaa vibatiki, sidiria, watoto wa kiume! Sasa sheria zetu haziwezi kufanya hivyo, tunapiga piga *mark time* hapa, walete sheria kwamba uki–*post* unakamatwa, tabia zako hazieleweki unakamatwa, jopo la Madaktari wanakaa wanathibitisha. Watazame sheria ya juzi Mahakamani pale, yale mambo ya Zanzibar anasemaje yule mtalam pale, anasema: "*Ninachoweza kuthibitisha ni kwamba tundu la huyu mtu unaweza kuingiza vidole viwili.*" kaishia pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watu wanavaa blauzi, kwani sisi tunakereka na ushoga kwa taarifa ya Mwakyembe na zile taasisi kwa sababu gani? Kwa sababu watu wanaonekana, sikilizeni taarifa ya Mwakyembe, sikilizeni yule dada na yule aje afanye *presentation* hapa mwone. Usiku kuna mzungu Masaki huko anakusanya mashoga wanafanya *party*. Sasa hili ni jambo ambalo kama tunakereka nalo, Serikali wana *machines,* watumie kwa hawa, wawapakie kwenye malori, wawapeleke kwenye magereza, sisi Idete

kule, Kilombero kule magereza yetu ndiyo magereza yanayoongoza kutokuwa na watu wa kutosha, wawalete kule wawafunge na mashamba ya kulima yapo, unalima na jembe futi moja hivi, waje kule walime. Watu wanachezacheza hapa ushoga, ushoga, tunalalamika tu, wawakamate hao watu wawatie ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kwa sababu ya muda, nataka kumshukuru Mheshimiwa Rais, kwa miradi mikubwa ambayo ametuletea lakini hasa hasa niseme kuhusu Barabara yetu ya Ifakara – Kidatu, kweli Mheshimiwa Rais ametusaidia. Utakumbuka nilitaka kukaa chini kwenye kapeti hapa kuhusu Barabara yangu ya Ifakara – Kidatu, lakini tangu Mheshimiwa Rais Samia ameingia miaka miwili hii tayari nina kilomita 42 katika kilomita 66 za lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wakati huu tayari tumeshapata bilioni 42 za Mradi wa Maji wa Kiburubutu. Nimejulishwa hapa tayari tuna pesa ya *VETA* iliyoenda kujenga Chuo cha *VETA* pale Ifakara ambapo *advanced* milioni 45 imeenda kwa ajili ya ku–*clear* eneo na tumepata Mahakama mpya. Namshukuru sana Waziri wa Mambo ya Ndani alikuja Kilombero na ni imani yangu atatusaidia kupata Kituo cha Polisi chenye hadhi ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru Serikali katika mikakati yake ya Kilimo, Waziri Bashe, ametuambia kwa mara ya kwanza Serikali itaanza kununua mpunga kwa bei nzuri, tunaomba mbolea iwahi, tunaomba suala la wakulima wa miwa lifanyiwe kazi, tunashukuru kwa kiwanda cha sukari kipya kinaendelea, tunaomba kikamilike kwa wakati, tunashukuru Mheshimiwa Rais, kwa sekondari nane mpya tumejenga. Tumejenga zahanati nne, tumejenga vituo vya afya viwili, juzi ametuingizia milioni 300 Ifakara za sekondari, ametupa milioni 470 za sekondari *advanced*, ametupa milioni 500 juzi la Jengo la Mama na Mtoto katika halmashauri yetu na ametupa bilioni 13 za Mradi wa *Substations* ya kukuza

umeme Ifakara, ametupatia lami kilomita mbili Ifakara, ametupatia lami Mwaya na mambo mengi Mheshimiwa Rais, ametusaidia kufanya. Tangu dunia iumbwe Halmashauri ya Ifakara na Wilaya ya Kilombero haijawahi kupata fedha nyingi kiasi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya alikuja Ifakara, akatembelea *St*. Francis Hospitali, ni Hospitali ya Rufaa, hospitali ambayo inasaidia halmashauri tano na wilaya tatu, Baba Askofu pale anaomba msaada kwa sababu tunashirikiana na Serikali *CT–Scan, MNRI* na *Ultrasound* za kisasa, naomba Waziri awasaidie, kama alivyofika pale ametembelea, ameona hali halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba viwanda, tuna majengo tayari ya viwanda. Kutokana na kwisha kwa muda naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abubakari Asenga, ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Fakharia Shomar na Mheshimiwa Riziki Lulida ajiandae.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante. Kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu pamoja na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa Hotuba yake nzuri, ilikuwa ndefu lakini tumemwelewa dhima na dhamira yake aliyoikusudia kwa Tanzania na kwa Bunge zima. Vile vile sina budi kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Mama Samia, kwa kazi nzuri anayoifanya kwa kuiletea maendeleo Tanzania pamoja na Mheshimiwa Hussein Mwinyi Rais wa Zanzibar, kwa kazi nzuri kwa kushirikiana bega kwa bega na Mama Samia, kwa kuifanyia kazi Tanzania na Zanzibar kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 27, Serikali ilizungumzia jinsi Mahakama zetu zilivyoongeza watendaji ambao Majaji wa Mahakama ya Rufaa, Mahakimu na

baadhi ya viongozi wengine kwa kuweza kufanya kazi kwa weledi katika Mahakama zetu, lakini kwa kweli utendaji bado uko chini, siyo wa kiwango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameongezwa lakini kazi iko vile vile *as usual,* kwa sababu umewekwa pale kama Hakimu, wamewekwa pale kama Majaji Wakuu lakini kazi wanazozifanya na watendaji wao haziridhishi raia, raia bado wanapiga kelele, Mahakama hazitendi haki, mahakama zinakawia kufanya shughuli zake na mwisho hata hayo magereza yetu pia yameambukizwa kwamba nayo yanafanya kazi chini ya kiwango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija ukurasa wa 86, hii ambayo inazungumzia shughuli za Muungano, imesema kwamba kulinda, kuenzi na kudumisha Muungano wetu. Hili ni kusudio kubwa kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikishirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Nasema hivyo kwa sababu nilimwona Mama, Mheshimiwa Dkt. Samia kipindi kile alichopewa pesa za UVIKO, alikasimu akaleta Zanzibar na huu ndiyo mtazamo mwema wa Muuungano kwa sababu zilikuja Zanzibar zimetenda kazi katika Sekta za Jamii, Sekta za Afya, Sekta za Elimu na Sekta za Maji. Sasa hapa moja kwa moja unaona kwamba Muungano wetu unafanya kazi pande zote mbili. Kinachopatikana huku na huku kinapelekwa, Mwenyezi Mungu ambariki Mheshimiwa Rais, wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri ya jinsi anavyotuangalia raia yake kwa pande zote mbili za Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja katika ukurasa wa 84, unaozungumzia ukatili wa watoto. Mheshimiwa Waziri Mkuu, alisema kwamba kuna mikoa nane ambayo imeunda Madawati ya Ulinzi na Usalama ambayo madawati hayo yako 1,993. Nasema hivi, haya madawati ni kidogo kwa mikoa nane madawati yawe kwa Tanzania nzima, hali

imebadilika sasa hivi Tanzania, tunasikia mambo yanavyokwenda, tunasikia watoto wetu wanavyodhalilika, tunasikia watu wanavyopenyapenya wa kutaka jinsia moja, sasa hii dawati ikiwepo itatoa elimu nzuri na watoto watakuwa rahisi kwenda kuwa–*face* kule na kuweza kuzungumza. Nasema hivi kwa sababu tatizo lililopo sasa hivi ulezi tumeuachia Serikali, wenyewe wazazi kila mmoja yuko *busy* anatafuta maisha na kwa vyovyote Serikali haiwezi kulea mtoto, mtoto alelewe na wazazi wake kwa kushirikiana na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar na Tanzania Bara zote zinahitaji kuangaliwa kwa jicho pana, kwa sababu hili jambo lipo sehemu zote za Tanzania na tunatakiwa tuungane ili kulipiga vita. Unajua ushoga si jambo zuri, bora akuharibikie mtoto mwanamke unajua ataolewa, atastirika, lakini akikuharibikia mtoto mwanaume *kwishinei*, kaisha, hawezi kitu. Taifa litakuwa limeharibikiwa, mzazi kaharibikiwa na yeye mwenyewe kaharibikiwa, ina maana hawa madada poa na makaka poa Tanzania wawe hawana nafasi. Maana kama hatukukazana hii aibu haitokuwa kwa yule mtendwa na mtenda, itakuwa aibu kwa Taifa letu. Tupige kelele, tupaze sauti, twende na sheria, tuwe na uwajibikaji kwa vitendo Serikali tuwajibike kwa vitendo siyo kupiga kelele, tukipiga kelele hili jambo mtu anaona ahaa si wanasema tu, lakini kama tutakuja kwa vitendo hili jambo litakoma. Tanzania bila ya ushoga inawezekana, tujikaze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija ukurasa wa 83 haya ya 199, hili linazungumzia kuhusu sheria ziwe za Kiswahili, tuzitafsiri, siyo mbaya kwa sababu hii itatatua migogoro kwa wananchi. Baadhi ya wananchi hawazifahamu hizi sheria kwa Kiingereza na hili si gumu kwa sababu wenzetu Baraza la Wawakilishi Zanzibar wanalifanya. Ya Kiingereza iwepo na ya Kiswahili iwepo na nashukuru Dkt. Samia Hassan Suhuhu, kalibariki hili lifanyike na katika maelezo ya Waziri Mkuu kalisema, sasa naomba hili jambo lifanyike ili nasi ile dhamira iliyokuwa

imekusudiwa itekelezwe na mambo yetu yote waweze kukaa sawa na tuweze kufanikiwa. *(MakofI)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Fakharia Shomar. Tunamalizia na Mheshimiwa Riziki Lulida.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nikushukuru. Pia nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kutujalia afya njema na kuwepo hapa. Nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa Hotuba nzuri ambayo ametuletea hapa, tuzidi kumwombea Mwenyezi Mungu, amjalie aweze kufanya kazi kwa njia akiwa na afya njema na atubariki sana tumepata bahati nzuri kuwa na Waziri Mkuu msikivu, mpole, mwenye hekima, ana uwezo mkubwa, Mwenyezi Mungu mbariki zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nipo hapa kumshukuru sana sana Mheshimiwa Rais wangu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Samia Suluhu Hassan, ni mwanamke jasiri ambaye ana upendo kwa kila kona anaonyesha nini anachokifanya na mimi nitazungumza kwa yale ninayoyaona kwa macho yangu kama ushuhuda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania asilimia 67 ni vijana na hawa vijana ni kundi kubwa ambalo inabidi lifanyiwe kazi ili kuweza kuleta uchumi wa nchi. Leo tunaona vijana wanamaliza vyuo vikuu, wanamaliza katika maeneo mbalimbali lakini hawana ajira na Wizara tuliyokuwa nayo hii sasa ya Wizara ya Vijana, Kazi na Maendeleo ya Jamii kuna hitaji msukumo mkubwa sana wa kuhakikisha kuwawezesha hawa vijana baadaye usije ukawa mzigo wa nchi. Nitazungumza kwa ninayoyafahamu, leo hili vijana hawa waweze kupata ajira, wajiajiri wenyewe, Serikali ni lazima

ihakikishe inawapelekea fedha na inapeleka fedha kwa wakati ili waweze kusomeshwa na wajiajiri wenyewe baadhi ili kuweza kusukuma uchumi wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilikuwa katika mkutano wa madini. Tumeambiwa wachimbaji wadogo wadogo ambao ni vijana na wanawake wameweza kuleta pato la Taifa asilimia 40 *vis-a-vis* wawekezaji wakubwa lakini changamoto waliyokuwa nayo wale wanasema hawana mitaji, hawana vitendea kazi. Sasa kama hawa wanaweza kuleta pato la uchumi mkubwa kwa asilimia 40, unayaachaje makundi haya yasiwezeshwe? Tunakwenda katika bajeti kuna *SGL* ambayo inabidi iende asilimia 30 iende kwa vijana, walemavu, wanawake lakini nimeshangaa imepelekwa bilioni tisa badala ya bilioni 87.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukajaribu kujadiliana wakasema baadhi ya pesa hizi zinakwenda kwa mifuko (mkopo) *board loan,* sawa, lakini haiwezekani bilioni 87 zote wapeleke katika mikopo ya wanafunzi, wanaliacha hili kundi kubwa ambalo linaingia mtaani, halina kazi, halina mtaji, wanategemea kuzalisha kitu gani? China, India, Singapore, Malaysia walisimama na vijana na walihakikisha wanasoma katika *vocational training centers* ili badaye waje waweze kujitegemea wao wenyewe kwa kuweza kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaambiwa katika eneo hili hapatengwi pesa ya kutosha, wanasema hawaweki pesa, kama huweki pesa unategemea hili kundi wanalipeweka wapi? Hili kundi litatuletea zogo baadaye maana yake vijana wakikaa baadaye akijiona amemaliza *PhD*, sina kazi, si ajiriwi, watu wanaajiriwa kwa mafungu ambayo ni ya watu wachache, makundi maalum, hawa vijana ni lazima, naomba hizi pesa tulikubaliana juzi na Waziri wa Fedha, atakuwa shahidi walisema watakwenda kukaa, nataka waje watuambie hapa wametenga kiasi gani angalau basi

watupe robo. Katika bilioni 87 wakitupa robo angalau kundi hili la watu 42,000 ambao tumepanga waanze kupata mafunzo liweze kufanya kazi. Si hivyo tunawapa mzigo mkubwa Wizara ya Kazi na Vijana wakati hawana kazi ya kufanya nao na tutahakikisha vijana hawa badala ya kupata mafunzo maalum, itakuwa vijana hawa ni vibaka, ombaomba mitaani na tutaendekeza wengine wajiingize katika masuala ya ushoga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetembelea maeneo mbalimbali, tumekwenda Tengeru Meru. Vijana wana *degree* zao wameamua kutengeneza *greenhouse* zao, wale vijana sasa hivi wanauza mboga, wanauza matunda, wanapeleka maua nje ya nchi. Matokeo hayo ni kwa sababu wamepewa *incentive,* tujifunze Halmashauri ya Meru nini wamefanya kuwasaidia wale vijana ili halmashauri zingine Tanzania nzima wajifunze ili kuhakikisha vijana waliopo kule wanapata mafunzo na wanapewa *greenhouses* ili wawatoe katika umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kundi maalum la watu wenye ulemavu; toka mwaka 2015 tunazungumza mpaka leo hawajaweka bajeti hata senti tano katika Kifungu cha Vijana na Mikopo. Leo walemavu nina *PhD* za walevu zaidi ya sitini hawana ajira, nina *masters* za walemavu hawana ajira, nina *degree* za walemavu hawana ajira, basi hata fungu lao la hela hawawekewi *allocation* ya *funds* hata kidogo. Walisema watatupa bilioni tatu, mpaka leo napata kigugumizi kusema kuwa hata senti tano haijawekwa. Mimi ni mlengwa, ni mlemavu niliyepata ulemavu nikiwa hapa Bungeni, naona maumivu makubwa ambao wanapata watu wenye ulemavu katika kuwa kwanza hawaajiriwi, wanawaona kama siyo haki yao ya kuajiriwa, lakini hata hii mikopo yao ya kuwasaidia hili waweze kujiendesha wenyewe nayo ni kigugumizi. Hii ni Wizara na hii kama ni Wizara wote watu wa Wizara wananisikiliza, hili kundi maalum la watu wenye ulemavu na hizi bilioni tano ambazo Waziri wa Fedha alisema atazitoa,

naomba zifanye kazi na zitolewe ili hawa watu isije ikawa baadaye ni mzigo na kulaumiwa wanaitwa ombaomba sijui maskini, lakini si maskini hawa wana akili tosha na wana uwezo tosha wa kufanya kazi. Mfano Mbogwe, *STAMICO* tena Wizara ya Madini inasimama na watu wenye ulemavu wamewapa vitalu, wanachimba dhahabu, kwa maana moja hata mlemavu ukimwezesha anaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia barabara Mkoa wa Lindi, ni toka tumepata Uhuru na Waziri Mkuu wa Kwanza wa Tanzania hii alikuwa Mheshimiwa Rashid Mfaume Kawawa, anatoka Liwale. Barabara ya kutoka Nangurukulu mpaka Liwale mpaka leo ni kigugumizi, hakuna jibu linalotolewa na Serikali, tumedanganywa sana kuhusu barabara ya Liwale, barabara hiyo ya Liwale hata kumuenzi Mheshimiwa Rashid Mfaume Kawawa, ambaye alikuwa Waziri Mkuu wa Nchi hii. Barabara ile haitengewi, watu wa Liwale leo wanakwenda huko kwa siku mbili anatoka hapa anakwenda mpaka Lindi, Lindi Nachingwea, Nachingwea anakwenda mpaka Liwale. Naomba nipate majibu kwa nini Barabara ya Lindi ya Nangurukuru – Liwale mpaka Nachingwea imekuwa kigugumizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nitazungumzia masuala ya kijinsia. Ukisikia neno demokrasia ndani kuna jinsia, Tanzania ni Nchi huru, Tanzania tuna utamaduni wetu, Tanzania tuna *culture* yetu sasa hatutaki kuingizwa katika mambo ambayo wao wanayataka kwa ufirauni wao ili kutuletea Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu cha Quran nitazungumza kwanza huko, wanasema "*Walaa taqrabu zinaa, innahu kana faahishatan wa saa sabiila*" akasema tena "*Azaniyatu wazanii fajilidu kulla wahda miatu-l-jadda*" hakika vitabu vyote Biblia na Quran vinakataza zinaa, lakini siyo zinaa tu, ikija huko ndiyo hatari kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitaje miji ambayo ni hitarishi sasa hivi ambayo inaangamia kwa ajili ya ushoga. Kwanza Zanzibar, watalii wanaokwenda Zanzibar wako huru wanakuja wanaume kwa wanaume, wanalala mahotelini, tunataka Zanzibar ionyeshe mfano. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Riziki Lulida, ahsante sana.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru kwa kumalizia mchango wako. Waheshimiwa Wabunge, tumefikia mwisho wa michango yetu ya makazi yetu ya asubuhi hii hadi kufika mchana. Nawapongeza kwa michango yote ambayo kwa kweli naamini Serikali iko makini hapa inasikiliza na inafuatilia kwa umakini wa hali ya juu, lakini kama sikutilia mstari kwenye suala ambalo limeibua hisia la masuala ya ndoa ya jinsia moja na naamini kidogo kwamba swaumu yangu sitoitendea haki.

Waheshimiwa Wabunge, ushoga ama ndoa za jinsia moja kwa kiasi kikubwa ni chimbuko la kuwaharibu watoto wetu wakati ni wadogo. Kwa asilimia kubwa sana tukitaka tusitake, kuwalawiti na kuwaharibu watoto wadogo ndiyo chimbuko linalokwenda sasa kutupeleka kwenye janga la ushoga katika Taifa letu. Kwa hiyo pamoja na kupaza sauti zetu kwenye suala la kupiga vita ushoga Serikali, Bunge, taasisi zinazosimamia haki, wazazi, walezi pamoja na jamii kwa ujumla kama tusipofanya hima kwenye suala la kudhibiti uharibu wa Watoto, suala la ushoga litakuwa gumu kuli–*handle*. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naomba nitaje majina ambayo yatachangia jioni Mheshimiwa Emmanuel Shangai, Mheshimiwa Japhet Hasunga, Mheshimiwa Almas Maige, Mheshimiwa Dkt. Pius

Chaya na Mheshimiwa Luhaga Mpina. Hayo ndiyo majina ambayo wataanza kwa jioni.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 10.00 jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Ofisi ya Waziri Mkuu Mwaka wa Fedha 2023/2024**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Waheshimiwa, tunaanza Kikao chetu cha jioni kwa kumuita Mheshimiwa Emmanuel Shangai, ajiandae Mheshimiwa Hasunga.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwamba ameendelea kunilinda na kwamba nipo hai sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa kuendelea kuwatumikia Watanzania kwa weledi mkubwa sana, ninamshukuru pia kwamba kwenye Jimbo letu la Ngorongoro tumeendelea kupata

fedha nyingi sana kwa ajili ya maendeleo zikiwepo fedha za afya, elimu, maji pamoja na umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba pia nichangie hoja ambayo Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia katika Bunge lako, kuhusiana na masuala ya ufisadi kwenye nchi yetu. Nimesikia kwamba Wabunge wengi wanasema hao watu watupishe. Watupishe waende wapi? Wanatakiwa warudishe fedha za Watanzania ndiyo waweze kitupisha, hili linatakiwa kufanyika na wale wote waliopewa mamlaka na Mheshimiwa Rais, kwa sababu inaonekana Mheshimiwa Rais yeye amechukia ufisadi sana, lakini inaonekana kwamba baadhi ya watu ambao ni wateule wa Mhehsimiwa Rais, hawauchukii ufisadi ndiyo maana tunamuona Rais anachukia lakini watu wengine wamenyamaza.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Jimbo langu la Ngorongoro tumepata fedha nyingi kwa ajili ya maendeleo lakini kunakuwepo na vikwazo vingi sana. Kwa mfano, leo Wizara ya TAMISEMI inaleta fedha kwa ajili ya ujenzi wa madarasa lakini unampa mtu wa Ngorongoro shilingi milioni 20 ajenge darasa sawa na mtu aliyeko Dar es Salaam! Kule ukitoa *cement* kutoka Arusha mpaka Ngorongoro *cement* inafika kwa shilingi 25,000. Mwananchi aliyeko Arusha Mjini ananunua *cement* kwa shilingi 16,000. Inatakiwa tunapotoa fedha kwa jaili ya miradi ya maendeleo tuangalie umbali na mazingira katika Majimbo yetu. Siyo unampa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro milioni 20 ajenge darasa na hivyo hivyo unampa mtu wa Dar es Salaam Milioni 20, Mkurugenzi wa Dar es Salaam ananunua *cement* kwa shilingi 14,000 mpaka 15,000 lakini Ngorongoro *cement* inafika kwa shilingi 25,000, yule Mkurugenzi utakuwa unamuonea!*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawaomba watu wa TAMISEMI wanapanga miradi ni lazima waangalie maeneo

wanayopeleka hizo fedha. Unampa Mkurugenzi shilingi milioni 400 ajenge Sekondari akiwa Dar es Salaam, akiwa Morogoro unampa pia na wa Ngorongoro ajenge kwa shilingi milioni 400. Wakati kule hata lori ya mchanga ni zaidi ya shilingi 300,000 lakini kusafirisha kutoka Arusha mpaka Ngorongoro unatumia gari za shilingi 1,500,000 mpaka Ngorongoro wakati mtu wa Arusha anakodisha gari kwa shilingi labda 200,000 tu. Kwa hiyo, ukijaribu kuangalia ni lazima tutekeleze miradi, tutenge fedha za miradi kwa kuangalia maeneo. Majimbo yetu yaliyoko mbali ni lazima tu – *consider cost* tunazowapa.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Jimbo letu la Ngorongoro huduma zetu za afya bado ni duni sana. Ukijaribu kuangalia kwenye Kata zetu. Kati ya kata 28 unakuta kwamba ni zaidi ya Kata Sita tu ndiyo zenye vituo vya afya lakini Kata nyingine 22 hakuna vituo vya afya. Kwenye Vijiji pamoja na Kata hakuna zahanati, lakini mwaka jana Serikali ilisitisha huduma kwa ajili ya ndege ya *Fly Medical Service* iliyokuwa inatoa huduma ya chanjo kwenye vituo 18 ndani ya eneo la Ngorongoro. Kupitia Hospitali ya Wasso kulikuwa kuna vituo 10, kupitia Hospitali ya Kanisa ya Endulen walikuwa wana vituo Nane lakini Serikali imesitisha huduma hiyo. Kwa hiyo, wale wananchi waliokuwa wanahudumiwa kwenye vituo 18 kwenye Kata ambazo hazina zahanati na Serikali haijafikisha barabara katika yale maeneo wananchi wale hawapati huduma ya chanjo, watoto wadogo pamoja na wakina mama wajawazito.

Mhehsimiwa Naibu Spika, ninaishauri Serikali tuiangalie kwa sababu ndege ile imesajiliwa Marekani mwaka 1979 na imetoa huduma Tanzania kwa miaka yote 44 bila shida, lakini hatujui ni nini kimetokea mwaka 2022 ndege ile ikanyimwa kufanya kazi. Wale wananchi wakina mama wajawazito ambao hawana namna ya kufikia hospitali na watoto kupata chanjo ni wakati muafaka sasa Serikali kuwaruhusu wale

wamisionari waweze kutoa huduma tena katika eneo la Ngorongoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishauri Wizara ya Afya pamoja na Wizara ya Uchukuzi, Waziri wa Afya Mheshimiwa Ummy Mwalimu anajua nilishamwandikia, Waziri wa Uchukuzi anajua, pamoja na Waziri Mkuu anajua nilishamwambia suala hili kwa muda mrefu, toka mwaka jana mwezi wa Sita mpaka sasa hivi kuna watoto wadogo wanazaliwa na ambao wana miezi Tisa sasa hawapati huduma.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu ilikuwa inaratibu suala lingine la kuhama kwa hiyari eneo la Ngorongoro. Suala lile hakuna mtu anayepingana na mtu anayehama kwa hiari, wananchi wamendelea kwenda wenyewe. Tumeona kwenye ripoti ya *CAG* kwamba wananchi waliohama ni 2.5 *percent* ambayo ni kaya 500 zenye watu zaidi ya 2,580, lakini wananchi wengine waliobaki kwa sensa ya juzi ni zaidi ya kaya 25 ambazo zina watu zaidi ya 100,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakaa, siku ile Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema hapa kwamba ni suala la hiyari, lakini wananchi waliobaki zaidi ya 100,000 ukienda kwenye eneo la Tarafa ya Ngorongoro kuna shule zaidi ya 26 za msingi zenye watoto zaidi ya 18,167. Watoto wa Sekondari zaidi ya 3,250 hakuna vyoo, watoto wanaenda chooni porini kwa sababu Serikali imekatalia kujenga vyoo, vyoo vimejaa, hawatoi ruhusa ya wananchi kujenga vyoo kwa ajili ya watoto wao, kwa nini hili linatokea kama suala lenyewe ni hiari kwa nini watu walazimishwe kuishi katika maisha ambayo hayafai kwa binadamu?*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri kwamba ni lazima Serikali iweke wazi lengo lao kwenye eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, kama ni kuhama kwa hiari watu wanaondoka lakini mpaka leo watu waliojiandikisha ni kaya 1,500, lakini

mpaka leo wamechukua kaya 500. Wale waliobaki kaya zaidi ya 1,000 hawana mbele wala nyuma hawajui wanafanya nini, wako *stranded* katika maisha yao hawawezi kuendelea tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninaomba katika eneo letu la Tarafa ya Ngorongoro Wizara ya TAMISEMI inapanga fedha inapelekwa wananyimwa vibali kwa ajili ya kujenga na watoto wanakaa madarasani mpaka nje. Ni lazima Serikali iweke wazi wale wananchi wasiendelee kuishi kama watu ambao hawatambuliki kama watu ambao hawatambuliki katika nchi yao. Ni vizuri tujue kwamba wale wananchi wako pale lakini suala hili ni la hiari. Suala lenyewe limekuwa ni upigaji mtupu, angalia leo usafiri kutoka Ngorongoro mapaka Handeni gari ni sawa na kontena kutoka China kuja Tanzania ni ufisadi mtupu. Watu wanajitochotea fedha, watu wanawalipa watu ambao hawahusiki, unakuta nyumba zingine ni hewa. Nyumba unaandikiwa namba 59 hiyo nyumba haipo, mkatafute, au nyumba namba 57 na 58, 55 na 56, nyumba hazipo, watu wanajiandikia wanajichukulia fedha za Serikali.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichoonekana kwenye ripoti ya *CAG* ninaishauri Serikali mkafuatilie ule mradi muone kwamba ni mradi wa watu ambao ulibuniwa kulikuwa kuna fedha ambazo zipo walitaka wale wakakosa njia. Eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro sasa hivi watu wanasema limejaa lakini eneo lenye watu ni *five percent only,* maeneo mengine yako wazi, bado inaweza kumudu *model* ya *multiple land use model.*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende tena kwenye suala la barabara yetu ya lami kutoka Wasso mpaka Sare. Tunaishukuru Serikali kwamba tumepata kilomita 49, lakini niiombe Serikali muendelee kutuangalia, Ngorongoro barabara iliyopo ni hiyo moja na ndiyo inashikilia uchumi wa Wilaya yetu ya Ngorongoro. Nimwombe Mheshimiwa Waziri

wa Ujenzi na Uchukuzi, kwamba aliahidi kilomita 50 tunaiomba kwenye bajeti hii iweze kututengea kwa ajili ya wananchi wa Jimbo la Ngorongoro nao kunufaika na matunda ya rasilimali zetu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala la umeme. Tunazo Kata za Malambo, Samunge, Pinyinyi pamoja na Kata ya Kirangi eneo la Mageri pamoja na Bwero Kata ya Samunge na maeneo mengine ambayo hayana umeme kwenye Jimbo letu la Ngorongoro. Wameweka nguzo zaidi ya miaka 5 mpaka sasa hivi nguzo zingine zinaanguka, ninaishauri Serikali sasa iweze kumalizia miradi ya umeme kenye Wilaya yetu. Wananchi wanahitaji maenedeleo na umeme ni maendeleo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ningetaka kulizungumzia ni suala la elimu. Wataalam wanasema ukitaka kuliua Taifa uharibu vitu viwili. Suala la kwanza ni afya pamoja na elimu. Kwenye shule zetu za msingi tunakuwa na mrundikano mkubwa wa wananfunzi ambao inapelekea wengi kuhitimu Darasa la Saba hawajui kusoma na kuandika, nimesikia pia Wizara ya Elimu wako katika utaratibu wa kuweza kubadilisha mitaala yetu. Nafikiri tusifanye elimu kama eneo la majaribio.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Hasunga, jiandae Mheshimiwa Almas Maige, jiandae Dkt. Chaya.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Jambo la kwanza nichukue nafasi hii kwanza kumpongeza…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hasunga *aah sorry*!

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan, pamoja na Makamu wa Rais na Waziri Mkuu kwa kazi kubwa ambayo wameendelea kuifanya katika kuleta maeneleo ya nchi hii. Sote tunashuhudia Rais halali, usiku na mchana anahangaika huku na huko kutafuta rasilimali kwa ajili ya maendeleo ya nchi hii na maendeleo ya Watanzania. Nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Taasisi zake kwa kuja na mipango mizuri ambayo tumeisoma kwenye bajeti hii nzuri kabisa, bajeti ya mwaka 2023/2024, kwa kweli nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali pia kwa kuanza mchakato wa kuja na Dira Mpya ya Maendeleo ya kuanzia mwaka 2025 mpaka mwaka 2050. Dira iliyopo ambayo tulianza kuitekeleza mwaka 2000 mpaka 2025 ilikuwa na vipaumbele vitano ambavyo vilikuwa ni msingi wa kujenga nchi yetu. Kwanza ilikuwa ni kuboresha hali ya maisha ya Watanzania. Sote ni mashahidi miaka 25 sasa bado hali yetu haijawa vizuri sana, maisha ya Watanzania katika maeneo mengi bado hayajaimarika na hiyo inatupa fursa sasa kwamba tuangalie mikakati gani tunaiweka ili tuweze kuboresha maisha haya.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ilikuwa ni kuwepo kwa mazingira ya amani usalama na umoja ndani ya nchi yetu. Katika hili tumefanikiwa kwa kiwango kikubwa sana, hii ndiyo kigezo kikubwa cha kuiweka nchi yetu iwe tofauti na nchi zingine. Tatu ni kujenga utawala bora wenye uwajibikaji ufanisi na wenye tija. Nne, ilikuwa ni kujenga jamii iliyoeleimika na inayoendelea kujifunza na mwisho ni kujenga uchumi imara wenye kuweza kushindana na uchumi wa dunia yaani uwezo wa kukabiliana na ushindani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika hali hiyo malengo hayo ni mazuri na ninaamini hata katika dira mpya

itakayokuja itazingatia haya ambayo tumeyatekeleza yale ambayo tutakuwa hatujafanikiwa basi inaweza ikayapeleka kuyaweka katika dira inayokuja mpya ili tuweze kufikia miaka 50 Tanzania iwe ni nchi tofauti.

Mheshimiwa Spika, yapo mambo kadhaa ambayo ningependa kuchangia, lakini kwa leo nitachangia suala moja nalo ni suala la ajira kwa Watanzania. Tatizo la ajira ni kubwa katika nchi yetu, ajira ni haki ya kila mtu, na tunaposema ajira, iwe ni ajira ya kuajiriwa Serikalini pamoja na Taasisi zake, iwe ni ajira ya kuajiriwa kwenye kampuni binafsi na makampuni yao, iwe ni ajira ya kujiajiri ni haki ya kila Mtanzania kuifanya hiyo, hiyo ndiyo itakayoleta mchango mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukichukua Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Ibara ya 11(1) inasema; Mamlaka ya nchi itaweka utaratibu unaofaa kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa haki ya mtu kufanya kazi, haki ya kujipatia elimu na haki ya kupata msaada kutoka kwa jamii wakati wa uzee, maradhi au hali ya ulemavu na katika hali nyingine za mtu kuwa hajiwezi na bila kuathiri haki hizo Mamlaka ya nchi itaweka utaratibu wa kuhakikisha kwamba kila mtu anaishi kwa jasho lake.

Mhshimiwa Naibu Spika, kumbe hili suala la kufanya kazi ni haki ya Kikatiba, kila Mtanzania lazima afanye kazi. Ukisoma Ibara Ndogo ya Pili inasema kila mtu anayo haki ya kujieleimisha na kila raia atakuwa huru kutafuta elimu katika fani anayopenda hadi kufikia upeo wowote kulingana na ustahili na uwezo wake. Hii ni haki ya Kikatiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia maisha ya Watanzania sasa hivi wapo vijana wengi wamesoma katika vyuo vikuu, wamesoma katika vyuo vya kati, wana taaluma mbalimbali, wapo ambao hawajasoma lakini wote ni Watanzania. Wote wanatakiwa wapate ajira na ajira maana

yake ni kufanyakazi. Sasa hivi ukienda mahali popote, ukienda huku Mijini wapo vijana wengi hawana kazi, hawafanyi kazi. Ukiienda kule vijijini vijana wengi hawafanyi kazi, TAIFA letu haliwezi kujengwa na watu kutokufanya kazi, lazima tuje na mkakati wa kuhakikisha ni wajibu wa Serikali kuratibu kwamba sasa watu wote wanafanya kazi na kila mtu tujue wewe unafanya kazi gani unachangia nini katika nchi, kila mtu lazima tujue na pale ambapo mtu hana kazi ni wajibu wa Serikali kuratibu na kumuonesha kwamba kuna fursa hizi kuna hii kuna hii, wewe unaweza kufanya kipi ili kila Mtanzania afanye kazi, kwa kufanya hivyo ndipo tutajenga uchumi imara.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya umaskini wetu uliopo inatokana na Watanzania wengi kutokufanya kazi. Watanznaia wengi kutokuwa na ajira. Kutokuziona fikra, kutokuziona fursa za kufanya kazi, hii inaturudisha nyuma sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyakazi wa Tanzania wanaofanya kazi sekta ya umma bado maslahi yao siyo mazuri sana. Nina imani Serikali itaendelea kuboresha maslahi yao hawa wafanyakazi ili waweze kufanya kazi kwa weledi, kwa tija na kuleta ufanisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia wapo wafanyakazi wa sekta binafsi ambao tunawasahau, hawa wanalipwa viwango vidogo sana. Vile viwango wanavyolipwa haviwawezeshi kuishi, haviwawezeshi kujenga uchumi, haviwawezeshi kuwekeza, wala haviwawezeshi kulipa kodi. Kwa mantiki hiyo, hatuwezi kuondokana na umasikini kama hatutaweka nguvu katika hili kundi kubwa linalofanya kwenye sekta binafsi ambao viwango vyao ni vidogo. Huu ni wajibu wa Serikali kuratibu na kuangalia tufanye nini ili wapate maslahi mazuri ili walipwe vizuri waweze kufanikiwa. Hili litatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali, ili Watanzania walipe kodi, ili tujenge uchumi, ili tuwekeze; ukilipa vizuri zile hela ndiyo unawekeza na ndiyo unatoa ajira kwa watu mbalimbali. Hawa watu wote wakiwekeza kule, ndiyo ajira zitakuwa zimepatikana. Hatuwezi kuitegemea Serikali peke yake kuajiri watu wote, haitawezekana. Watanzania ni wengi, wote wanahitaji kufanya kazi. Ni wajibu wa Serikali kuratibu kwa mujibu wa Katiba yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufanikisha hili, tulitangaza vita vya ukombozi wa Afrika na tumefanikiwa kwa kiwango kikubwa, Tanzania ikiwa inaongoza ukombozi. Sasa ukombozi ule ulikuwa wa kuleta uhuru, sasa hivi tunahitaji ukombozi wa uchumi, na kubwa zaidi ni ukombozi wa fikra za Watanzania ili Watanzania hawa waone fursa na Serikali iwasaidie hizo fursa waweze kujenga uchumi imara.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila sisi kufungua fikra zetu, bila sisi kufungua nchi hii yenye baraka, nchi hii ambayo ina ardhi nzuri yenye rutuba, ina madini, ina milima, ina maji, ina mbuga za Wanyama, ina kila kitu; Watanzania hatustahili kuwa masikini. Umasikini wetu lazima tukae chini tuone tunautatuaje ili nchi hii iweze kuwa ni yenye uchumi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka kusema, nchi yetu sasa hivi tutangaze vita ya kuja na ukombozi wa kifikra wa Watanzania ili tujenge uchumi wetu. Nchi yetu tunahitaji maendeleo ya watu, tunahitaji maendeleo ya nchi. Nami naamini, kama tutakaa chini na kutafakari haya, Tanzania itakuwa ni nchi bora katika Afrika na duniani. Moja, ni mahali pazuri pa kuishi; pili, ni mahali pazuri pa kufanya kazi; tatu, ni mahali pazuri pa kukaa; na Tanzania ni mahali pazuri pa kuwekeza. Tukijiona hivyo, nchi yetu itafanikiwa kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini dhamana hii Mheshimiwa Waziri Mkuu anayo, ataweza kuifanya vizuri kwa kushirikiana na Mawaziri, kwa kushirikiana na Serikali kwa ujumla, na kwa kushirikiana na Watanzania wote wenye uwezo, wenye weledi, wenye utaalamu wa kila namna, ili nchi hii tuisukume mbele tupate maendeleo, tuondokane na umasikini, tulete miradi ya maendeleo, tuwasaidie wananchi wa Vwawa, wananchi wa Tanzania, wananchi wa Mkoa wa Songwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Almasi maige, jiandae Mheshimiwa Dkt. Chaya na Mheshimiwa Mpina.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nakushukuru sana kuniruhusu nichangie hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo imetandawaa kwenye bajeti yote, lakini pia imekuwa mtambuka kwa maoteo ya bajeti yote ya Serikali kwa mwaka huu unaokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo niko hapa kuipongeza Serikali. Pamoja na upungufu ambao umetajwa na *CAG,* nimeweka kiporo kwa sababu kwa kweli siyo muda wa kujadili hotuba ile, hotuba ile itakuja baadaye baada ya kuangaliwa vizuri kwenye Kamati yetu ya *PAC.* Najua taarifa ile imeonesha uchafu, lakini kuifua nguo inaruhusiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kuipongeza Serikali kwa mambo makubwa; miradi mikubwa ya kiuchumi ambayo imefanya hata ikasababisha uchumi wa nchi hii kubaki kama ulivyo na pia bila kukua kwa bei za vitu. Japo bei zimepanda, lakini kiujumla, nitamke wazi wazi kwamba, sisi hapa tumefanya huu mfumuko wa bei ubakie chini kuliko nchi zote za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi mikubwa ambayo imejengwa na Serikali ambayo inajengwa sasa hatuioni kwamba muhimu, lakini ni muhimu sana. Nikiitaja kwa mfano Bwawa la Umeme la Rufiji, Reli ya *SGR,* ujenzi wa madaraja, ujenzi wa meli kadhaa maziwani, ujenzi wa barabara za kisasa, ununuzi wa ndege, miradi ya afya, miradi ya maji, miradi ya elimu, na kadhalika, mambo haya yakikamilika, nchi hii itapaa na watu wengi watakuja kushangaa kwa nini tulifanya hali ngumu hii na tukamwona Mheshimiwa Mama Samia anahangaika, lakini badaye watu watafaidi na watafaidika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jimbo langu tumefanyiwa miradi mingi sana. Alama ambazo ziko kwenye jimbo langu ni mfano wa kazi nzuri aliyoifanya Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan. Kwanza elimu; bado wanafunzi wanasoma bure, vile vile tumejenga madarasa, nyumba za walimu na kituo kikubwa kabisa cha *VETA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maji, jimboni kwangu kuna mwamba chini ukichimba visima maji yanakauka. Leo tumetandaza maji ya Ziwa Viktoria, tunafungua maji kwenye mashamba na chini ya miti. Leo kuna vijiji 64 vina maji ya bomba kutoka Ziwa Viktoria. Hili siyo jambo dogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu umeme, tulipoanza hapakuwa hata na Kijiji kimoja chanye umeme. Leo kuna vijiji 51 vina umeme katika jimbo langu. Hili siyo jambo rahisi. Pia barabara za ndani, tumekuwa na barabara kila mahali ambako kulikuwa hakuna barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya afya. Sisi jimbo lile ni jipya na Wilaya yetu ni mpya, ilikuwa haina hospitali ya Wilaya. Tumejengewa hospitali ya Wilaya nzuri kabisa, lakini vituo vya afya katika jimbo langu, vinne vinajengwa, vilevile tumejenga zahanati katika jimbo langu na kule kulikokuwa hakuna huduma ya afya, sasa inapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utawala bora. Serikali ya Awamu ya Sita haikutusahau. Halmashauri ya Uyui haikuwa na majengo kabisa. Naipongeza sana Serikali, sasa tuna majengo mapya ya Halmashauri. Hili limetufanya sisi wana-Uyui tujisikie kwamba ni sehemu ya utawala bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo mawili ambayo ninadhani ni muhimu sana niyachangie leo. Katika Jimbo langu na Wilaya yangu ya Uyui tunaishi na ahadi za Marais watatu kuhusu kujenga Kituo cha Afya. Huu ni mwaka karibu wa tatu, wa nne, au wa tano umepita, lakini Marais wote; Marehemu Benjamin Mkapa, Marehemu John Pombe Magufuli na Rais wa sasa waliahidi kujenga kituo. Ilitokea historia ya kituo hiki kujengwa na Marehemu Benjamin Mkapa. Alikwenda kufungua kituo kidogo cha afya, lakini alipokwenda akasema kituo hiki ni kidogo, mimi nina miaka 97, naahidi kwamba, nitajenga hospitali kubwa hapa. Akamaliza muda wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipoingia madarakani tumeenda kuanzisha mradi wa kituo kile, alipokuja marehemu Magufuli, Rais wangu aliyetangulia, nikamwambia kuna ahadi ya Mheshimiwa Benjamin Mkapa, akasema anzeni, nami nakuja kuchangia, tutamaliza, na nitakuja kufungua mimi. Bahati mbaya amefariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia alikuja Tabora Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wangu mpendwa, mama mwenye maono makubwa, nikasimama tena nikamwambia, kuna ahadi ya Marais wawili. Akasema hili jambo litafanyika mara moja. Wakati huo Mheshimiwa Silinde alikuwa Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Akamwambia hili tafuteni hela mara moja, hili limeisha. Sasa kumekuwa na kuhamishwa Mawaziri huku na huku, suala lile la hospitali ile ya ahadi ya viongozi watatu, limekuwa mwiba kwa wananchi, hawaelewi kwa nini hospitali ile haijengwi,

tumejenga sasa mpaka imefikia wodi ya mama na watoto, lakini bado ahadi hiyo haijatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia liko suala la pili ambalo linanisumbua mimi. Tumekuwa tunashauri humu ndani kwamba ni muhimu sana kupanua wigo wa kodi. Mimi nimetoka katika sekta ya ulinzi binafsi na kule kuna hali nzuri sana ya kukusanya kodi, lakini kampuni zile karibu 1,200 sasa hakuna *GN* wala sheria ya kuiziongoza. Kwa hiyo, zinajiendea tu. Tumejaribu kuzikusanya huku na huku sisi wenyewe tumekusanyana na kuanzisha sekta ya ulinzi binafsi. Chama chetu kinaitwa *Tanzania Security Association* lakini ni vigumu sana kusema wanalipaje kodi?

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tunagombania kodi. Nilileta Muswada Binafsi hapa mwaka 2017, na Muswada ule ulinigharimu sana kwenda nchi za nje kutafuta *input* za Muswada ule. Nilipouleta hapa, Muswada ulipelekwa Bungeni kwa Katibu wa Bunge, lakini Mheshimiwa Spika na wataalamu wote wa Bunge wakapitia Muswada ule wakasema unafaa, Serikali ikauchukua ikasema itauleta hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutumia Kanuni ya 94 ambayo inaruhusu Mbunge kuleta Muswada Binafsi Bungeni, na kanuni hizi ndiyo zinatulinda sisi hapa tuweze kufanya kazi kama Wabunge, mpaka leo Serikali haijaleta Muswada huu. Licha ya kuahidi na kuuliza maswali ya kibunge, lakini Muswada huu utasaidia kodi, utasaidia mapato ya Serikali, utaanzisha mamlaka kama vile *EWURA,* mamlaka kama vile ya kusimamia sekta hii ya ulinzi binafsi ifanye vizuri. Tangu mwaka 1980 zikiwa kampuni mbili, zimekua mpaka kuwa kampuni 1,200, lakini hakuna sheria, hakuna kanuni, wala miongozo ya kampuni hizi. Serikali inapoteza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulisema juzi juzi hapa, tozo, tozo! Leo tozo tunafaidika, tunajenga barabara, tunajenga

shule na kadhalika. Tozo au kodi itakayotokana na uendeshaji bora wa kampuni za ulinzi zitafaidisha wananchi na zitafaidisha Serikali. Kwa hiyo, nilikuwa naomba, ili kuweza kupanua wigo wa kodi, basi Serikali ilete ule Muswada wa Sheria ya Sekta ya Ulinzi Binafsi hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu waajiri; kumekuwa na matatizo sana huko kwa waajiri, lakini mjue waajiri tumefanya kazi kubwa sana ya kuzuia migomo hapa nchini, kwa kuongea vizuri na wenzetu wa *TUCTA* na wafanyakazi wenzetu. Sisi tunalalamika; nina maana waajiri wanalalamika, sheria ile ya Na. 6 ya Mwaka 2004 imepitwa na wakati, inatakiwa ifanyiwe mabadiliko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baraza linasaidia kutunga sheria za kazi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Maige, kengele ya pili.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Chaya, jiandae Mheshimiwa Mpina.

Kabla ya Mheshimiwa Dkt. Chaya, naomba kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge na watumishi wa Bunge kwamba leo *CRDB* imeandaa hafla ya Iftar kwa ajili ya Waheshimiwa Wabunge na watumishi wa Bunge. Hafla hiyo itafanyika katika viwanja vya Bunge leo siku ya Jumanne, tarehe 11, 2023 kuanzia saa 12:30 jioni. Mgeni Rasmi atakuwa Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Mbunge, Spika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Waheshimiwa Wabunge na

watumishi wote wanaalikwa katika Iftar hiyo ambayo pia itahudhuriwa na viongozi wa dini wa Mkoa pamoja na viongozi wengine wa Serikali.

Mheshimiwa Dkt. Chaya.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nakushukuru kwa kunipa hii nafasi. Kipekee namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya. Sisi katika Jimbo letu la Manyoni Mashariki kuna kazi nyingi sana zimeshafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu la Manyoni Mashariki tumepata fedha nyingi sana. Tumepata shilingi bilioni nne kwa ajili ya ujenzi wa shule ya wasichana ya Mkoa; tumepata shilingi bilioni 1.4 kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha *VETA;* tumepata shilingi bilioni 12 kwa ajili ya mradi wa maji wa Kintinku Msilile; na pia tulipata shilingi bilioni 1.7 tukajenga shule tano mpya za sekondari. Haya ni mafanikio makubwa sana. Nasi watu wa Manyoni kwa kweli hatujawahi kupata fedha nyingi hizi huko nyuma, kwa hiyo, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais na tunamtia moyo aendelee kuchapa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze sana Waziri Mkuu na timu yake; Mheshimiwa Prof. Ndalichako na mama yangu pale, wanafanya kazi kubwa sana. Wanaitendea haki sana Wizara ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi leo nachangia upande wa ajira, lakini nataka nioneshe uhusiano uliopo kati ya ajira na ile taasisi yetu ya *TAESA (Tanzania Employment Service Agency)*. Mheshimiwa Hasunga ameeleza hapa kwamba, tatizo la ajira Tanzania bado linaendelea kukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikwambie, *it is a time bomb.* Ni bomu! Kwa sababu gani? Kwa mwaka, takwimu

zinatuonesha, tunatoa vijana takribani 800,000 hadi 1,000,000 wanaingia kwenye soko la ajira, lakini ni chini ya asilimia 20 ya vijana wanapata ajira. Hili ni tatizo kubwa sana. Mimi nimefundisha katika taasisi za elimu ya juu, nina vijana ambao wamekaa zaidi ya miaka 10 tangu wamalize hawajapata ajira, wapo mtaani. Hili ni tatizo kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulianzisha *TAESA* 2002. Lengo la *TAESA* lilikuwa kuratibu ajira, lakini tujiulize, wangapi wanaijua *TAESA?* Je, *TAESA* ina *capacity* ya kuratibu tatizo la ajira? Vile vile tulianzisha *TAESA* ili iweze kuwa-*connect* wanaotafuta kazi na waajiri kwenye sekta binafsi na sekta ya umma. Je, haya yanafanyika?

Mheshimiwa Naibu Spika, *TAESA* iko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Mwaka 2016 walianzisha *program* ya mafunzo ya kazi kwa vijana wanaomaliza vyuo vikuu, inaitwa *internship program;* lakini mwaka 2017 Ofisi ya Waziri Mkuu ilianzisha Mwongozo wa Mafunzo ya Kazi kwa Vijana Wanaomaliza Vyuo Vikuu *(National Internship Guideline)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna Mwongozo, lakini leo hii umewasikia Wabunge wengi wakisema, huko kwenye Halmashauri zetu kuna vijana wanachukuliwa wanajitolea, wanalipwa kiasi ambacho hakipo kwenye mwongozo. Nini maana ya kuanzisha huu Mwongozo ambao uko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, ambapo tulitegemea utasaidia kuhakikisha kwamba, unaratibu suala la kutumia hata hawa vijana kwa *part time,* na vilevile kuhakikisha kwamba taasisi zote za umma na sekta binafsi wanatumia huo Mwongozo kwa ajili ya kuwasaidia vijana wetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, *program* ya kuwapa mafunzo vijana waliohitimu vyuo vikuu hadi sasa takwimu nilizonazo, imefikia vijana zaidi ya 13,000. Hao vijana wanaingia mkataba wa miezi sita hadi 12, wanalipwa 150,000/= kwa mwezi. Maana yake ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa hivi takribani shilingi bilioni 18 zimetumika kwa ajili ya hii programu. Swali langu linakuja, kuna uhusiano gani kati ya *TAESA* na Sekretarieti ya Ajira? Kuna uhusiano gani uliopo kati ya *TAESA* ambayo inawatafutia vijana ajira na Sekretarieti ya Ajira? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekretarieti ya Ajira imejikita kwenye ajira za umma. Sasa swali langu linakuja? Je, wale vijana ambao *TAESA* imewapa mafunzo, ni jinsi gani inaratibu kuhakikisha kwamba wale vijana wanaotoka *TAESA* inawapeleka kwenye Sekretarieti ya Ajira ili waweze kupata ile ajira?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo. Hakuna *link* iliyopo kati ya *TAESA* na Sekretarieti ya Ajira. Hawa ni watoto wa baba mmoja na mama tofauti. Nilitegemea kwa sababu, *TAESA* ime-*invest* hela nyingi sana kuwajengea uwezo hawa vijana, nilitegemea zinapotoka ajira za Sekretarieti ya Ajira, kipaumbele kiwe kwa wale vijana waliotoka *TAESA*. Leo nikimwuliza Mheshimiwa Waziri aniambie ni vijana wangapi waliopata mafunzo ya *TAESA*, walipata ajira za Sekretarieti ya Ajira, inawezekana wakawa wachache sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo na kwa kweli, tunahitaji kulifanyia kazi. Tukiangalia katika nchi za wenzetu, kwa mfano Kenya. Kenya wana *TAESA* kama ya kwetu, lakini wenzetu walichofanya wameanzisha kitu kinaitwa *National Employment Authority*. Ukiangalia majukumu yake ni tofauti sana na ya kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TAESA* yetu haina meno. Tunategemea *TAESA* yenye meno ambayo itasaidia vijana wetu kupata ajira. Siyo lazima ajira ya Serikalini, lakini iweze ku-*connect* vijana wetu na ajira mbalimbali; iwatafutie ajira; iwajengee uwezo; na mambo mengine, lakini bado tuna tatizo kubwa sana kwenye suala la ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa Serikali, kama nilivyotangulia kusema, tatizo la ajira bado ni kubwa sana. Kweli tunasema vijana wajiajiri, lakini mzazi anapopeleka mtoto shule, chuo, anategemea yule mtoto aje awe afisa; hayo ndiyo mategemeo ya kila mtu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ushauri wangu ni nini? Kwanza, tunahitaji kupitia upya *TaESA,* tuipe nguvu ya kifedha, tunahitaji tufikie vijana wengi. Tuone uhusiano uliopo kati ya *TaESA* na Sekretarieti ya Ajira. Wale vijana ambao wamekuwa *groomed* na *TaESA* tunategemea wachukuliwe na Sekretarieti ya ajira; hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, hizi taarifa za hizi nafasi za *internship* tunahitaji ziwe za uwazi. Vijana wote wa Kitanzania wapate. Nilitegemea kusikia vijana wangu wanaotoka Manyoni vilevile wamenufaika na huu mradi wa *TaESA,* lakini nikiuliza inawezekana nisiwapate.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, nilitegemea kuona kuna kanzidata *(database)* ya kuhakikisha kwamba vijana wote wanaomaliza vyuo vikuu wanajiunga kwenye ile kanzidata ambayo itakuwa chini ya *TaESA* ili iwe rahisi *TaESA* wenyewe kuratibu masuala ya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudie kuishukuru sana Serikali, hususan Mheshimiwa Rais, kwa kazi kubwa mnayoifanya, sisi Manyoni ametupa miradi mingi sana. baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja; ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi uliyonipa na nianze kabisa mwanzo niwaombe kabisa Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Naibu Spika kwamba Bunge hili tusikubali kutumika kama

mahali pa kuhalalisha wahalifu na wabadhirifu wa fedha za umma, na kwamba la kuvunda halina ubani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuwashukuru sana na kuwapongeza sana mamlaka za ukaguzi pamoja na za uchunguzi, *CAG, CPA* Charles Kichere pamoja na *CP* Salum Hamdun, Mkurugenzi wa TAKUKURU, kwa kazi nzuri sana waliyoifanya ya ukaguzi wa fedha za umma mwaka huu. Taarifa zao walizozitoa pamoja na watendaji wao kule ofisini ni kielekezo kikubwa sana cha uzalendo wa Taifa lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana kipekee Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kukataa katakata nchi yake kugeuzwa kuwa shamba la bibi. Na mimi nasema Mawaziri waliohusika, watendaji wote wa Serikali waliohusika mapema iwezekanavyo wakamatwe, washtakiwe na wafunguliwe makosa ya uhujumu uchumi wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii tunajadili hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuna mambo mawili tu ya kiujumla ninayotaka kuyasema; moja bajeti ya maendeleo tuliyopanga mwaka huu wa fedha, katika mpango wetu wa miaka mitano tulipanga iwe asilimia 37.1 lakini mpango wa maendeleo uliowasilishwa na Serikali, fedha za maendeleo ni asilimia 34.1 tu; nini kilichosababisha mpango wetu kushuka, nini kilichosababisha fedha za maendeleo kushuka tofauti na mpango wa maendeleo tuliouweka wa miaka mitano?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni suala zima la Katiba; nimesoma mpango wa maendeleo na ukomo wa bajeti sijaliona suala hili; nimesoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu sijaliona suala hili, na suala hili Mheshimiwa Rais amelisisitiza sana, sikutegemea nilikose kwenye hotuba kubwa ya Mheshimiwa Waziri Mkuu au kwenye taarifa kubwa ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ikija Serikali hapa itueleze hili suala likoje, licha ya Mheshimiwa Rais wetu kulisema kwa msisitizo mkubwa kwamba ni lazima tufanye mabadiliko katika Katiba yetu na ikiwezekana tupate Katiba mpya inayohitajika kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tatu ni suala la vihatarishi au changamoto mahususi katika utekelezaji wa bajeti tunayoizungumza leo. Ukipitisha bajeti kukiwa na vihatarishi vingi ambavyo vinaashiria kwamba mpango wa bajeti tunaoupitisha unakwenda kukwamba tu, ni lazima ujishirikishe, ufanye tathmini ya kutosha juu ya tahadhari hizo, juu ya changamoto hizo, ufanye tathmini ya kina, uone ni namna gani unakwenda kuzitatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa Serikali kupitia mpango wa maendeleo ukurasa wa 89 kipengele cha 2.4.2 inakiri wazi kwamba kuna vihatarishi vingi vinavyopinga utekelezaji wa bajeti. Kwa kifupi tu kwamba kuna upungufu mkubwa wa rasilimali watu, kuchelewa kukamilisha taratibu za utoaji cheti cha msamaha wa kodi, usanifu duni, usimamizi usioridhisha katika utekelezaji wa miradi kwa mujibu wa mikataba na mipango kazi kwa baadhi ya watekelezaji wa miradi, kucheleshwa kwa malipo ya wakandarasi na sababu nyingine nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi sababu inasema Serikali yenyewe kwamba hizi ni changamoto. Moja, maana yake Waziri Mkuu atuambie kwamba Serikali imeshindwa kuzidhibiti hizi sababu? Lakini la pili; tunashindwaje kutoka pale? Na ukienda sasa kuzichambua hizi hoja ndizo hizi ambazo zinaturudisha nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakaa hapa, tutaidhinisha bajeti ambayo mwisho wa siku inakwenda kutafunwa na watu wachache. Tunarudi hapa tena unatupa tena jukumu

la kupitia bajeti inakwenda kuliwa na watu wachache. Ni lazima hizi nyufa tuzizibe leo. Tunapopitisha bajeti na nyufa zenyewe tumeziziba ili fedha za wananchi zisiende kuliwa tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, kushindwa kutekeleza mpango wa manunuzi ni jambo ambalo kwenye mpango wa maendeleo wamesema wao wenyewe Serikali na hapa imetokea, na *CAG* amelisema. Jumla ya trilioni 3.14 hazikutumika, zikiwemo fedha tulizozituma kwenda *TANROADS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania mwaka 2021/2022 waliahidiwa kujengewa barabara zao zaidi ya trilioni 2.9 za *TANROADS* hazikwenda kufanya kazi, hakuna mradi ulikuwa *implemented.* Leo tena tunarudi hapa kupitisha bajeti halafu pesa zikawekwe, Watanzania waendelee kuteseka bila kupata maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kutokufuata Sheria ya Manunuzi. Tunajua tunapitisha bajeti hapa, mwisho wa siku hizi pesa zinakwenda kutekeleza miradi ya maendeleo kupitia Sheria ya Manunuzi, halafu sheria hiyo inakiukwa kila leo, halafu tunaletewa tena bajeti inakiukwa na fedha za wananchi ziliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisimama hapa kwenye Bunge lako tukufu nikazungumzia juu la *Lot No. 6,* mradi wa *SGR* kutoka Tabora kwenda Kigoma kwamba *TRC* imeacha bei ya ushindani kwa kilometa moja ya *standard gauge* ya bilioni 9.1 imekwenda kumpa mkandarasi *CCECC* kwa bilioni 12.5, zaidi ya bilioni 3.4 kwa kilometa na kuisababisha Serikali hasara ya trilioni 1.7. Mkataba huu bado unaendelea, tusipofanya *intervention* utaendelea. Nchi imekula hasara ya bilioni 1.7.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Lot 3* na *Lot 4* mkaguzi ame-*confirm* kwamba tumepunjwa trilioni 1.7; lakini pia na ununuzi wa mabehewa bilioni 503; jumla trilioni nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi fedha ni za Watanzania, Waziri wa Fedha alikwenda kukopa hizi fedha kwa sharti la kuvunja Sheria ya Manunuzi ambayo hana uwezo huo, hana uwezo huo mkubwa wa kisheria, hana uwezo mkubwa huo wa Kikatiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa hivi Waziri wa Fedha, Waziri wa Uchukuzi na Mkurugenzi wa *TRC* kwa nini hawajakamatwa na kufunguliwa makosa ya uhujumu uchumi mpaka sasa hivi wako hapa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, tusicheke, shilingi trilioni nne za Watanzania zinakwenda kupotea kwenye mradi huu. Hata kama tungeenda kukopa mkopo sijui wa riba ngapi, tunalipa fedha kidogo sana katika mambo mengine haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hizo dakika tatu zilizobaki, nizungumzie mambo mawili ya mwisho; kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere hapa na kwenyewe tulisema sana hapa Bungeni ikiwemo mimi, kwamba jamani hawa watu tunawadai fedha zetu, kwa nini hawalipi? Majibu ambayo yanatolewa na Waziri wa Nishati hayaeleweki, kila leo tukiuliza hapa Bungeni. Mkaguzi amekwenda ku-*confirm* tunawadai bilioni 327 kwa mwaka mmoja wa 2022. Mwaka 2023 tunadai zingine, kwa hiyo ni jumla ya bilioni 655. Ukijumlisha na zile za *CSR* ni bilioni 270; jumla ni bilioni 926 tunazowadai. Na mkataba unakaribia kwenda mwisho, lakini fedha hizi hazidaiwi na hawa watu, Waziri wa Nishati yupo, Mkurugenzi wa *TANESCO* yupo, hawadai fedha hizi na bado wapo kwenye ofisi za Serikali. Mamlaka zinazotakiwa kuchukua hatua ziko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho; leo tulikuwa tunalalamika hapa sisi tunawezaje kupitisha Bajeti, halafu mtu mwingine anakwenda kutumia matumizi nje ya bajeti, mtu mwingine anakwenda kukopa mikopo zaidi ya fedha tulizoidhinisha hapa. Kwa hiyo, fedha alizokopa hatujaidhinisha, matumizi ya hizo fedha zinakwenda kutumika kwenye nini, hatujaidhinisha. Leo mkaguzi amekwenda ku-*confirm,* mwaka wa 2021/2022 Waziri wa Fedha amekwenda kukopa trilioni 1.285 bila ridhaa ya Bunge, bila ridhaa ya mtu yeyote, fedha za Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatujui hizo trilioni 1.285 zimekwenda kufanya nini, hatujui alizikopa akazipeleka wapi, mpaka sasa hivi na jambo hili linaendelea kutunzwa kwa usiri mkubwa. Mambo haya inawezekanaje yakafanyika hivyo yanavyofanyika?

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa tunawadai *IPTL* bilioni 342, fedha hizi tulishashinda kesi kihalali toka tarehe 1 Machi, 2021; kazi ni *TANESCO* na Waziri wa Nishati kwenda kuzidai, imeshindikana. Wanashindwa nini kwenda kudai; wana ubia gani na huyu *IPTL,* wananufaika nini na huyu *IPTL* fedha za Watanzania? Na kama jambo hilo limewashibda si wawaachie Watanzania wengine wazalendo ambao wanaweza kuzipigania fedha za Watanzania. Watanzania wanyonge hawa ambao wanateseka kwa kodi zinazowaumiza kila leo, fedha zao wanazoweza kuzichukua, ambazo zipo kwa mujibu wa sheria hazidaiwi na watu ambao walishapewa dhamana ya kuziomba. *(Makofi)*

*Mheshimiwa Naibu Spika, kwa summary tu hapa, ubadhirifu wote huu wa CAG ambao mimi nimeainisha na bado naendelea kuainisha ni zaidi ya trilioni 30. Sasa ukishakuwa na ubadhirifu wa trilioni 30 unakaa kwenye bajeti kufanya nini? Yaani unazipitisha hela zote zikagawanywe? Na hapa lazima tuchukue hatua kali dhidi ya watu hawa wanaofanya haya mambo. Kama Bunge lako litashindwa*

*kuchukua hatua katika hili, basi hili Bunge liwajibike…* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mpina, muda wako umekwisha. Na Waheshimiwa Wabunge, tuelewe utaratibu ulivyo ni kwa Serikali na muda wa kujibu hoja zote hizi na wataleta kwenye Kamati ya *PAC* watakaa na tutatapa majibu sahihi.

Mheshimiwa Profesa Mkumbo, wajiandae Mheshimiwa Kandege na Mheshimiwa Mwanakhamis Said.

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, uongozi mpya siku zote ni fursa na sisi tuna fursa hapa ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan na fursa imejitokeza. Nakumbuka maono yake yameshatolewa katika maeneo makubwa mawili, kwanza katika hotuba ambayo ilitolewa hapa Bungeni mwaka 2021, ya pili ni kwenye Makala ambayo aliiandika tarehe 01, Julai, 2022. Makala ambayo alikuwa anaakisi miaka 30 ya mfumo wa demokrasia ya vyama vingi nchini ambapo aliibuka, nataka kunukuu hapa, alieleza kuwa: - "*Ndiyo sababu kwenye uongozi wangu ninaamini katika kile kinachojulikana kama 4R – ikiwa ni ufupisho wa maneno manne ya Lugha ya Kiingereza; Reconciliation (Maridhiano), Resilience (Ustahamilivu), Reforms (Mabadiliko) na Rebuilding (Kujenga Upya)*" mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yangu kwamba wenzetu Serikalini, Mawaziri, watakapoleta bajeti zao hapa tutaona jinsi ambavyo wametafsiri ndoto hii ya Mheshimiwa Rais kupitia mipango na bajeti ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa leo nataka nizungumzie eneo moja katika hizo *4R, R* ya tatu ambayo ni *reforms* (mabadiliko). Na Mheshimiwa Rais alisema kuwa nimedhamiria kwamba kwenye kuenzi miaka yetu ya demokrasia ya vyama vingi, Serikali yangu itajitahidi kufanya mabadiliko katika mifumo ya kisiasa, kiuchumi na katika sheria. Lengo ni kwamba Tanzania yetu iende na wakati" mwisho wa kunukuu

Mheshimiwa Naibu Spika, Katiba yetu Ibara ya 6 inatambua Serikali tatu, aina tatu za Serikali katika nchi hii; Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali za Mitaa. Hizi ndizo aina tatu za Serikali. Na zote zina Rais wake; Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yupo, Rais wa SMZ yupo na Rais wa Serikali za Mitaa bahati nzuri ni huyohuyo wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tumeweka sheria mbalimbali kwenye kutafsiri maono haya ya Katiba; Sheria ya Serikali za Mitaa tunafahamu Sura Na. 287 na 288 kwa maana ya wilaya na miji. Tumeweka sera ya ugatuaji, na sera hii tumekuwa tukiitekeleza tangu mwaka 1998. Ililenga kuhamisha na kupeleka madaraka katika maeneo makubwa mawili, kutoka Serikali kuu kwenda ngazi ya halmashauri za wilaya, miji, manispaa na majiji. Pili, kutoka ngazi ya halmashauri kwenda kwenye ngazi za msingi za kata, mitaa, vijiji na vitongoji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma hii inazungumzia *vertical decentralization,* haizungumzii *horizontal decentralization.* Lakini sisi kwenye tafsiri yetu, tulichofanya tuka-*decentralize* kutoka Wizara ya Maji, kutoka Wizara ya Elimu kwenda Ofisi ya Rais, TAMISEMI ambayo bado ni *central.* Kwa kutumia falsafa ya Mheshimiwa Rais ya *reform* lazima tuliangalie upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *decentralization* ilikwamia sehemu haijafika mwisho, na ndiyo maana wakurugenzi kila kukicha safari zao kutoka Ubungo, kutoka Songea kuja Dodoma. Wako wapi; kwenye kikao Dodoma, kwa sababu Mamlaka za Serikali za Mitaa hazifanyi kazi yake sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye sheria tumeweka vyombo vitatu vya kutekeleza hili. Cha kwanza tumesema Baraza la Madiwani ndicho chombo cha juu cha maamuzi katika halmashaui. Sasa Waheshimiwa Madiwani wenzangu mliopo hapa niwaulize; hivi kweli Baraza la Madiwani katika halmashauri zetu ndicho chombo cha juu cha maamuzi? Ndivyo ilivyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesema ya pili Kamati ya Maendeleo ya Kata *(Ward Development Committee)* ndicho chombo cha maamuzi katika ngazi ya kata ambapo Mwenyekiti wake ni Diwani. Na mwisho tumesema Mwenyekiti wa Kijiji/Mtaa ndiye kiongozi na Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo, sheria na sera zipo vizuri sana, tunahitaji *reform* kuhakikisha kwamba sera hizi zinafanya kazi sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka nipendekeze maeneo matatu ya *reform;* kwanza tuna changamoto ya kwanza kati ya viongozi wachaguliwa, wateule na waajiriwa. Tukienda kwenye uchaguzi tunachagua viongozi watatu; tunamchagua Rais, Mbunge na Diwani. Inapokuja kwenye utekelezaji wa majukumu, Rais ni msimamizi wa shughuli za Serikali katika Serikali Kuu na kwa vitendo anaonekana hivyo, lakini Diwani ambaye ni msimamizi katika kata yuko wapi? Hili ni eneo la *reform* ambalo lazima tuliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili; Madiwani kisheria tumewapa jukumu la usimamizi wa programu za maendeleo katika ngazi ya kata. Kisheria ndio wakuu katika shughuli zetu za maendeleo. Tukawaongezea pia jukumu la kusimamia ukusanyaji wa mapato katika kata zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Madiwani ni *part time workers*. Umewahi kuona wapi duniani mtu umekabidhi jukumu la usimamizi halafu ni *part time?* Hili ni eneo ambalo lazima tuliangalie, linahitaji *reform. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenyekiti wa Kijiji ambaye ndio kiongozi na mkuu wa Serikali, huyu naye ni *parttime,* lakini kwenye kata tukaenda tukarundika. Nilikuwa naangalia muundo wa kata moja pale Dar es Salaam, ofisi ya kata moja ina watumishi 16, watawala saba, afya wawili, elimu wawili, maendeleo ya jamii mmoja, afisa ustawi wa jamii mmoja, kilimo mmoja, mifugo mmoja, uvuvi mmoja. Dar es Salaam afisa uvuvi kwenye kata anafanya nini? Dar es Salaam afisa mifugo kwenye kata anafanya nini? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji *reform,* hawa watu wapunguzwe ili mshahara unaotokana na hawa tumpe Diwani awe *fulltime worker. (Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama tupo *serious* na *local government authority*, Madiwani ni muhimu wawe wafanyakazi wa kudumu wawe *salary*, wapewe mishahara, kwa sababu hawa, sisi angalau kwenye Bunge ni wakutoa ushauri. Diwani sio wa kutoa ushauri ni msimamizi inakuaje msimamizi asiwe mfanyakazi wa kudumu? Tunahitaji eneo hili lifanyiwe *reform*...

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimwia Naibu Spika Taarifa.

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO:** Vivyo hivyo mkuu wa Serikali ya Kijiji na mtaa. Mkuu wa Serikali ya Mtaa unamfanyaje kuwa *part-time*?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Taarifa Mheshimiwa Naibu Spika

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO:** Huyu naye lazima tufanye *rationalization* ili kwamba huyu naye awe ni sehemu ya utumishi katika eneo lake.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kitila kuna taarifa.

**T A A R I F A**

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika,naomba nimpe taarifa mazungumzaji Profesa Mkumbo; najua ni mwanafunzi mzuri sana wa *decentralization* na nimewahi ku-*share* naye kwamba *decentralization*…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa twende kwenye taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa nimpe taarifa tu kwamba kwa mfumo wa ugatuaji wa Serikali za mitaa nchini hauiondoi Serikali za mitaa kwenye *unitary government*. Pamoja na kuwa kuna hayo mamlaka ambayo tumewapa hawa madiwani lakini mfumo hautoi madiwani kuwa na *workforce* ya kumwezesha kutekeleza majukumu ambayo anajaribu kuyazungumza. Ndiyo maana kwenye ngazi hiyo wameweka wataalam wa kada mbalimbali kama ilivyo kwenye Wizara, Waziri ni mmoja, Naibu ni mmoja lakini kuna katibu mkuu na watendaji tofauti wa kumsaidia ku *discharge* majukumu ya Serikali kwenye ngazi ile hautegemei majukumu yale afanye mwanasiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

**NAIBU SPIKA**: Ahsante, Mheshimiwa Mkumbo.

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO**: Mheshimiwa Naibu Spika, Siipokei hiyo taarifa kwa sababu inakinzana na hoja yangu, kwa hiyo sipokei hata kidogo. Lakini hoja ya msingi ameipata, mimi ni mwanafunzi wake mzuri wa *local government,* sasa amenifundisha mwenyewe halafu ananipinga, haiwezekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya msingi ni kwamba wale watu ambao wanafanya kazi za kila siku za kusimamia maendeleo yetu ili tuone *impact* kwenye *government reform* ni muhimu sana wakapewa majukumu yao na yaendane na hadhi yao, wapewe wafanye kazi zao za msingi ikiwemo utumishi wa kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho na mimi nichukue nafasi hii kumpongeza sana kwa mkitadha huu Mheshimiwa Rais kwa kuja na haya mambo manne *(4R)* na kwakweli Waheshimiwa Wabunge sisi tunajukumu la kutafsiri hizi *4R* za Mheshimiwa Rais hapa ndani na katika utendaji wa Serikali. Mwisho nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa jinsi anavyomsaidia Mheshimiwa Rais kwenye kusimamia shughuli za maendeleo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, kengele ya pili.

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kandege…

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Kiti.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Chief Whip* Mwongozo.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, ninaomba kupata Mwongozo kidogo tu, hivi punde nimemsikiliza Mheshimiwa Mpina alivyokuwa akichangia hapa ndani na alimaliza hoja yake kwa kutangaza kwamba ubadhirifu ambao umekwisha kuibuliwa ambao unaihusu Serikali unafika karibu trilioni 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina tatizo na ripoti ya *CAG,* lakini nataka *clarity* na hasa kuondoa taharuki ambayo inaweza ikaibuka kuanzia siku ya leo baada ya tamko hili.

Kwa mujibu wa Kanuni za Bunge na kwa mujibu wa Katiba na utaratibu wa uendeshaji wa shughuli za Bunge na hasa mjadala na ufuatiliaji wa hoja ambazo zimeibuliwa na Mkaguzi Mkuu wa Serikali zitahitimishwa pale ambapo ratiba nzima ya utaratibu itakuwa pia imehitimishwa na hapo tunaweza tukajua kwa kina kabisa ni kwa kiasi gani Mkaguzi Mkuu wa Serikali ameweza kutusaidia ndani ya Serikali na Taifa kwa ujumla kujua ubadhirifu huu umeweza kufika kiasi kipi.

Sasa nilikuwa naomba tu Mwongozo wako kama ni sawasawa kuanza kutamka mawanda makubwa ya fedha ambazo zimetamkwa kwamba zimetumika ndivyo sivyo kabla mchakato huo mzima na utaratibu bado haujakamilika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jenista nakubaliana na hoja yako kuwa muda wa kujadili kwa undani kabisa ripoti ya *CAG* ni bado na Serikali imepewa muda wa siku 21 kwenda kujibu kwenye Kamati ya *PAC* ambapo *CAG* na timu yake na timu ya Serikali watahojiwa na Kamati ya *PAC* kwa mujibu wa utaratibu wa sheria na kanuni za Bunge na Katiba ili kupata uhakika wa ripoti na jicho la *CAG,* kwa maana hiyo maneno hayo aliyosema Mheshimiwa Mpina yanaondolewa kwenye

*Hansard* mpaka hapo Serikali na *CAG* na Kamati ya Bunge watakapo kaa na kuja na ripoti ikiletwa rasmi Bungeni na kujadiliwa na Bunge.

Mheshimiwa Kandege.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi jioni ya leo niwe miongozni mwa wachangiaji wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane na wenzangu ambao kwa dhati kabisa wamepongeza kazi iliyotukuka inayofanywa na Mheshimiwa Rais katika kuhakikisha kwamba Taifa hili linasonga mbele. Sisi wananchi wa Kalambo hatuna la kumlipa zaidi ya kumwombea kwa Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo machache ambayo nitataja, mimi leo nawiwa kutaja kwenye upande wa barabara. Kwa sisi wananchi wa Kalambo tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais tumeweza kupata jumla ya shilingi bilioni 37 kwa ajili ya kujenga barabara kutoka Matai kwenda Kasesha *Border* kilometa 25 na kilometa zingine 25 ziko kwenye mchakato wa manunuzi. Ni imani yetu kubwa kwamba akipata fursa ya kuja Mkoani Rukwa atapita Kalambo na kutuwekea jiwe la Msingi kama sio kufungua barabara hii. Barabara hii ni kiunganisho kikubwa sana kutoka nchi ya Zambia lakini pia itapunguza umbali mrefu ambao wasafiri wanalazimika kusafiri kutoka maeneo ya Mwanza, Uganda, Kenya kuzunguka kwenda Tunduma kwa kuwa sasa watapunguza zaidi ya kilometa 600, hivyo tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama hiyo haitoshi kuna daraja letu ambalo kwa muda mrefu tulilipigia kelele. Safari hii tumeweza kupata jumla ya Shilingi isiyopungua bilioni tano,

sasa litajengwa. Daraja hili ni kiungo kikubwa sana kwa barabara ya zamani inayojulikana kama Barabara ya Mjerumani ambayo inaenda Bismark Kasanga.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupongeza hayo naomba pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na niunge mkono hoja ambayo imewasilishwa. Pia niweze kumkumbusha Mheshimiwa Waziri Mkuu, alipokuwa amekuja Kalambo mwaka 2020, akiwa Kasanga pale aliwaahidi wananchi wa Kasanga na Tarafa ya Kasanga ujenzi wa kituo cha afya. Wamenituma nije nimkumbushe kwa sababu kwa muungwana ahadi huwa ni deni. Naamini katika majumuisho atalisema na hilo ili tuweze kujua lini ujenzi unaanza maana eneo la kujenga tayari tumeshaliandaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza maneno hayo naomba nichangie katika maeneo yafuatayo. Muda ukiruhusu nitachangia kuhusiana na mfuko wa dharula kwa maana ya *contingency fund*.

Mheshimiwa Spika, nitachangia kuhusiana na mgawanyo wa rasilimali watu kwa watumishi wa umma, utaratibu wa shughuli za Serikali na kodi ya majengo kwa maana ya *property tax* na usimamizi wa mifumo ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na mfuko wa dharula *(Contingency Fund)*. Uanzishwaji wa mfuko wa dharula kwa Taifa ni takwa la kikatiba ibara ya 140(i)a. Na kama hiyo haitoshi inaenda kukaziwa na Sheria ya bajeti ya mwaka 2015 kifungu cha 22.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Taifa, sheria ya bajeti inataka asilimia moja ya bajeti kila mwaka itengwe kwa ajili ya kupelekwa kwenye mfuko wa dharula.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakubaliana, kama Taifa tumekuwa tukiona nchi majirani, hivi juzi ilitokea nchi ya Malawi, wakapatwa na ile dhoruba, sisi kama Taifa tunawajibu wa kuhakikisha kwamba mfuko huu unaanzishwa; na bahati nzuri unatakiwa kusimamiwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Tumekuwa tukishuhudia yakitokea maafa, fungu linalotumika ni Fungu 21 hazina ambapo kwa mujibu wa Sheria ambayo ipo kwa mujibu wa Katiba na Sheria ya Bajeti sio sahihi kuendelea kutumia Fungu 21. Ni wakati mwafaka kama Taifa tuhakikishe kwamba mfuko wa dharura unakuwepo na unafanya kazi iliyokusudiwa kwa mujibu wa Katiba. Katika hali ya kawaida hakuna familia yoyote ambayo inaweza ikajidai pale ambapo hawana hata akiba likitokea lolote la kutokea unaanza kukimbilia kwenda kwa majirani. Ni wakati mwafaka tutekeleze takwa la katiba na takwa la kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini eneo lingine ambalo naomba nichangie ni ukusanyaji wa kodi ya majengo *(property tax)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, na wewe ni shuhuda ukirejea siku za nyuma halmashauri na hasa hata halmshauri yako ya Ilala ilikuwa inaonekana inakusanya vizuri zaidi kulikoni utaratibu uliokuja kuanzishwa ambao mpaka leo tunashindwa kupata uhakika hayo makusanyo ili tulinganishe na vile ambavyo halmashauri zetu zilikuwa zikikusanya. Umekuja utaratibu wa kutumia Luku lakini nayo imekuwa ni changamoto. Ni wakati mwafaka Serikali, na hasa baada ya kuendesha zoezi zuri la sensa tuna uhakika kwamba kila mwenye mali kama ni nyumba anajulikana kwa mujibu wa sensa iliyofanyika. Sasa, ni wakati mwafaka kwa Serikali kuhakikisha kwamba sensa na takwimu zake zitusaidie ili kuwezesha kukusanya mapato yake halali kuhusiana na *property tax*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni eneo ambalo lina fedha nyingi sana. Tukilisimamia hakika maendeleo ambayo Mheshimiwa Rais anapigana nayo kila siku tutamrahisishia kazi kwa sababu eneo hili ni eneo oevu. Linachukua muda mrefu, ukiuliza *TANESCO* hawana *interest* na makusanyo hayo kwa sababu si fedha ambayo inaingia kwao; lakini hata halmashauri nazo wanajiweka nyuma kwa sababu hawaoni manufaa yake; halikadhalika na Serikali kuu. Mfumo ambao ni rasmi wa kuhakikisha kwamba *property tax* inakusanywa na ikagawanywa kwa ajili ya maendeleo haifanyiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni imani yangu kubwa kwamba wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu anakuja kuhitimisha atatuambia wamefikia wapi ili tuwe na mfumo mahsusi wa kuhakikisha kwamba kodi hii inaenda kukusanywa ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala zima la mgawanyo wa rasilimali watu kwa watumishi wa umma; amelisema vizuri sana Profesa Kitila. Hata hivyo, ukitafuta idadi ya wafanyakazi wa Serikali au wa umma hutashangaa kukuta baadhi ya halmashauri wapo wengi lakini ukienda maeneo mengine hawapo. Sasa Dar Es Salaam Kinondoni unamweka Afisa Kilimo wa kazi gani badala ya kumpeleka Kalambo ambapo wakulima wanamuitaji? Ni wakati mwafaka wa Serikali kufanya *human resource audit* ili kujua kabla ya kuanza kuajili tunao watumishi wangapi ndani ya Serikali na tunawatumiaje ili *effect* yake iweze kuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, na ni ukweli usiopingika, unakuta maeneo ambayo wapo watumishi wengi wazuri hata maandiko yao wakiandika wakati wa kupitisha *project* wanafanikiwa; lakini maeneo mengine wanakuwepo wachache hata namna ya kuweza kuandika hata *project* hawezi kufanikiwa. Ni wakati mwafaka Serikali mtujie na utaratibu wa kuhakikisha kwamba utakuwepo mgawanyo sawia kwa kadri ya mahitaji ya maeneo na halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia lipo tatizo kati ya taasisi za Serikali, pale ambapo taasisi moja inakwenda kutekeleza mradi lakini inakwamishwa na taasisi nyingine kwa sababu taasisi haziongei lugha moja.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:**Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Taarifa.

**T A A R I F A**

**NAIBU WAZIRI,OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:**Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa Mheshimwa anayechangia kwamba ndani ya Serikali sasa tunao mfumo ambao unaweza kukupa taarifa za watumishi wa Serikali katika kada zote katika mikoa yote na kwa idadi yao na mahali walipo. Kwa hiyo anapozungumza kwamba Serikali haina taarifa hiyo sio jambo sahihi na ningeomba atoe maneno yake hayo katika taarifa yake.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kandege; hiyo ilikuwa ni taarifa au? ulikuwa umeomba taarifa wewe.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mimi naamini alikuwa anachangia na kama hilo ndio ukweli maana yake hatutarajii hawa ambao naambiwa wako Dar es Salaam wanafanya kazi ambayo haihusiani wangeweza kuwa hapo. Tulitarajia kama ndivyo hivyo basi wangepelekwa maeneo ambayo wanatakiwa kwenda kufanya kazi ili *productivity* yake iweze kuonekana, hiki ndicho tunachokisema. Kwa hiyo kama wanataarifa ambazo hawazifanyii kazi basi hazitusaidii. Ni vizuri ifike pahali ambapo taarifa hizo walizonazo wazifanyie kazi ili haya mapungufu ambayo tunayasema tusiyaseme tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uratibu wa shughuli za Serikali. Nilikuwa nimeshaanza kuelezea kwamba taasisi za Serikali haziongei lugha moja. Nitatolea mfano; pale ambapo *REA* wanataka kupeleka umeme eneo "X" lakini wanakwamishwa kupitisha umeme kwa sababu kuna msitu ambao *TFS* wanasema hawawezi kupitisha. Tafsiri yake ni nini mradi haufiki kwa wanachi ilhali wananchi wanataka maendeleo yaonekane.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hiyo haitoshi unaweza ukachukulia mfano mwingine, *TARURA* wanajenga barabara, wakimaliza kujenga watu wa maji wanakuja kuchimba barabara ambayo imejengwa na *TARURA as if* hawakujua mradi huu unafanyika lini waka *coordinate* ili kama ni maji yakatangulia barabara ikafuata, haya ndiyo tunayosema. Kwa hiyo ni vizuri taasisi za Serikali zisomane ziseme lugha moja ili wananchi watuelewe kwamba hiki kinafanywa na Serikali, isije ikaonekana kwamba ndani ya Serikali taasisi zenyewe zinakuwa zinakinzana…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kengele ya pili.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono.

**NAIBU SPIKA:**Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, jiandae Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, jiandae Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo, Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo. Hayupo?

**MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID**: Mheshimiwa Naibu Spika,ahsante na mimi kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia kwa jioni hii ya leo. Kama hukumshukuru

binadamu mwenzio kwa analolifanya basi hata Mwenyezi Mungu huwezi kumshukuru. Katika vitabu vya Quran mwanamke ametajwa mara tatu. Nichukue nafasi hii kwa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Dkt. Samia Suluhu Hassan anafanya mambo makubwa sana. miaka miwili tu lakini ameitumikia nchi hii kwa nguvu zake zote kwa sababu anahofu ya Mungu, Mama Samia ni mcha Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mama Samia amefanya miradi mingi katika nchi hii kama vile barabara, skuli na miundombinu mbalimbali. Sisi hapa Wabunge tumetoka kwenye majimbo ambayo haya hatukuyaanza sisi, wapo wenzetu walipita. Sasa, kuna miradi walitengeneza Wabunge wenzetu waliopita lakini sisi hatukuiendeleza miradi ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mama Samia mtangulizi mwenziwe aliyepita amefanya miradi mingi sana na miradi ile yote haikukamilika, lakini Mama huyu alivyokuwa ni mcha Mungu na ana hofu ya Mungu miradi hii ameisimamia kikamilifu na bado anapambana nayo, na Mungu ndiye atamlipa. Kwa nini akasimamia miradi hii, ni kwa sababu ni kodi za wananchi, ni pesa za wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Samia anafanya mambo makubwa sana, hata mazungumzo yake anapoyazungumza ni maneno laini yanamtoka ndani ya mdomo wake. Ni mama mmoja mwenye sura ya tabasamu muda wote, hata akikasirishwa basi yeye bado ametabasamu, huyu ni mcha Mungu wa kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge hususani wanawake Rais wetu ni mwanamke. Tulikuwa tuna nyimbo tunaimba mwanamke kuwezeshwa, lakini sasa mwanamke hawezeshwi mwanamke anafanya mwenyewe. Mama Samia anakwenda kila pembe kila na kwenye kila kichochoro. Mama huyu ni mcha Mungu, hata ukimtazama

kwenye kipaji chake cha uso, ni mcha Mungu. Anapokwenda popote hatoki mtupu lazima atakuja na kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mama Samia Miradi aliyoiacha Mheshimiwa Magufuli ameiendeleza. Sisi Wabunge humu tuseme Wabunge wangapi miradi tuliyoikuta ya wale Wabunge wetu watangulizi waliopita tumeiendeleza? Tukifika tunaanza miradi mingine mipya lakini ile tumeiacha. Mcha Mungu huyu ameendelea kufanya kazi, kuwatumikia Watanzania. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge wanawake tusimame na Mama Samia Suluhu Hassan, tumuimbe Mama Samia Suluhu Hassan, tumpigie makofi Mama Samia Suluhu Hassan, tumwombee dua Mama Samia Suluhu Hassan. Vile vijineno vijineno tuachane navyo, tuvipuuze, hususani wanawake Mama Samia ametubeba, ametupa uhuru, muda huu mwanamke tulikuwa tunaidai asilimia 50 sasa imetimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba wanawake tumsafishie njia Mama Samia Miaka mitano, miaka miwili amefanya mambo haya miaka mitano ijayo atafanyaje? Nakuombeni Watanzania maneno yanayozungumzwa mengine yapuuzeni, Mama anapambana, ni mwanamke, amezaliwa na mwanamke, lazima tumuunge mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mama Samia anapokwenda kuzunguka anachokileta anakileta kwa maendeleo ya Watanzania sote. Hawaletei watu wachache kama wakitumie wao peke yao, ni cha kwetu sote, lazima tumuunge mkono, tumpe nguvu Mama yetu, tumpe nguvu Rais wetu, tumpe nguvu Shujaa wetu hususan wanawake. Wanawake huu ni muda wetu, huu ni wakati wetu, wanawake lazima twende kifua mbele. Mama ni shujaa, Mama ametuwezesha, anaposafiri kwenda nje haendi kuzungumza na makapuku, anazungumza na wanaume, walioshiba, anazungumza nao na wanamwelewa akirudi

anarudi na chochote. Nawaomba Watanzania Mama Samia amefanya mambo makubwa, ni mwanamke lakini anapambana, anaitetea nchi na kumtetea mwanamke. Mama Samia anamtetea mwanamke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumze suala lingine kuhusu mwanamke. Mwanamke ni nguvu kazi ya Taifa letu, leo mwanamke huyu tunayesema ni nguvu kazi ananyanyasika, anadhalilika, wanawake wamekuwa wanauliwa kiholela, Ofisi ya Waziri Mkuu walisimamie suala hili. Wanawake wanauliwa sana. Hivi karibuni tuliona mwanamke, mumewe ni Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji, baba ametoka nyumbani, anarudi mke wake ameuliwa. Juzi mwanamke ni Mhasibu amepigwa mpaka amechomwa moto. Kwa kweli inasikitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanamke ni Taifa kubwa, mwanamke ni kila kitu, naomba Ofisi ya Waziri Mkuu ilisimamie suala la haki za mwanamke. Mama yetu anatutetea sana wanawake, lakini bado mwanamke hatujamsimamia. Waheshimiwa asilimia kubwa Wabunge humu waliopita walikuwa ndugu zetu *albino* wanateseka, wananyanyasika, lakini Serikali hii ilisimama na kuwatetea ndugu zetu wale *albino* na liliisha. Kwa nini lisiishe suala hili la mwanamke kunyanyaswa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini lisiishe mwanamke kuuliwa? Kwani sasa hivi wanawake wengi tunasoma kwenye mitandao wanawake wanapata matatizo, wanauliwa wengi sana. Je, wale waliokuwa hawatangazwi kwenye mitandao, ni wangapi? Naomba sana Serikali, chonde chonde tusimame na mwanamke, Rais wetu ni mwanamke na sisi wanawake ni jeshi kubwa, tumpambanie Mama Samia miaka mitano tena ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Paresso na Mheshimiwa Ntara, Mheshimiwa Mwakamo na Mheshimiwa Tadayo wajiandae.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hoja iliyopo mbele yetu kuhusu hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyoiwasilisha hapa Bungeni. Nianze kwa maneno ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba nchi yetu imejaliwa au imebarikiwa rasilimali nyingi na za kutosha na tuna utajiri wa kutosha sana. Imekuwa tu ni bahati mbaya rasilimali na utajiri tulionao unatumika vibaya na unatumika kwa wachache na walio wengi hawanufaiki na rasilimali. Ni vema tukatambua na tukakumbushana kwamba hii Nchi ni ya Watanzania wote, hii nchi sio ya watu wachache. Vile vile ukitaka kujua jinsi gani nchi hii inaliwa, ripoti ya *CAG* imeonesha ubadhirifu mkubwa, matumizi makubwa na mabovu ya rasilimali fedha za Watanzania na ufisadi, upigaji wa dili na kila kitu umeoneshwa katika ripoti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tukitaka kumsaidia Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ni lazima kwa wale wote ambao wamehusika kwa namna moja ama nyingine tuone neno uwajibikaji kwa vitendo. Bahati mbaya sana neno uwajibikaji halijawahi kutokea ila tumezoea mpaka tuone tumetenguliwa, tumepangiwa kazi nyingine, tumeondolewa lakini haijawahi kama ni mtumishi kama ni kiongozi akawajibika. Kama tunampenda Mama Samia waliohusika kwa namna moja ama nyingine wawajibike katika nafasi zao. Vile vile tunataka rasilimali za Watanzania, fedha za Watanzania ziwafaidishe Watanzania wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza ukashangaa na kujiuliza…

**MHE. CATHELINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa,

**MHE. CATHELINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuzingatie kanuni, muda wa kujadili taarifa ya *CAG* bado haujafika.

**NAIBU SPIKA:** Huo ndio ukweli lakini, kwa sababu *CAG* ame-*cite* mapungufu aliyoyaona yeye, yanakuja Bungeni, sasa Bunge ndilo lenye kuamua baada ya kuhoji pande zote. Kila Mtu ana haki ya kusikilizwa, sasa kama mnafurahi tu kwenda kuwachanganya wananchi, hii sio sahihi. *(Makofi)*

Endelea na mchango wako.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Sasa bahati mbaya sana pia badala ya kuisaidia nchi hii tukiwa tunajificha kwenye taratibu na nini nadhani sio sahihi. Ndio maana kama tungekuwa tunataka kweli kumsaidia Rais hata haya mambo tungeyajadili kwa dharura. Ni kiasi kikubwa cha fedha kimeonesha ubadhirifu mkubwa. *Anyway,* utaratibu upo lakini mwisho wa siku ni lazima tutafakari na kufanya maamuzi kwa maslahi mapana ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nifanye *reference* hapa kwa sababu kufanya *reference* haikatazwi na ikishaletwa hapa, maana yake *it is a public document* na ipo kwenye mitandao na iko kila mahali. Saa unaweza ukajiuliza, tunatumia fedha nyingi kuhifadhi vyura Marekani badala ya kumhudumia Mama wa Kitanzania ambaye anaenda kujifungua leo. Inasikitisha yaani nini kipaumbele chetu cha kwanza kwa Mtanzania? Kwa hiyo ni mambo kama haya na mengine mengi sasa wakati ukifika tutajadili kwa undani zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ulikuwa ni utangulizi, sasa nijikite kuchangia kwenye Sekta ya Ardhi. Ardhi ni mtaji, ardhi ni rasilimali muhimu sana na tuna bahati kama nchi tuna ardhi ya kutosha na nzuri ambayo inafaa kwa matumizi mazuri. Ardhi yetu ni lazima ipangwe, ipimwe na kumilikishwa na lazima tutambue kwamba ardhi haiongezeki lakini mahitaji ya ardhi yanaongezeka na watu ambao wanahitaji ardhi wanaongezeka. Sasa ni lazima Serikali iweke mipango mizuri ya kuhakikisha masuala ya upangaji wa ardhi, umilikishaji wa ardhi na matumizi ya ardhi kwa ujumla yanafanyika kwa wakati na yanatiliwa msisitizo wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali iliyoko sasa hairidhishi na haiendani na uhitaji na bahati mbaya sana takwimu zinaonesha toka tumepata uhuru kati ya vijiji 12,319 ni vijiji 2,600 tu ndivyo ambavyo vimepimwa kwa matumizi bora ya ardhi, toka tumepata uhuru mpaka leo tunapoongea. Sasa ni vizuri sana tukaweka fedha za kutosha kuhakikisha kama tunaweka mkazo wa kupima ardhi yetu ya vijiji tunavipima kweli kweli, kama tunapima kwenye haya maeneo mengine, tunapima. Kwa hiyo, kwa kufanya hivyo maana yake tutapunguza kwa kiwango kikubwa migogoro ya ardhi. Kwa hiyo, tujikite katika kupanga matumizi bora ya ardhi, tusijikite katika kutatua migogoro, tukipanga tutapunguza migogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunaona Kamati ya Mawaziri inazunguka nchi nzima, ile ni gharama, wanatumia fedha, wanatumia gharama kubwa, lakini kama tungewekeza katika kupanga tungepunguza haya mengine ambayo yanajitokeza leo. Kama haitoshi kati ya mwaka 2013 mpaka mwaka 2022, Serikali ilipanga kurasimisha maeneo 2,348,000 ili wapatiwe hati, lakini mpaka leo mwaka 2022 ni takribani miaka nane, ni maeneo 171,210 ndio peke yake yamerasimishwa na yakapewa hati. Miaka 8 tumeweza kurasimisha kwa asilimia saba tu. Sasa tutegemee ni kwa kiwango gani tutafikia kurasimisha kwa kiwango kikubwa ardhi yetu? Ardhi yetu ndiyo mtaji wetu, ardhi yetu ndiyo

rasilimali yetu Watanzania. Kwa hiyo, ni lazima pawepo na msisitizo wa kuhakikisha ardhi hii ya Watanzania inapimwa kwa kadri ya mahitaji na kulingana na soko lilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haitoshi mwaka 2012, Serikali ilitarajia kutoa hati miliki 1,638,000, lakini kwa mwaka huo tu waliweza kufanikiwa kutoa hati 643,000. Sasa kama nilivyoeleza kwa kutumia ardhi hii tu Serikali ingeweza kupata mapato ya kutosha sana. Kwa hizi hati ambazo zimetolewa 643,000 ukichukua kiwango cha juu kabisa ukasema kila mwenye hati alipe angalau Sh.120,000 ya kodi kwa mwaka, maana yake Serikali ingepata mapato ya Shilingi Bilioni 77.2 kwa hati hizo chache tu. Vipi kama tukiweza kupima ardhi nzima ya Tanzania tukatoa hati, wenye hati wakailipa kodi kwa wakati? Kwa hakika Serikali ingeweza kupata mapato ya kutosha na yale mahitaji ya msingi ya Watanzania yangeweza kuwafikia kwa wakati na lakini kuhakikisha tunadhibiti ufisadi na mianya yote ya upigaji. Maana yake tungeweza kutengeneza namna bora ya kupata mapato halafu tukatengeneza na namna nyingine ya kupiga mapato haya bila kuwafikia watanzania kwa ujumla. Kwa hiyo haya ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kama haitoshi, kuna maeneo makubwa ambayo yanaitwa kwa majina tofauti tofauti. Mfano sisi kule Kaskazini, tunaita mashamba makubwa ya Wawekezaji, kuna mashamba ya *settlers,* maeneo mbalimbali nchi nzima. Hao wamekuwa wakimiliki ardhi kwa muda mrefu wana *lease* ya miaka 99, wengine wamelimiliki toka wakati wa ukoloni mpaka leo, lakini wapo wengine ambao wanabadilisha matumizi ya ardhi hii bila kufuata utaratibu. Wako wengine ambao wametekeleza mashamba haya, wako wengine yaani inakuwa ni marufuku kuingia kwenye haya mashamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano maeneo ya kaskazini, maeneo ya Meru kule, Maeneo ya Karatu, haya mashamba

wanaomiliki wameacha mapori, wanyama wanajihifadhi humo, wananchi wanateseka katika nchi yao wakiwa wanaenda, mfano mmoja, kwenye shamba mojawapo katika Wilaya ya Karatu, mwekezaji ameacha pori, hilo pori wananchi wanapita kwenda kupeleka watoto shuleni. Juzi kati hapa mama ameuawa na mbogo akiwa anampeleka mtoto shuleni asubuhi, lakini eneo limeachwa ni pori linahifadhi. Halmashauri haiwezi kufanya kitu, Mwekezaji anasema ni mali yake ndiye ameamua hivyo kwa sababu ana hati. Haiwezekani lazima ifike mahali tuwaonee huruma Watanzania, lazima ifike mahali haya mashamba ambayo kwa namna moja ama nyingine hayajaendelezwa yafutiwe umiliki Watanzania wagawiwe ardhi hii waweze kuyaendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema watu wanaongezeka, mahitaji yanaongezeka, ardhi ni ile ile haiongezeki. Kwa hiyo, tuweke msisitizo katika kupima, kupanga na hatimaye kumilikisha kwa maslahi mapana ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ya mwisho, suala la utawala bora. Suala la utawala bora hasa kwenye halmashauri zetu na kwenye wilaya zetu kuna changamoto kubwa…

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tungepunguza mazungumzo, tupunguze mazungumzo.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunategemea kuona utawala bora ni utawala unaofuata sheria, lakini kwenye maeneo yetu, utaratibu na jinsi ambavyo sheria na kanuni inataka, ni kuwepo na Mikutano Mikuu ya vijiji, kuwepo na usomaji wa taarifa ya mapato na matumizi, huo utamaduni uliishakufa na uliishapotea hakuna. Baadhi ya Wenyeviti wa Vijiji, Watendaji wetu wa Kata na Watendaji wetu wa Vijiji kule wamekuwa Miungu watu, yaani

wao ndio wanafanya kila kitu, wao ndio watatengeneza michango, watakusanya wao, watapangia matumizi wao, watawatoza faini wananchi, watawaweka kwenye *lockup* zao wanazozijua. Hatuwezi kuwa na nchi ya namna hii…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** kengele ya pili.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** …tunataka utawala wa Sheria na utawala bora ufuatwe…

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili, ahsante.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ntara, wajiandae Mheshimiwa Mwakamo na Mheshimiwa Tadayo.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nianze moja kwa moja kwa kuipongeza Serikali ya Awamu ya Sita hasa kwa eneo kubwa kabisa la suala la mikopo. Sasa hivi hali imetulia, wanafunzi wametulia, angalau zile *Message* za mikopo zimepungua. Jambo kubwa sana limefanyika na Serikali hii, lakini bado niombe Serikali hao wanafunzi wa vyuo vya kati, naomba Serikali wajipange safari hii, hatutaki kelele za hao wanafunzi wa vyuo vya kati nikiwa na maana vyuo vya ufundi, maeneo ya afya na maendeleo ya jamii, hata wao waweze kupata mikopo. Tukifanya hivyo tutawasaidia sana watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye suala la maadili. Leo kwa mara ya kwanza nimefurahi sana kuona baadhi ya Wabunge hasa wanaume akiwemo Mheshimiwa Sanga na

Saashisha wanalizungumzia suala hili la maadili na hasa katika maeneo ya kuona watoto wetu na hasa wa kiume wanafanyiwa mambo ambayo hayafai.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ifike wakati Serikali ilete Muswada hapa ili kuweza kuwa na sheria kali na sheria kali hizi hatutakuwa sisi wa kwanza. Tunaogopa, mtu akinyongwa tunasema haki za binadamu, lakini huyu mtoto anayelawitiwa hana haki? Tulete sheria niwaombe Wabunge jamani tusimame wote kwa umoja wetu, Serikali walete Muswada hapa wa Sheria hawa watu wanaofanya hivyo wahasiwe au wawekewe dawa wawe wanapata vifafa, yaani mtu akipata kifafa hata zile nguvu zinakuwa hakuna. Nimwombe sana Waziri wa Afya, wao wnajua hayo mambo ya *chemicals,* watafute dawa hawa watu tuwa-*fix,* kama hatutaki kuwahasi basi tuwape wadudu wale wa kupata kifafa, waendelee kuanguka na kifafa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu gani Waheshimiwa Wabunge? Hiki kizazi ni cha laana, haya mambo wanayofanya ni laana, tukiendekeza kuwaacha nawaambieni wote hapa tutapata laana. Tuondoe hicho kizazi waondoke kabisa na dawa ya kuwaondoa hawa ni kuwahasi tu wasiendelee na ule mchezo mchafu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakuwa na huruma na watu ambao hawana huruma na watoto. Leo hii fikiria una mtoto, wengi hapa mna watoto wadogo, sasa fikiria kama ungemkuta yule mtu anamfanyia mtoto wako kitendo hicho wewe ungefanya nini? Ungemshika hapa umpeleke Polisi? Naamini wengi hapa ungemnyonga pale pale, ungemmaliza. Sasa kwa sababu kunyonga wanasema sijui haki za binadamu basi wahasiwe, vyombo viko hapa wanawakamata wanawahasi huko huko kimya kimya au wanaweka wadudu wa kifafa waendelee ili wasiwe katika dunia hii. Hata hivyo, tukiendelea hivyo hawa watoto

wanafanyiwa toka wakiwa wadogo, basi kundi la mashoga litaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, wako baadhi ya Viongozi sijui ni wapagani, sijui wana dini gani? Ndani ya Makanisa watu wanatetea ushoga, Serikali wanawaangalia tu, kweli jamani? *Clip* zinatoka mtu anatetea ushoga, anasema kwani ushoga ni nini? Si mtu unaamua mwenyewe? Serikali iko kimya, huyu wangemchukua kabisa hapo Madhabahuni anakohubiri ushoga wangemchukua wakamfanyia hicho kitu… *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa mchangiaji kwamba sio sahihi kwamba hakuna hatua zilizochukuliwa. Watu ambao wamefanya hiyo tayari wameshachukuliwa hatua na sheria inachukua mkondo wake na Serikali haitaendelea kuvumilia aina yoyote ya uvunjifu wa sheria za nchi hii. Kwa hiyo naomba nimpe taarifa hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Daktari, taarifa hiyo Waziri mhusika amekupa.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Masauni mimi nakuheshimu sana, sheria hizo zipo, hizo sheria zipo lakini bado siyo kali, ndiyo maana wanaendelea kufanya hayo madudu, leteni sheria tukifanya kwa watu watano, kwanza ukiwahasi unafikiri watatangaza kwamba mimi wamenihasi? Hawawezi! Leteni hapa tutaweka hiyo sheria, kwa nini mnatetea Mheshimiwa Masauni, hivi kweli hawa watoto tunaowazaa kwa uchungu vile wanafanyiwa hivyo? Hapana, hebu tujipange. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusu ndoa za utotoni. Leo hii mimi huwa nashangaa sana, tunakaa hapa ndani ya Bunge tunasema ndoa za utotoni hazifai, ndoa za utotoni hazifai halafu tunajichanganya wenyewe tunasema eti mtoto akishapevuka anaweza akaolewa wakati wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto wa siku hizi wasichana wanapevuka kati ya miaka tisa na miaka kumi. Fikiria una binti yako ana miaka kumi, eti unaenda kumuoza kwa sababu amepevuka, unaenda kumuoza kwa mwanaume mwenyewe ni *giant* natamani kutaja hata majina ya mfano, kweli. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba unilinde mtoto ana miaka kumi, kumi na moja, kumi na mbili kumi na tatu, kumi na nne, unaenda kumuoza kwa mwanamme, mtu kama Festo Sanga. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ni mfano, huyu mtoto anapokwenda pale anaenda kuolewa, anaenda kubakwa?

**NAIBU SPIKA:** *Order please, order.*

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, huyu mtoto anaenda kuolewa ama anaenda kubakwa? Huyu mtoto si atajeruhiwa tu? Zamani watu wanashangaa wanasema zamani…

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Napenda kumpa taarifa Mama yangu pale. Mdogo wangu Festo yupo *under forty* ni mdogo, nadhani ana miaka sijui 32 kwa hiyo huo ni mwili tu usije ukaogopa. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa endelea.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, zamani Mama zetu walikuwa wanaolewa wakimaliza Darasa la Saba. Ni kweli wanaolewa miaka 16, miaka 17, miaka 18 lakini lazima tujue kwamba walikuwa wanamaliza Darasa la Saba au Darasa la Nne hana pa kwenda. Hakuna *VETA*, hakuna shule za sekondari, leo hii kuna shule za sekondari kibao, kuna *VETA*, watoto wamalize Darasa la Saba waendelee na masomo. Niwaambie ukweli hata wale wazazi wetu walivyokuwa wanaolewa zamani wakiwa wadogo wengi wao ukiwauliza wanasema mwanangu tulikuwa tunaolewa ni mateso matupu, wala tulikuwa hatufaidi hayo maisha ya ndoa, kwa sababu kibinti kinaolewa kidogo kwa hiyo kinakwenda pale kinanyanyasika, kilichokuwa kinatokea pale ni *sexual abuse*! Sasa wewe leo unasimama mahali unahutubu unasema eti mtoto akishapevuka akaolewe!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge muda wako umekwisha.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa namuita Mheshimiwa Michael Mwakamo ajiandae Mheshimiwa Tadayo.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi jioni ya leo kuwa mmoja wa wachangiaji. Ni kweli muda wa kupongeza unakula muda wa kuchangia lakini ni hakika kabisa katika Bunge hili kwa namna ambavyo Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano anatekeleza majukumu yake tunazo kila sababu ya kutumia dakika chache za kuchangia tunazopewa kumshukuru yeye na Serikali yake kwa mambo mbalimbali makubwa anayoyafanya kwenye nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa kuchangia hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu, nami nitachangia eneo moja dogo sana la kukuza uchumi kwenye nchi hii. Kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ametuonyesha namna ya hali ya ukuaji wa uchumi duniani na katika nchi yetu, amejaribu kutaasa na kutuambia kwamba inakadiriwa itakapofika 2023 uchumi wa dunia utashuka kwa asilimia 2.9 kutoka asilimia 3.4 ya mwaka 2022. Ameweza kutueleza pia kama nchi mwaka 2022 uchumi ulikuwa asilimia 5.2 na unakusudiwa kuongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko hili la kiuchumi ambalo linaonesha katika taarifa ya nchi yetu na ukiangalia ongezeko la kidunia linaloonesha kwamba uchumi unakadiriwa kushuka isitupe faraja kwa sababu katika nchi yetu zipo changamoto mbalimbali ambazo zinaashiria kwamba tunakoelekea hali ya kiuchumi pia inaweza ikawa mbaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya jambo ambalo nina wasiwasi nalo, leo hii katika Majimbo mbalimbali nchini idadi ya tegemezi nchini inakuwa kubwa sana na utegemezi huu unasababishwa na mambo mbalimbali, moja hali ya hewa katika maeneo mengi ambayo kilimo kilikuwa kinachukua nafasi hali ya hewa imebadilika wakulima wengi hawalimi, kwa hiyo inatokea sasa wananchi wengi wanaelekeza nguvu

zao kuwategemea ndugu zao wachache wenye kipato kidogo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa kukataa maelekezo ya Kiti ni utovu wa nidhamu, Kanuni ya 84 na inaweza ikampotezesha mtu mambo magumu sana, endelea Mheshimiwa Michael.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, nilikuwa nasema kwamba pamoja na takwimu ambazo tumezipata za kuongezeka kwa hali ya uchumi nchini lakini hali halisi kwenye Majimbo na kwenye nchi yetu tegemezi wanaongezeka kwa kiasi kikubwa sana, utegemezi huu unasababishwa nimesema na mabadiliko ya hali hewa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikoa mingi ambayo wakulima walikuwa wanatumia kilimo kama moja ya chanzo cha kujipatia mapato na kukuza uchumi wao, hali ya hewa imepelekea kubadilisha hali hiyo na watekelezaji na mavuno yanakuwa machache kitendo ambacho kinapelekea sasa watu wengi kuwategemea ndungu zao wachache wanaoingiza vipato kwa njia nyingine ambazo zinaweza zikapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni moja ya athari zinazopelekea kuona kwamba hata wizi kwenye taasisi mbalimbali unaongezeka, watumishi wengi wa umma kwenye taasisi mbalimbali wanawategemezi wengi nyuma yao na yote yanasababishwa kwamba hao wanaowategemea wengi hawana shughuli za kufanya, kama alikuwa mkulima ameshindwa kulima kutokana na hali ya hewa, ameshindwa kulima kutkana ana mogogoro ya wakulima na wafugaji, ameshindwa kulima kutokana na sheria nyingi za matumizi ya mabonde kutokutumia maji ya umwagiliaji, ameshindwa kulima kwa sababu ya kukosekana miundombinu ya kilimo kwenye maeneo mbalimbali nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri Serikali ijielekeze kuangalia ni namna gani italiondoa hili wimbi kubwa la watu kuwa tegemezi na njia pekee ya kuliondoa wimbi kubwa la watu kuwa tegemezi ni kufungua miundombinu ya kuwafanya watu hawa waweze kuwa wazalishaji na wanaweza kuwa wazalishaji kwenye sekta ya kilimo na kwenye taasisi mbalimbali ambazo wanaweza wakapata ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote hapa ni mashahidi nchi yetu leo inaongoza kwa ujenzi wa viwanda, Mkoa wa Pwani ambao natokea ni moja ya Mikoa ambayo ina viwanda vingi vya kutosha. Tujiulize viwanda hivi ambavyo vimejengwa katika maeneo mbalimbali nchini vinalipa kiwango gani cha mishahara kwa Watanzania. Sasa kama wananchi ambao wanapata nafasi wachache kuajiriwa kwenye viwanda hivi ambavyo vimejengwa mshahara wao hauendani kabisa na hali ya uchumi mtaani, nini kitatokea? Ni lazima wapo watakaoshindwa kumudu kufanyakazi, matokeo yake wataachakazi na wataendelea kuwa tegemezi kwa ndugu zao wachache wenye kipato kwa njia moja au nyingine.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tunaona tuna maeneo mengi na mabonde mengi ambayo yanastahili kwa kilimo. Tujiulize mabonde haya yamewekezwa kwa kiwango gani na Serikali ili wananchi wengi wanaoyazunguka mabonde hayo watumie hayo mabonde na maji yaliyoko kwenye maeneo hayo kufanya uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishauri sana Serikali ijielekeze kwenye kuwaongezea wananchi uchumi ili hii takwimu ambayo wana wasiwasi nayo ya kuongezeka au kushuka kwa uchumi na Pato la Taifa kushuka isiwe katika mazingira ambayo tunayazungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo bado tunaona kwamba mfumko wa bei wa bidhaa mbalimbali nchini unapelekea wananchi kushindwa kumudu kugharamia maisha yao ya kawaida. Watumishi wa kawaida ndiyo pale tunaposababisha sasa pesa za Serikali zinakwenda kwenye maeneo hayo kusimamia miradi, matokeo yake wanatokea watu wanaiba! Wanaiba kwa sababu hali ya mtaani ya bei haifanani na kipato chake cha mwezi anachofanya yeye na wale tegemezi alionao. Ni vema Serikali ikajielekeza kwenye namna bora ambayo inaweza ikawaondolea watu wake hali ngumu ya kiuchumi ili waweze kuhakikisha kwamba mambo mbalimbali yanakwenda.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefanya ziara Wajumbe wako wiki moja, wiki tatu zilizopita wengi walikuwa kwenye Kamati zao, tumetembea kwenye maeneo mbalimbali kukagua miradi mbalimbali. Kwa kuwa, Ofisi ya Waziri Mkuu ndio inasimamia utekelezaji wa majukumu ya Serikali katika nchi hii tuifahamishe tu kwamba hali ya miradi mingi nchini ni tete. Usimamizi wa miradi katika maeneo ambayo watu wengine tumeyakagua haiko vizuri, haiko vizuri kwa sababu pesa za miradi zilizopelekwa hazikufanya kazi za tija na ndiyo hii ambayo leo watu wanashindwa kujizuia hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii kila mtu anaesimama anajaribu kupata nafasi ya kuijadili hotuba ya *CAG* na hii inafanana na mtu mwenye kikohozi, kikihozi huwezi kukizuia kinakuja kutokana na hali uliyonayo kwa wakati husika. Wabunge wanapata hamu ya kuichangia hiyo ripoti wakati wakifahamu muda bado kutokana na hali ya taarifa ilivyo na inasababishwa na hali ambayo inaonekana, wameiona kwa macho kwenye ziara, wameiona kwenye taarifa za *CAG,* kwamba usimamizi wa miradi kule hauko vizuri, miradi imepigwa, unakuta mradi una-*phase* mbili mpaka ya tatu lakini *phase* ya kwanza haijaisha, yote hii inasababishwa na usimamizi mbovu, inasababishwa na wizi ambao umefanywa na wasimamizi ambao wapo kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasemekana ni vibaya kuwaaambia wizi leo kwa sababu wakati bado lakini lazima tuseme kwamba hali ni mbaya lakini katika sehemu mbalimbali inaonekana hali mbaya hii inasababishwa na huu utaratibu wetu wa *force account*. Tuiangalie hii *force account*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona kama ni njia mojawapo nzuri ya kupunguza gharama za miradi lakini kiukweli hali halisi gharama za miradi hazipungui kwa sababu kila sehemu ambako pesa zimepelekwa bado Wakurugenzi, Wasimamizi wa miradi hiyo wanaomba pesa za ziada.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge ahsante.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa ahsante, sasa namuita Mheshimiwa Tadayo na ndiyo mchangiaji wetu wa mwisho.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kufunga dimba la uchangiaji jioni hii. Awali ya yote kama ambavyo wachangiaji wenzangu waliotangulia walivyosema mimi kwa kweli naishukuru sana Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kazi nzuri na kubwa wanayoifanya ya kumsaidia Mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa majukumu haya ambayo tumemtwisha ya kuiongoza nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi yote hii inayotekelezwa pamoja na kazi nyingine ambazo Mheshimiwa Rais anatuongoza vizuri, uratibu wake unafanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa hiyo tuna kila sababu ya kumpongeza na hata kwenye taarifa yake tumeona jinsi ambavyo miradi hii ya *SGR*, Bwawa la Mwalimu Nyerere, *ATCL*, Bomba la Mafuta,

madaraja makubwa na kadhalika yanavyokwenda ni chini ya uratibu wake, anaziratibu hizi Wizara anazosimamia, kwa hiyo lazima tumpongeze kwa kazi nzuri na pia tumemuona akitembea huko na huko akikerwa na kutoa maelekezo mbalimbali juu ya miradi inayosinziasinzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa miradi hii unachangia pia katika kuongeza mzunguko wa fedha katika nchi yetu, ndiyo maana kuna umuhimu wa kuhakikisha kwamba miradi hii inatekelezwa mpaka ifikie mwisho ndiyo kazi kubwa iliyoko mbele sasa hivi ya kuhakikisha kwamba miradi hii inakamilishwa. Pamoja na kukamilishwa vilevile tuwe mstari wa mbele katika kusimamia haya makandokando yanayojitokeza kama haya yanayotokea kwenye ripoti ya *CAG* yanayotusumbua sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kama basi kweli muda wa kikanuni haujafika wa kujadili lakini nadhani wakati mwingine tunaiogopa hii taarifa kwa kudhani kwamba labda taarifa ya *CAG* ni kitu hasi, tuichukulie *positively*, ni kitu chanya kwamba angalau sasa tuna mifumo ambayo inaweza ikatuambia nini kimetokea, sasa unapotuambia nini kimetokea na kinajadiliwa mitaani hatuwezi kufumba midomo kabisa. Lazima tufike mahali tutaje na zipo namna nyingi za ku-*justify* mjadala huu katika kipindi hiki hatuwezi kukaa jambo linajadiliwa na wananchi huko sisi tukakaa hapo kimya kana kwamba siyo sehemu ya nchi hii, hilo nadhani tuwekane huru kuligusia wakati tunachangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee kuhusu Jimbo langu la Mwanga. Wananchi wa Mwanga wanaishukuru sana Serikali ya CCM chini ya Mama Samia Suluhu Hassan, miradi mingi sana imetekelezwa kuanzia miradi ile ambayo tulikubaliana kama Mwanga kwamba ni miradi ya kimkakati, kama ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ambao unakwenda vizuri kabisa kwa kasi, ujenzi wa barabara *bypass* kilometa 13.9 tutakayoita Msuya, ujenzii wa chuo cha *VETA*, ujenzi wa jengo

la utawala la Halmashauri, pamoja na ahadi ya Mheshimiwa Rais ya stendi ya kisasa ambayo hii kwa kweli haijafikia mahali pa kuridhisha na ndiyo maana nahitaji hapa kuwakumbusha wanaohusika kwamba Mheshimiwa Rais aliwaahidi wananchi wa Mwanga kwamba watapata stendi ya kisasa na utekelezaji ulianza katika maana ya kutakiwa kupeleka andiko na michoro, yote haya yalifanyika lakini kuna mahali pamekwama ambapo ningeomba sana kwamba pakwamuliwe ili mradi ule utekelezwe.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *specifically* kwa mradi unaowagusa wananchi kama mradi wa hospitali ya Wilaya tunaomba sasa tupatiwe zile fedha zilizobakia Shilingi Bilioni 1.3 na Watendaji wangu, Wataalam wangu wa Halmashauri na Baraza langu la Madiwani ambao kila siku namuombea Mungu awabariki na kuwalinda, wameniahidi kabisa kwamba wakipata fedha hizo za mwisho bilioni 1.3 ukifika mwisho wa mwaka huu tutaanza kuomba vifaa ili tuweze kutoa huduma zile za msingi pale za *OPD* na baadhi ya huduma za kulaza. Tuko kwenye jengo la mionzi sasa hivi tunaomba Wizara husika isituangushe kwa fedha zilizobakia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa vituo vya afya tumeendelea vizuri. Tuna vituo vya afya vya kimkakati vipya vitatu na vile vya zamani ni vitatu jumla vituo vya afya Sita. Vituo vyote vinakabiliwa na changamoto inayofanana ya watumishi wa afya pamoja na vifaatiba. Nilipochangia mara ya mwisho kwenye ripoti ya *LAAC* nilitoa takwimu ya mapungufu tuliyonayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie Kituo cha Afya cha Kata ya Lang’ata ambacho kwa kweli kimechakaa sana, tunaomba kituo hiki kikarabatiwe ili kiweze kutoa huduma katika viwango vya vituo vya afya vilivyokusudiwa kwa sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti hii tulipaswa kupata vituo viwili vya afya vya kisasa, kimoja tumepata kwenye Kata ya Kirya ambacho ni Kituo cha Afya cha kisasa kabisa, kinahudumia mpaka watu wa kutoka kwa rafiki yangu *Senior Brother* hapa Mheshimiwa Ole-Sendeka kule Simanjiro pia kutoka Same wanapata huduma pale. Pia kile kituo kingine ambacho kilipaswa kujengwa bado hakijapata fedha tunaomba tupate fedha kwa ajili ya kituo hiki cha afya cha pili ili mpango ule na ahadi ile iweze kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miradi ya elimu, tuliahidiwa kupata shule mbili kwenye Kata zile mbili ambazo zilikuwa hazina shule. Bado Kata moja ya Toroha haijapata shule yake pamoja na kwamba tulifikia mahali kabisa mpaka pa kuwa *requested bank account* ili fedha ziingie lakini hapo palipokwama sasa tunaomba pakwamuke ili fedha ziweze kupelekwa wale wananchi wangu ambao wengi wao ni jamii ya wafugaji waweze kupata shule. Shule ambayo tumeipata moja ya Kivisini imekamilika vizuri na tumekusudia kuifanya moja kati ya shule zetu bora kama ilivyo shule ya Dkt. Asha Rose Migiro, Shule ya Kamwala na Shule ya Usangi 'A' ambazo ni moja ya shule bora Kimkoa na Kitaifa zinazotokea pale Wilayani kwetu Mwanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna tatizo kubwa la Walimu. Suala la ajira ya Walimu ni tatizo kubwa sana. Juma lililopita tulikuwa tunafanya tathmini ya kila Mwalimu jinsi ambavyo ame-*perform* na alivyofaulisha kwenye somo lake, wako Walimu wa kujitolea ambao hawalipwi chochote lakini wameongoza katika kufaulisha masomo yao. Walimu kama hawa zawadi pekee ya kuwapa ni kuwajiri kwa kweli katika shule hizi. Vinginevyo wapo ambao wamejitolea muda mrefu ninaogopa wanaweza wakafikia umri wa kustaafu kabla hawajaajiriwa halafu wakapoteza kila kitu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la maji. Ipo miradi mingi lakini kwa kweli kasi ya miradi ya maji

haijaridhisha bado. Mheshimiwa Waziri wa Maji juzi alikuja nilimweleza hili jambo, kubwa kuliko yote ni shukrani kubwa sana kwa Serikali kwa ajili ya mradi mkubwa wa maji wa Same - Mwanga - Korogwe ambao utalisha maji katika Wilaya ya Mwanga eneo lote la tambarare Same mpaka Korogwe, huu ni mradi mkubwa sana wa Shilingi Bilioni 262. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais mradi huu ulikwama kwa muda mrefu lakini mwezi uliopita alikuja Mheshimiwa Waziri wa Maji akakwamua mradi ule tukasaini *restatement agreement* na kuahidiwa kwamba ndani ya miezi 14 maji yatatoka, tunaomba ahadi hii ambayo watu wameichukua kwa thamani sana kwa sababu ni ahadi ya Mheshimiwa Rais ikamilike kama ambavyo imeelezwa pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la barabara linaendelea vizuri lakini kipekee niishukuru Serikali kwa ajili ya usanifu unaoendelea wa barabara inayotoka Kisangara kwenda Nyumba ya Mungu kilometa 17 kwa kiwango cha lami. Barabara hii ni muhimu kwa sababu eneo lile lina miradi mikubwa ya Kitaifa, huku mradi wa umeme ambapo tunachangia kwenye *Grid* ya Taifa na miradi mingine mingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kengele imegonga niseme moja la mwisho iko barabara nyingine ya kutoka Kifaru kutokea kituo cha Ng’ombe kilometa 75, hiyo ni barabara ya mpakani. Kwa hiyo kwa ajili ya umuhimu wake, kwa ajili ya mambo ya usalama na miradi mikubwa ambayo inaendelea katika eneo hili, hii ni barabara inayounganisha Tarafa Tano tunaomba iwe *upgraded* kufikia kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna tatizo kubwa sana la vyanzo vya mapato, vyanzo vyetu viwili vimetelekezwa. Kimoja ni Bwawa letu la Lang’ata ambalo lilikuwa likitoa Samaki na mapato makubwa sana, tunaomba kauli ya Serikali tatizo ni Samaki wamedumaa au tatizo ni mbegu isiyofaa? Mpaka sasa hivi hakuna kauli ya Serikali juu ya

bwawa lile tunaomba lifanyiwe kazi pamoja na suala la magugu maji katika Ziwa. Naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Tadayo kengele ya pili. Waheshimiwa Wabunge wachangiaji wote wamekwisha, naendelea kuwasihi na maneno yetu tunayoyasema yanafika nje kwa wananchi, wananchi hawaelewi taratibu za Bunge, tusubiri taratibu za kisheria za Kibunge za kujadili na kupata taarifa ya Kamati ya *PAC* ambayo ndiyo itakayokuwa na maamuzi baada ya kuhoji watu wote. Ninayasema haya kwa sababu sitaki wananchi wapate taharuki kwa mambo ambayo bado hayajaiva.

Waheshimiwa Wabunge, ninawakumbusha tena futari ni Saa Kumi na Mbili na Nusu, *Iftar* ya *CRDB* na Mgeni Rasmi ni Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wabunge pamoja na Watumishi.

Waheshimiwa Wabunge, ninaahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho Saa Tatu Asubuhi.

*(Saa 12.00 Jioni Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumatano Tarehe 12 Aprili, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*